# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

ORGANISED GROUPS

EMBAKASI CONSTITUENCY,

HELD AT DANDORA KINYAGO SHOOL

(GITARI MARIGU)

ON

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, EMBAKASI CONSTITUENCY, HELD AT DANDORA KINYAGO SCHOOL (GITARI MARIGU) ON 28TH MAY, 2002

**Present**

1. Com. Isaak Lenaola
2. Com. Abdirizak Nunow
3. Com. Salome Muigai

**Secretariat Staff in Attendance:**

1. Solomon Anampiu - Programme Officer
2. E. Wetangula - Assistant Programme Officer–
3. Regina Mwachi - Verbatin Recorder
4. David Muturi - Language Interpreter

Speaker----- Ebu tuanze Mkutano, tafadhali chukua ile microphone utuombee halafu twendelee

**Mrs. Wafula:** Nafikiri sasa tutasimama kwa maombi, kabla hatujaanza, mimi naitwa Mrs. Wafula. Na sasa kila mtu aweke roho yake pamoja, uwache mawazo ya huku na huku tafadhali, haya, tumeinama, asante Baba mwenyezi Mungu muumba Mbingu muumba dunia, tasama wakatu huu tumekuja mbele yako Bwana, Bwana naomba uweke mkono wako hapa katikati mwenyezi Mungu, tasama tunatoa maoni bali bali mwenyezi Mungu, utoe ibilisi abaye anaweza kutatiza mkutano mwenyezi Mungu, Baba odoa mwenyezi Mungu, wakutuhaibisha kwa hii kijiji mwenyezi Mungu, najua hii kijiji inadhalauliwa mwenyezi Mungu, wanasema kijiji ya maofu mwenyezi Mungu haina maana, Baba naomba uyatoe hayo yote mwenyezi Mungu, naomba mwenyezi Mungu tazama, kuna wageni wengine hawajafika Baba, uwaongoze safarini Baba, uwe katikati ya hapa mwenyezi mungu, Baba uongoze kila jambo ambayo lolote kila ambayo tunaenda kutoa kutoka nia vyetu Baba, naipokelewe mbele yako Baba, Baba usituhaibishe katikati hapa, naomba mwenyezi Mungu hawa wageni wametufikia nao Baba, uwe nao pamoja mwenyezi Mungu, uwalinde baba, uwaongoze baba, kwa kila jambo ambayo watasikia baba, isiwe na haya isiwe ya kuwakasilisha Baba, roho mchafu yule atakuwa hapa katikati, naomba kwa jina lako, naomba kwa upendo wako, Baba upate kuwaondoa Baba, Baba usituhaibishe mwenyezi Mungu, naomba mwenyezi Mungu nikililia, uwe hapa katikati tukianza wakatu

huu mpaka wakatu ambao tutamaliza mwenyezi mungu, weka mkono wako katikati hapa baba, baba utulinde, utuongoze baba, mwenyezi mungu naomba, kwa wale wageni hawajaingia, uwaongoze barabarani, wafike hapa mwenyezi mungu kwa neema yako, naomba nikililia, mwenyezi mungu, sisi hatuna uwezo, uwezo unatoka kwako, nguvu inatokoa kwako mwenyezi mungu, naomba hayo machache kwa jina la Bwana Yesu Kristo aombaye kwa mwenyezi Mungu. Amen.

**Commissioner Isaack Lenaola:** Asante Mrs Wafula kwa maombi, ningependa sasa kuwajulisheni wale ambao wametoka tume, kabla kumuita mmoja wa committee yetu katika Embakasi atujulishe wenzake. Wa kwanza ni mwenzangu Commissioner Salome Muigai ambaye yuko kwa mkono wangu wa kushoto. Pamoja nasi pia tuko na bwana Solomon Anampiu, ambaye ni Programme Officer ako pale mbele. Tuko na bwana Emmanuel Wetangula, ambaye atakuwa akiandika reporti ya leo. Natuko na Mrs Regina Mwanchi, ambaye atakuwa akinasa sauti na report ya leo pia, natuko na David Muturi ambaye atakuwa akishuhulikia kazi ya kutranslate kwa wale ambao ni viziwi. Ndio huyu sasa. Sasa mzee juliza committee yako halafu twendelee.

**Raphael Thimbo**: Basi commissioners mlioko hapa, members wa 3Cs mimi kwa majina naitwa Raphael Thimbo, ni mmoja wa 3Cs, ningechukua jukumu hili, nimjulishe macommissioners wale members wa 3Cs ambaye wamefika sasa, pale tuna Justus Kweo, ambaye ndiye Chairman wa 3 Cs hapa, Charity Wangari – mama yuko hapa ni member wa 3 Cs, Mr. Grater, also ni member wa 3Cs, nakuna wengine nafikiri watakuja, so mnakalibishwa ata ingawa watu hawajakuja tumetangaza ya kutosha, lakini waafrika unajua masaa nayo dio hiyo. Wale wamejiandikisha kutoa maoni tutaendelea na tuna hakika watu watakuja - asante.

**Com. Isaak Lenaola:** Asante sana, mimi naitwa Isaak Lenaola, ningependa kuwajulisheni tu njia ya kutoa maoni, jambo la kwanza tuko na hulu kutumia lugha yeyote, lugha ya Kiswahili, lugha ya Kingereza, ama lugha yeyote mtu angetaka kutumia, kwa hivo hakuna tashushu lugha utakatazwa.

Jambo la pili ni kuomba kuwe na heshima katika mkutano – mtu akiwa na maoni angependa kutoa, akumbaliwe kutoa mbila kupigiwa makelele mpaka amalize.

Jambo la tatu tutakuwa tukiketi pale na baada ya kutoa maoni utaenda kujiandikisha kwamba umetoa maoni.

Jambo la nne, mtu akiwa na memorandum tutampa dakika tano aandaze (ku-highlight) ile memorandum yake, mtu kama hana maadishi tutampa dakika kumi azungumze yale angependa kuyasema. Na kufikia hapo nafikili vizuri sasa nimuite mtu wa kwanza ambaye ni Joseph Kimani. Karibu Mzee, jua pale utasema jina alafu uongee nakutoa maoni yako.

**Joseph Kimani**: Kwa jina ni Joseph Kimani, naa-ni sikua tayali kutoa maoni yangu lakini nina mengi yakusema , lakini sikuwa tayali kabisa nilijiyadikisha jina yenyewe, lakini kwa maana nilikuwa nimekuja kusikiza, nii- sikuwa tayali kabisa, lakini sikosi la kusema nikiwa katika nchi yangu maana yake mimi nimezaliwa nchi hii ya Kenya na mengi yamepita kama mimi ni mzee hivi.

Na tangu wakati wetu wa zamani, nilijionea yale yalikuwa maana mimi ni mzaliwa katika Satelight area. Niliona yaliokuwa na wabeberu na yale ya katiba, na hata wakatu huu nimeyaona vile tulianza, tukaanza na mzingi, niliuona vizuri, lakini ukaja ukififia, ukififia, ukififia, na ata wakati huu ata mkitazamia, mtaona tumefifia. Kwa hivyo katiba vile ilitengenezwa ingekuwa ikifanya kazi, tukitazamia kama sasa tulipo hapo, ukitazama ni kama nchi isiyo yetu, ukitazama kama makaratasi ya nylon yamejaa na tuna watu wanaweza kutufundisaha kwa kila jambo ata hali ya kukaa. Na mimi nikiwa mzee namna hivi, naona katiba yetu itengenezwe na iangaliwe, sana sana, iwe ya kibinadamu, kama hapa tuko sasa, tuko na jambo nyingi sana – tuna watoto wale ni watoto wetu na wanaitwa, watu wanawapatiza jina ni chokola – Ni mwanadamu kama mimi, mimi ningeitwa chokola wa kwanza, ata kama ninalala pahari, mana mwanadamu ni mwanadamu na hali ya mwanadamu hakuna mkubwa kuliko mwingine, hakuna mdogo kuliko mwingine, kwa hivyo hakuna chokola, ni mtoto amekosa malezi, na malezi yangetokana na katiba yetu, unaiona, yani kutazamia watoto kama hao, wawe ni juu yao kuangaliwa wa wale wanao uwezo lakini ninaona hakuna jambo hili linafanywa katika nchi yetu na lingetaka lianzwe. Nikiwa mzee kama hivi nilivyo nilikuwa nikifanya kazi, na watu walio wa chini kiwango cha chini sana wamewekwa kiwango cha chini, sana, sana, si kama wanadamu, na mwanadamu ni mwanadamu, isipokuwa hatuwezi kuwa sawa sawa lakini ata vidole tulivyo nazo, si sawa sawa, kuna kikubwa, kuna kidogo lakini hazipitani sana, tubo yetu ile tunayo tunakula chakula hakuna mtu anakula sahani kumi na mwingine sahani moja – kwa hivyo katiba yetu tunataka itengenezwe sawasawa.

Kitu kingine, nasema, tangu commission ianze, mimi nashangaa sana nikisikia hawajamaliza kazi yao, hiyo kwa commissioner nawaambia, si kazi ngumu sana, waikamilishe wakati waliaanze kusema ikamilike. Ata mkiiweka kwa miaka kumi, kama hamwezi kukamiliza, siku mlichokuwa nacho naomba katika commission yetu nawasihi sana waikamilize mapema. Maoni yale yatatolewa na wachache, maana hamuwezi kwenda kila pahali, hamuwezi kwenda kila pahali ama kutoa maoni kwa watu, sasa watu wametangaziwa kama hapa na ninaona ni wachache, sijui ni kwa nini na wametangaziwa, kwa hivyo mkamilize kazi yenu mkijua hii ni kazi ya Mungu mmetumwa kuifanya, si kazi yenu, ni kazi ya Mungu kwa hivyo ningewauliza mikamilize kamili kwa mnda unaofaa ndio tuweze kuendelea vizuri. Wakenya nawauliza muwe watu wa huruma, nyote mkubwa, mdogo na wowote, muwe watu wa huruma, tukiwa na huruma nchi hii yetu, tutaifanya, tumeshidwa wote, mkisema watu fulani wameshidwa, sisi, mimi kwa maoni yangu nasema tumeshidwa, wote, wote tumeshidwa, maana hakuna mtu anafanya kazi yake kama vile inatakikana. Na sitasema mengi maana kuna wengi wanaweza kusema ata zaidi ya mimi. Nasema hivi nikiwa mzee pengine maoni yangu ni ya uzee lakini nayaona yale mazuri yakiliwe manani, yale yasiofaa, ni hivi ***(interruption)***

**Commissioner Salome:** Ningependa kumuita sasa bwana Ngei Katiku, Ngei Katiku, Ngei Katiku, E-m John Wachira, John Wachira, John Wachira, John Wachira; kama hayuko, wacha nimuite, Charles, ***(noises)*** James Ndung'u Mungai, James Ndung 'u Mungai, Ndung'u Mungai, Mary Ayuma, (***footsteps noises)*** Karibu, sema jina arafu upeane maoni.

**Martha Ayuma:** Hamjambo wote, jina langu ni Martha Ayuma, na niko na maoni kidogo kuhusu hiyo Constitution review. Maoni ya kwanza, ni sisi wa mama, ningependa tuwe na mbunge mmonja, wambunge wamama, ili wawe wakitulipresent huko mbungeni kwa sababu sisi tunaelemisha watoto wa kisichana, ama wamama, wamama siku hizi wameelimika sana, nahatuoni

haja yakuwa wanaume pekee yao ndio wako mbungeni na sisi wamama hatui huko kurepresent wengine, nikisema hivyo namaanisha ya kwamba, wamama tuko na violence against women, wamama huwa tunapigwa sana natungependa kama tuko na wambunge wamama huko wangekua wanatutetea upande huu. Upande wa raping pia, wamama tunarapiwa sana, na kama tungekuwa na mbunge mmama ama wambunge wamama wangekuwa wanatrepresent. Freedom ya speech pia tunahitaji kwa sababu wanaume wametuweka kama tunafinyiliwa sana kwa sababu hatuwezi ongea kitu chochote tunaambia sisi you have got no say. Tena freedom ya worship tunahiji, freedom ya education pia wamama pia tunahitaji, tunaelimisha watoto wasichana na wakiwa huko, ama wakiwa kati yetu hakuna kitu ambayo wanafanya ile yakumaanisha wamekuwa educated. Sasa tungependa tuwe at least tuwe tunajaliwa sana. Tena upande wa domestic work, pia tunahitajiwa tuwe tunaangaliwa sana hapo. Tuko na hii next of Keen, wazee siku hizi wamekuwa wakora sana, unaweza fikiria wewe diye mama peke yako katita hiyo nyumba, na kumbe kuna wamama wengine, mzee ameweka mama mahari pengine, na wee hujui , sasa saa ile mzee anakufa unashtukia unaambiwa kuna mama mwingine mahari fulani, wewe hutabuliki saa hizo na labda umezaa watoto karibu watatu, watano kwenda mbele ama watoto kumi. Tena, grabbing of the deceased's property, unapata kama saa ile mzee amekufa, especially sisi watu kutoka Western, huwa wananyang'anywa vitu ati kwa sababu ni mali ya mzee na wewe saa hizo hutabuliki. Sasa tungependa kama kungekuwa na wambunge wamama, wawe wanaturepresent upande huo kuhusu hili jambo tungefurahia sana. Arafu tena kuna hii early marriages, kwa watoto wasichana, tungependa kama hapo tungekuwa tuna wambunge wamama hapo wanatutetea kwa sababu unaweza pata mtoto wako ameolewa kama bando ni mchanga, arafu akienda huko – akienda kwa bwana, bwana anam-mistreat anamwambia asikutabui saa hizi juu ameshapata wengine – sasa hapo tungependa kama kungekuwa na law iwekwe. Kama mme ama kijana amechukua msichana wa mtu, akikaa na yeye karibu miaka tatu ama ata zaidi ya miaka tatu na wakosane hapo awe akichuwa hilo jukumu juu yeye diye amemharibia maisha yake. Arafu kuna hii nini, inheritance – kama mama bwana yake amekufa, mashemeji wanakuja na nguvu wanataka wachukua hizo vitu na lazima ama wamrudishe, kama hiyo pia inasababisha mambo mengi sana kama hii ukimwi, wamama tunapati na hizo njia. Sasa tungependelea kuwe na rules hapo – yaani kama mtu amekufa, ako huru kukuwa vile anataka lakini si analazimiwa na familia ya mme, kuchukua mali yake na kumnyang'anya. Sasa ningependelea katiba yetu tuwekwe sisi wamama, - kama mme wako amekufa (nafikilia juzi mlisikia kwa news vile bibi ya Chelangat alikiwa - kama kungekuwa na- nini (nafikilia mnaelewa hapo kidogo) hangenyang'anywa vitu ama ingekua je!), lakini nafurahia vile ilitendeka kwa sababu wanaume tuwe tunaandika will kama bando tungali wazima, wamama pia tuwe tunaandika will incase of anything, kuwe na will ya kututetea. Nafikiria ni hayo tu niko nayo. Asanteni.

***Noises (no introduction)***

**Josephene Kalunda:** My name is Josephene Kalunda, I'm representing deaf people in Kenya and my way of communication is very slow, so, I see may be I will talk more than 5 minutes because I'm having the memorandum yes but I'm using an interpreter so my time will be abit …

"We deaf people of Kenya we are very oppressed because the constitution of Kenya and according to some culture, some cultures make us to suffer for a very long time, now we want , the time you are making this constitution, you give us a freedom of expression – for example me I need a sign language interpreter in different areas – for example in hospitals, in the courts, in

schools and other areas. This will make us and help us to get more information and be able to express ourselves of what we hear. In TV, we want to see a sign language interpreter put there because sometimes people think if we see TV (people think all people understand - but we don't hear because we are deaf people).

We want also to have health care, free education, free medical, freedom of ownering property, for example if a person is having a farmily with a person who is disabled, this person must be given land even if he is disabled. We have seen in some areas, where may be a person is a disabled man – the 1st born, then the father gives the 2nd born the land but the 1st born because he has diability, the property is not given.

Employment: Many disabled people are not given work, for example the deaf people, the government have employed very few deap people. Also, in employment, deaf people are employed the last and they are the same people who are fired first. So this is why we deaf people have continued being very poor, law should protect our lives. When a deaf woman is married, and she is kicked off by the husband, the husband must take the responsibility and care for the children.

Schools: Schools – all teachers in government schools and schools for the deaf, they first, these teachers must know sign language. It is very funny to see a teacher who is going to a deaf school but he knows no sign language, nothing. So the school must look first, they must supervise first if this person is knowing sign language.

In the courts, if a deaf person is arrested, he must be given a sign language interpreter before the proceedings are starting. Sometimes deaf people are forced to write statements without a sign language and they are not knowing what is happening. In the police station, the sign language interpreters must be brought there. Hospitals and on other areas to help us must be having sign language interpreter.

Time for election, we know very well many people they have disabled and they use the thumb to put __________ so the constitution must look for other ways for using these thumb prints because of the disabled people. Also, in the courts, deaf people should be given freedom of bringing their own personal interpreter but they should not be chosen for. Sometimes we are given interpreters there who are not aware of sign language. This make us to suffer a lot. We want sign language to be recognized as a national language for the deaf people, also for the people because we know the people they use Kiswahili but it is impossible for us the deaf people to understand this. So in any area the constitution must put a sign language interpreter for that area and the same language should also be taught in schools (this should be taught in the school curriculum). The government also should provide sign language interpreter because like now the government doesn't know the use of sign language or the use of the interpreters. If a deaf person gets a problem, so he must pay for his interpreter – the deaf person must pay for his interpreter, now we want the government to give us interpreters. Also we want the government to give us disabled fund. These disabled funds are there but they are controlled by normal person, abled people who are not disabled, we want disabled people to be controller for these funds for the disabled. So this will make us able to share these funds well. In

Kenya, we have seen many times some cultures make disabled people to suffer a lot for example there are some places you will hear there is a problem if may be you have had sex with a disabled person, (the disabled people would be left alone – and now we see we have this problem of AIDS.) This have given the disabled people the problem of AIDS. Also some cultures they block the disabled people from marriage. We know very well, being a disabled, it doesn't mean that your body is not working well – this person who is disabled have a right also of having a family. So the law must be put there to protect all the disabled people and to be married if they want to be married and to have their family.

In parliament we want to be represented, by a disabled person equally, - the deaf, the blind, the physically disabled, all to be there and to be welcome in the parliament and this will make us to get good services. Many deaf people in Kenya will have their vehicles here, they know how to drive very well, but the constitution does not allow them to have driving licences. We want to be given freedom of driving like other people in other countries. Many deaf people in other countries have the freedom of driving but in Kenya here we deaf people are being oppressed. Thank you.

**Commissioner Salome:** Thank you very much Josphene, that is a very good presentation. I only have one question for you, you said that the disabled or the deaf especially are the last to be hired and the 1st to be fired. What proposal do you have to make on employment? Do you have a complete proposal that we can put in the constitution to ensure that the deaf get employed and sustained in employment?

**Josephine:** Yes I have, many deaf people have gone to school, and they have gone to universities, and they have the certificates, they know how to work, but time of employment, they cant because of the communication breakdown, and the boss says I don't have time with this deaf person. The government must provide sign language interpreter and also to keep their money aside and the ones to be given freely to the deaf people of Kenya. We deaf people are borne here in Kenya and we were not thrown here so we have all the right, so we need to live and to have good life like other people. We want to depend on ourselves but we don't want to depend on other people.

**Commissioner Salome:** Thank you very much Josphene, please register, I'm glad that you have given your views. Samuel orara oyuga, Samuel orara oyuga, Esther Nyambura, Esther Nyambura, Steve Oyambo Steve Oyambo, Anthony Njuguna, Anthony Njuguna, Stephen Macharia, Stephen Macharia. Edelea pale, kuna mwingine pale, sema jina na uedelee.

**Stephen Macharia:** Kwa jina mimi naitwa Stephen Macharia, hamjamboni wote kwa jumla. Mimi kwa maoni yangu, ni machache tu. Mimi ni kijana na bali ni na famili yangu mimi ni mzee. Kwa hivo watu kama sisi vijana kulingana na hii Kenya yetu, naongea na vijana sababu hao dio sasa wako wengi. Kwa hii Kenya yetu vijana wamenyanyazwa, kila siku, kama ukienda kila mahari kama baba yako si tajiri, au baba yako hana kitu yeyote, kijana ata kama kuna kazi hawezi andikwa, sababu ukienda, unaambiwa toa kitu kidogo. Ile kitu kidogo, sijui nyinyi wazee mlijifunzia wapi ama mlienda country gani mkasikia ati vijana lazima watoe kitu kidogo. Hiyo kito kidogo nawauliza wazee, mliitoa wapi? Kwa hivo kwenda kwa nyinyi wazee, chukueni mfano vizuri kwa vijana ili mtu yeyote ata kama babake aliyeaga au hayuko, kama ni kazi, mnaangalia vijana

wale hawana wazazi ili kama ni kazi kama ni serikali isiangalie ati mtu yeyote yule babake ama mtu yeyote anaweza mtetea ndio anaweza andikwa, apana. Tatu ningependa sisi vijana serikali yetu upande wa police, wanatunyanyasa sana sisi vijana, ukitembea hukui na amani, na ukiomba, unaulizwa unafanya kazi wapi? wapi kitabrisho? Ukiwaambia wewe hufanyi kazi, unaambiwa wewe ni jabazi, na basi kazi haujapata. Kama kungekuwa na kazi unaweza itiwa kazi serikali imekuoffer ati kuna kazi umekataa kufanya ili (interruption) kwa Upande mwingine, ningetaka kujua hii habari ya Elections, kuna vijana wanataka kusimama councilors, kunao wanataka kusimas MP na wengine. Mimi ningeomba kama ni wale wazee na sheria ziwekwe mda wa miaka kama kumu, mtu yeyote kama akipigania kama ni kiti ya Councillor, akimaliza mda wa miaka kumi kama amechaguliwa au hajachaguliwa, yeye anagive way kwa wengine. Kama ni MP vile vile na President vile vile. Kuchukua ati all miaka yako uliingia, ukakaa pale oh kiti ya councilor, unataka ati kama ni Dandora kiti ya councilor miaka yote ni yako, apana ikifika miaka kumi unawachia wengine pia nao vile wapeane maoni yao nawaonyeshe vile wanawezafanyia wengine kazi. Ikifika miaka kumi unaondoka – iwekwe katika sheria.

Ya tatu ni upande wa wanawake – wanawake Kenya hii wamenyanyashwa, kama mwanamke wowote katika kijiji, katika kijiji hakuna mwanamke yeyote yuko na ruhusa ya kusema kitu yeyote. Bali wale wanawake wanakaa kule buruburu, upande ya matajiri peke yake hao dio wanasema. Nao wakisema kitu yeyote wanataka ipitishwe sababu hao dio wako na pesa. Na sisi wanawake wale wako hapa katika kijiji, mtu ukifuata sheria zingine, ukimuuliza ile sheria ilipitishwa, haijui, ata hajui ni nini hii, juu haimsaidii. Kwa hivo mimi ningeomba, _________ katika serikali, tunawangaliwa kwa wanawake wote kama ni wauhusiano wote, wote kwa jumla. Kama vijana vitu yeyote inahusu vijana wote kwa jumla, na kama ni kila mtu wote kwa jumla, wanahusishwa lakini si ati ukiingia kama ni mbunge au wakiingia mahali wako wanapitisha kitu wengine ata hawajasomeshwa hio kitu ni nini. Kwa hivo ningeomba kwamba kabla wapitishe kitu yeyote, wanasomesha raiya arafu ndio wanapitisha kulingana na maoni ya raiya. Asanteni .

***Ngoja Macharia, ngoja kidogo***

**Commissioner Salome:** Asante sana bwana Macharia, hiyo ni maoni mazuri. Nina swali moja tu kwako, unasema ni lazima kila wakati, wananchi waje wafundishwe kwanza, lakini tukitaka kusema wananchi wote lazima wasomeshwe ile inataka kupitishwa na bunge, lazima tuje kwa wananchi tuwasomeshe kuwa wananchi wote ni lazima wasomeshwe ndio ipitishwe? Vile vile nataka kuuliza nikusema kuna mengine yanaweza kupitishwa kwa ajili itakuwa mazuri kwa kila mtu ata bila kuja kuuliza watu kama kwanza elimu.

**Macharia:** Wasema elimu, yaaa?

**Commissioner Salome:** Ya kila mtu

**Macharia:** Elimu kwa kila mtu, kama ni kitu inahuzika na inaweza pitishwa kwa raiya. Ee ili nimesema, raiya wanahusishwa, na kama ni vitu hasihusi raiya, yaani watu wote wanaweza tangaziwa tu kwa radio, magazeti na Television.

**Commissioner Salome:** Jiandikishe pale kwamba umetoa maoni yako. James Ndung'u Mungai, James Ndung'u Mungai, Eem Teresia Omolo, na Edward Omolo yuko? Utamfuata huo.

**Teresia Omolo:** Habari zenu? Mimi nikiwa hapa nataka kutetea haki ya wamama. Wamama wananyanyashwa sana sababu tuseme watu wa huko Kisumu, mtu bwanake akikufa analazimishwa apewe bwana mwingine, pengine huyu bwana ako ni wacarrier, na analazimishwa na nguvu lazima upewe bwana mwingine. Kwa hivo sisi tunataka iwekwe kwa law hio kitu isifanyikange. Mtu anatakikana achague.

Nikiongea tena point ya pili, wasichana wanatakikana wasomeshwe vile vijana wanasomeshwa, unapata mtu ako na wasichana watatu na vijana wawili, na hao vijana dio anawapeleka shule na wasichana hawaendi shule at sababu msichana ataolewa.

Point ya tatu, ningetetea wasichana pia, mtu unapata kwao wako na mali harafu hii mali yeye hasaidiwi nayo, anasaidia tu vijana, ati vijana dio wanabaki kwa boma. We msichana ukisazaliwa na ukuwe mkubwa wanaona tu uolewe, hakuna mahali utasaidiwa, pengine umelelewa pahali watu hawana pesa, wewe utasubuka tu huko maishani mwako na huku wako na mali na wakusaidii sababu wewe umeshaolewa. Tungependa watuwekee hiyo kwa katiba – hiyo mali wagawe ikuwe kitu ya mama pia. Ni hayo tu machache.

**Commissioner Salome:** Asante sana Teresia, Jiandikishe pale, kwa maoni yako.
Kwa vile uko na memorandum yako tafadhali tangaza tu within 5 minutes. Thank you.

**Edward Omolo:** Asanteni sana, mimi kwa majina naitwa Edward _Omolo. Mimi ni mkaaji wa Dandora hapa na sana sana mimi naishi katita kijiji abapo iko shinda mingi. Niko na memorandum ambayo nimetengeneza, na siwezi nikaisoma yote, lakina nitapresent kwa utume.

Jambo la kwanza ambalo ningesema, na hii nitawasomea sisi wote tujue kwa vile katiba yetu ya Kenya vile iko saa hizi, haina utangulizi yaani – tuliletewa bila sisi kutengeneza. Sasa niko na jambo ambapo inatuhusu sisi Wakenya itatuonyesha mwelekeo, na nitasoma:

In the name of the living God, we the people of Kenya acknowledging the experience of the bitter past, conscious of our perpetual civil negligence, are aware of our denied rights recognizing our passion and tolerance believed in just society for the welfare of humanity for the present and future generations. Conscious of our commitment to enhance love and unity now hereby resolve to abrupt this constitution through this national constitutional conference this day of 28th May 2002. Huo ndio utangulizi ambao ningeomba tuwe nayo katika constitution yetu na hii memorandum yangu si tasoma yote na nitapeyana kwa watume na iwekwe katika katiba yetu ya Kenya. Asanteni sana.

**Commissioner Salome:** Asante sana bwana Wamalwa, tumeshukuru tumesoma kila neno kwa hii memorandum yako, tumeshukuru, Thank you very much. Jiaandikishe pale tumeshukuru sana

Muli Muya, Mary Muiya, Mary Kairu, Micas Makoha yuko? Micas Makoha yuko? Endelea bwana Muli. Sema jina arafu endelea na maoni yako.

**Muli Muiya:** Kwa majina yangu naitwa Muli Muiya, nami ni mkaazi wa Dandora, upande wa kijiji Gitari Marigu. Hamjambo nyote? Asanteni, Maoni yangu ni machache sana sababu sisi kama wana watoto wale ambaye wanatoka kwa nyumba, wanaambiwa waende wakafanye mitihani kwa shule na hajasomeshwa ili aweze kuchukuliwa kachukuliwa darasa la kwanza, na hajafunzwa na mwalimu ndio anajua kuandika ABCD. Sasa kwa mfano mimi Kenya tukipata huru niko. Kikamba sielewi, nakama ni kikamba mimi ningeng'ang'ana nayo tu, nijue nikisitakiwa shelia Number fulani, inamaanisha fulani. Kwa hivo sasa sioni aja ya kuambiwa nitoe maoni sababu sijasomeshwa, nitajua nitatoa maoni ya aina gani? Kwanza nisomeshwe ndio sasa nikienda kufanya ile mtihani ya maoni, ndio niwe nikijua nitatoa maoni ya aina gani.

**Commissioner Salome:** Bwana Muli ningependa kusungumuza hapa kidogo, unajua tayari umetoa maoni, umesema hujafunzwa kwa miaka arubaine kama ungependavyo, ungependa kufunzwa?

**Muli:** Ningeomba, sio kupenda mimi – kwa Wakenya wote.

**Commissioner Salome:** Unasema, lakini leo tunakuja , tusikie Mkenya kila mmoja peke yake. Wewe mwenyewe ungesema nini?

**Muli:** Ningependa mimi nifunzwe ili nijue ndio ukiniita hapa nitoe maoni niwe naelewa natowa maoni gani. Jambo la pili, Kenya ni sisi tunajitawala, tunachagua macouncillors, wanatuhaidi wanatufanyia hili na lile, majube ndio hao na wakipiga kula wanajipatia msahara mnono. Wanatusahau sisi wenyewe, waanjili wao, na wakati tunafanya hii cencus ambayo tunaambiwa tunahesabu hesabu yetu, na wakenya kuna masikini kiasi fulani, hao macouncillor, hao maminister wanaenda kuomba msaada kwa ajili yetu na ila haitufikii sisi wenyewe bado ile kazi ambaye masikini jule mnyonge ambaye hana hakii haimpitii.

**Commissioner Salome:** bwana Muli ningetaka pia kukuomba kuwa, kuna namna mbili za kutoa maoni kwa katiba, kuna ile yenye mmefundishwa na mmesema hamjafundishwa, lakini kuna maoni yako wewe mwenyewe kutokana na maisha yako vile umeona tabu zile umeona, kwa hivo tungetaka utupe mapendekezo yenye unatwambia, mimi ningetaka kitu kifanywe, nami ningetaka kitu kingine kifanywe na katiba yetu ili inisimamie mimi. Tabu ni mwalimu ___ twajua tabu ni mwalimu na kila mtu anafanya kazi ya mwalimu taabu, na kila mtu anafanya kazi ya mwalimu taabu , kwa hivo ile mambo yenye matatizo uliyo nayo itatusaidia tuweze kuandika katika katiba mpya na wewe kutupa maoni yenye ungependa kuendekeza, mapendekezo yako wewe mwenyewe. Asante.

**Commissioner Salome**: Bwana Muli umeongea juu ya macouncillor na maujube wako na mshahara kubwa kubwa, bila wewe

kuulizwa – ungependekeza nini juu ya hili jambo?

**Muli:** Kwa upande huo, Councillor na Mjube ni muajili wa raiya. Raiya walimwajili. Kwa hivo badala yakwenda kujipatia mshahara angerundi kwa raiya, awaulize, huyu ndiye uajili wangu mliniajili, ningestahili msahara nilifanya kutoka hapa mpaka pale, mmeaona kazi yangu niliwafanyia vile mlinituma, inafaa mniongeze msahara, nao raiya wanarudi wanaona hii mfanyi kazi wetu ametutumikia vilivyo, inafaa tumuongeze mshahara kiasi gani kulingana na kazi ile aliotufanyia.

Jambo la pili, _____ hii tunasikia wanawake, ni kweli wanawake wananyanyashwa na wanaume wenzetu kwanza, sababu mke nyakati unapomuoa, ni mapenzi umepatana nayo ni mapenzi unapatana nayo bali sio punda umbayo umeoa ikifika pale nyumbani iwe, wewe unakaa Nairobi, unakutana na wengine wale wameoga umemsahau yule ambaye uliyemuoa nyumbani. Ata wakati uliompenda, alikuwa umefaa kwako, unamtupa kule, mara akija pale unamtupa anakuwa hana mme, na umemzuia mwingine ambaye angemuoa amlinde. Hio ningefaa kwa waume wenzangu, wachukuliwe hatua, na upande wa kina mama nao wakati unaolewa ni yule mme, umekubali kabisa, huyu nimemchagua, awa mme wangu, umtii naye akufanyie vilivyo. Kwa hivyo tuwache tuwache kutesa watoto wetu tumewaleta hapa duniani kwa sababu ya kutokuwelewana mke na mme. Kwa hivyo watoto wamekuwa na wazima na wana wazazi na wanasema kule ukimuuliza mimi sina mzazi amekufa. Kwa kuwa mzee ameenda amemtupa mama. Mtoto akiulizwa kule ata hajui baba yake ni nani, ata hajamuona shula yake. Kwa hivo hiyo ingefaa waume wenzangu na wamama wanatenda jambo kama hilo, wachukuliwe hatua ili tupate kujiendeleza sisi ni wachanga kwa uongozi nchi Kenya. Hatuwezi kufananishwa na America, Sweden au nchi zingine ambayo ziko na miaka zaidi ya mia moja na mia mbili kuendelea. Kwa hivo upande wa katiba, ni wale ambao wanakibisha katiba, ni kitu ambaye itawekwa miaka mingi sana baada ya miaka mitano. Natungeomba, wafumiliwe watengeze kitu kwa sababu ukiajili mfanyi kazi, na umkibishe kwa ile kazi ikiwa hajamaliza utamchokeza na ata atakufanyia kazi bovu ili amalize contract yake. Kwa hivyo ata kama ingeenda kwa miaka mitano, na katiba iwe tutaifuata baada ya miaka million mbili sisi wakenya, ingekuwa bora sana sababu ata hawa wajumbe wetu hatuwakibishi tunawangojea wamalize miaka mitano. Na wanakuja tena tunawachagua – na ile katiba ningeomba kwa maoni yangu itengezwe kwa lugha ya mkenya, yeyote ambaye anaweza kuyasoma kwa lugha yake apate kuelewa hii inamaanisha nini. Lakini sasa ikitengenezwa kisungu, na yule hajui kisungu elimu yake ni ya ngubaru, sasa ile sheria akienda pale kuona Ronia ama wokiri, kunaongewa hata afadhali kuletwa lugha ambayo nina ijua. Hiyo lugha siijui, itengezwe lugha ya kabira ya Kenya, ichapishwe vizuru kama vile Bibilia imechapishwa. Si ililetwa na mzungu – lakini tuwache kuambiwa habari ya sijui nini, sijui nini, lugha ambaye hatapata _____. Itengezwe lugha ya wakenya, yule anataka kununua kisungu ananunua, anaelewa hiyo, wa kiswahili anajua, wakijaluo anajua, mkamba ananunua yake, anajua hili (vanacular) akiongea lugha hiyo narudi kwa kikamba, mi najua vile ameniambia mimi – si kweli bwana Thimbo – tutengezewa lugha abaye tunaielewa. Sina mengine ni hayo.

**Commissioner Salome:** Asante sana bwana muli – enda pale ujiadikishe kwa maoni yako. Asante sana. Lukas Micas Makhoha tena, micas Makhoha. Redeemed Church. – sema majina arafu utoe maoni yako. Tafadhali mtoe mapendekezo, mkitoa shida, toa pendekezo kufuata hiyo shida. Sio shida peke yake bila mapendekezo, tungependa mapendekezo zaidi.

Asante sana bwana K

Gitau: Asante, ningeuliza tafadhali kama naweza tumia kingereza na kiswahili,

**Commissioner Linaola:** Tulisema tena asubuhi wale walichelewa, uko na haki kutumia lugha yeyote. Nimesema kiswahili, kingeleza, kikikuyu, kisaburu, kitrukana, hatutakosa mtu wa ktranslate. Mtu ako na haki kutumia lugha yeyote.

**Gitau:** Asante sana. Yangu kabisa, ni kuhusu elimu – Ni mapendekezo. Elimu inifai sana huru kwa wote, (free for all) that is elimu ya msingi (watoto wa primary school) ifanywe mandatory na walazimishwe kwenda shule. Arafu, ukieweza kufanya mtihani vizuri kwa darasa la nane, uweze kwendelea mbele then hapo may be wazazi wanashrikiana na sherikali kulipa karo.

Ya pili na ya mhimu ni afya – Afya inafaa ifanywe bure kwa wote, ni haki ya kila Mkenya awe mtoto, mzeee, naama atibiwe na nikiongea haswa kuhusu sisi, wananchi wale tunaishi estate ya Ndadora, mapato yetu ni ya chini sana, abapo sasa mtu akiwa mgojwa, akienda pale hospitali kutibiwa, pesa anaitishwa inakuwa ni mingi kabisa mpaka inambidi kama ni dawa aapate dose kidogo hiyo ingine imani yake na Mungu wake imponye. So mi nafikiria afya ingefanywa bure kwa wote.

Jambo la tatu na la mhimu, ni ukosefu wa kazi (unemployment) hii issue ya unemployment inatokana na hivi, - wengi wetu hapa vijana, mimi wenzangu hapa tuna elimu, tumesoma, lakini hatupewi nafasi na serikali kwenda kutengeneza ujuzi wetu, kwa sababu jambo linaoitwa nicotism – unapata mtu kazi, kazi unapewa on vile unajuana, may be baba yangu ni director, mjomba wangu may be ako na cheo, unapata sasa kwa sababu mimi nina mtu ananijua, nitapata kazi. Mwenye hana mtu anamjua, then haajiliwi

Jambo lingine, ni ukabila kwa kazi, si siri kila mtu anaona, ukienda kwa corporation mingi unapata may be kabila moja ndio inadominate. So, ningependa hiyo tafadhali pia, itengenezwe, kazi mtu apewe on merit, kulingana na ujuzi, experience, elimu bila kubaguliwa – whether ukuwe wewe ni disabled ama una afya to kamili.

Jambo la nne ni land issue – Unapata mtu ako na udongo zaidi ya acre 200,000 ama acre 20,000, na yeye mwenyewe anatumia acre 3. Ili hadi kuna watu abao hawana ata that kasmall piece of land – ili abaye anafaa awe pale aweze kulima apate mapato kidogo ili afanye kuendeleza maisha yake day in day out. So ningependa kama una udongo zaidi ya ile unatumia, if you have may be 10 acres of land, you are using 2, then the rest 8 you either surrender ama ulipe tax, ili watu wengine wapate kutumia nini? Udongo huu!

Jambo la tano, ni kuhusu askari wetu – I believe so, tunawashukuru sana kwa kazi ile wanafanya lakini wamekiuka kabisa. What is meaning of Kenyan ukiniangalia? I believe I have the right as a Kenyan to leave work and ama own property at any place Kenya hii. Ni haki yangu kuwa na mali ama biashara, mahari popote kwenda, ama kufanyia kazi Kenya hii bila kusubuliwa. Abapo sasa nikiwa hapa Dandora, naweza kutana na police na asiniulize chochote, lakini nitaenda sehemu zingine,

nizuiwe kwenda ama niulizwe nafanya nini. Na ili hali akiniangalia anaona mimi ni Mkenya, na sina restriction ama ____ la kukanyanga anywhere. So, ningependa, kwa police I think mnda kidogo, ili waweze kutrainiwa properly. Na sana sana kuhusu public relation, vile unaweza kuongea na mtu, pengine asiwejiweza, pengine mtu masikini na pengine mtu tajiri pia.

Jambo lingine ni kuhusu katiba – hili ni pendekezo, - Naamini ya kwamba, wengi wetu hatujapata nafasi ya kuisoma hii katiba, ningependa ifanywe – ukifika daraja la pili ama secondary education, I believe so serikali inafaa ifanye mandatory ama free mafunzo, wafunze hawa wale wako mashule, na wale hatutaweza kupata nafasi hiyo ya kusoma shuleni, wakati una-apply kupata kipande chako, (your national ID card) ukiwa na 18 years, upewe copy, ama upewa katiba abayo imeandikwa kwa ile lugha ile unaielewa, hiyo ni yako kama vile kipande chako.

Jambo lingine na la mhimu ni Election – Naamini ya , election inafaa iwe free and fare – so ningependa hizo ballot boxes zikua open na transpalent dio kila mtu aweze kuona. Na urgue hio uwe umetekelezwa. Asante.

**Commissioner Lenaola:** Asante Bwana Gitau, hatuna maswali, you were very clear, thank you very much. Please register at the programme there. David Kuria, David Kuria. Karibu.
Tafadhali kuna watu wale wamekuja bila kujiadikisha, kama hujaadikisha please enda pale kwa meza kwa maana siwezi kujua utapenda kusungumza ndio nijue ungependa kusungumza. Asante: Na hapa kama hupendi kusungumza, ningependa kuwa na list ya wale watu wamekuja mkutano, kwa hivo kila mtu lazima ajiregister pale. Ata kama hapendi kusungumza. Endelea bwana Gitau, (kuria) Bwana Kuria.

**David Kuria:** Majina yangu ni David Kuria, mimi mkaaji wa hii kijiji. Sasa kitu ningependa kutoa, nikulingana na vile sisi wana kijiji tumekuwa tukifinyiliwa sana na sheria ama na sherikali, ambayo serikali yenyewe, inajua sheria lakini imejifanya ni kama haijui sheria. Nafikilia sijui ni sehemu gani ya sheria ambayo inayosema, kama yule mtu anaweza kaa mahari zaidi ya miaka kumi, huyu mtu hufai kumtoa hapo bila kumonyesha mahari pengine. Lakini sisi wanakijiji, tumeona haki zetu tukifinywa sana (kama juzi mmeona mjini Mombasa, watu wamekaa mahari zaidi ya miaka ishirini, arafu unashtukia siku moja tu tinga tinga inakuja inafujafuja mali yao – na ambayo sherikali ambayo ilitengeneza hii sheria na inafaa kulinda sheria, haiangalii. Sasa si ata tunashidwa, ata tukiwa na sheria aina gana, ile shinda ziko ni serikali haitii itakuwa vipi.

Kwa upande mwingine, ni upande wa watu wa Nairobi, tumekuwa tukifinywa sana, kama ni upande wa uajili. Nafikilia kuanzia 1982, wakati kulikwa na mapinduzi , hapa mjini Nairobi, hatujawai kusikia vijana wetu wakiajiliwa kazi ya jeshi, ama police, ilikuwa tu seheru zingine za Kenya unasikia Nanyuki wanachukuliwa jeshi, Kisumu wanachukuliwa jeshi, Hapa Nairobi sijui ni sheria gani iliundwa ikawa tunabaguliwa – arafu, kuna ingine sheria tunaona sisi wana Nairobi – ama watu hawana guvu sasa, tunaona kama kuna sheria zingine police wanatumia kwa kunyanyasa mtu ambaye hana guvu, kama nyumbani pengine unaweza kutana na askari – ata ile njia ya kukushika njia ya adabu hatumii. Unashtukia amekuja anakushika, unakaa wapi, kipande yako, unafanya kazi wapi? Arafu akisikia ni kama mtu tajiri, unaona ni kama anasikia anaenda kumshika na njia ya

adabu, anamwambia, habari yako mheshmiwa, wewe ni nani? Natakikana kwa kituo.  So ona hapo, sisi naona sisi ambao hatuna guvu, tunaendelea kufinywa.  Arafu kuna sheria zingine ambazo ziliundwa wakati serikali ilikuwa inatoka kwa wakoroni, ikiwa kwa mwananchi wa kawaida, nayo ilikuwako ni mambo ya kupigana na kutojua kusoma, umasikini na afya.  Wakubuka, kuna wakati, hakukuwa na hii mambo ya cost sharing.  Kama wewe ni mgojwa, ata kama ni ugojwa wa ina gani, ata kama ni Kenyatta utakaa miezi gapi, unashrikiana  na serikali; Saa sijui tena, ilikuwa ni vipi, ama ni ugojwa gani walikaa ikapiduliwa ikasemekana, lazima ukuwe na cost sharing, na that is tulikuwa tumepata uhuru kutoka kwa mkoroni, hiyo ndio mambo ilikuweko hapo mbele.  Na sisi wana kijiji at tumekuwa tukisubuka sana, ata mtu anaweza hapa na akuve, ata tunakosa pesa ya kwenda kumsika kwa sababu tukimpeleka Kenyatta itakuwa ni vingumu kumto? Kumtoa. Sasa ningeomba, zile sheria zilikuweko ambazo zilikuwako ni nzuri, serikali iweze kuzipindua ziwe zikifuatwa kwa sababu ata tukitoa sheria za aina gani na hazifuatwi, itakuwa ni kazi ya bule.

Na kwa upande ya hongo -  Ningeomba kama ni kiongozi ambaye amezaliwa mahari fulani, kwa madaraka magani, uwe ni councilor, uwe ni chairman wa kijiji, uwe ni chairman wa shule, upande wa hongo tuache kabisa.  Kwa sababu sisi ndio tunaweza leta ata ___ hii ya kawaida, kutoa rushwa kwa sababu hatujapewe ata kama kamsaada, ukimwambia ee tafadhali weleta shilingi mia mbili nikusaidie, unaonekana kama wewe ni vitu unafunza, lakini akija kwako, ata kama kuna shida, "kama uko na uwezo nisaidie" kama huna uwezo mwambie haiwezekani.  Na nihayo tu.

**Commissioner Lenaola:**  Asante sana bwana Kuria kwa maoni yako, umesikika vizuri, jiandikishe pale tumeshukuru.  Ninali.  Karibu, sema jina yako yote kamili arafu uendelee na maoni yako.  ***(unclear noises)*** Tutampa nafasi mtoto baadaye atoe maoni yake lakini sasa nafasi si yake.

**Elenina Mwimanyi:**  Asanteni sana, kwa wale watu wamekuja hapa – majina langu yote, mimi naitwa Elenina Mwimanyi na mimi ni mkaaji wa Dandora.  Sasa niko na maoni yangu tu kwa yale mambo naona hayaendi vizuri .  Hii ni serikali yetu tulitoa kwa mbebelu na itasemekana sisi tumejitawala katika uhuru, na hatuoni uhuru abapo iko.  Uhuru ili ambapo sisi tuko nayo, ni kunyanyashwa na wale watu viongozi wetu.  Maana ni hii, wale watu wanahudumiwa, ni matajiri kwa matajiri, lakini wale masikini wamekuwa kama ni kitu ile ambapo haionekani serikali.  Na ninaomba hivi maoni yangi ndio hii,  Hii katiba yenye tunatengeneza tukiwa tunaonana na nyinyi wote, wale ambapo wako hapa ni wa serikali na watu wakutengeneza katiba, katiba afuatiliwe sana.  Sisi ni wazazi, na tumezaa, na hakuna mzazi anaweza kupenda mtoto wake akuwe mbaya, ama mtoto wake anyanyashwe na serikali.  Kitu kiko hivi, mtoto kama amekosea, serikali na mzazi yafaa msaidianane, sio ati unyanyashwe at sababu yeye ni masikini, na imekua mazoea, sasa wakaaji wa Dandora tuko na shinda, sana, ata kama mnaona uchafu iko hapa, kweli tuko na vijana, lakini wale watu wengu sana mkifanya uchunguzi, watu wanatoka sehemu ingine wanakuja kuleta uchafu hapa, na ni katiba ile ambapo anatakikana kufanywa.  Kuna watoto wamesoma, hawana kazi, na hiyo ni jikumu ya serikali, kujua wale watoto ambapo wamesoma, na hawana hazi, wanaweza kusaidiwa kivipi?  Meradi ziko, na serikali ndio imeshkilia hio meradi, wachungulie vijana wetu wale ambapo hawana mapato ili vijana wawe wameshkiliwa hiyo meradi, ndio wakose kuonekana kwa barabara, na serikali ina nguvu ya kufanya hivo.

Kitu ingine ni hii, sisi akina mama tunanyanyashwa sana, hatuonekani, na tunataka katika katiba wamama wakuwe msitali wa mbele, sababu (ata mkihesabu hapa) wamama ndio wanatengeneza serikali, ata kwa kula wamama ndio wanakuwa katika mstali wa kwanza, na vijana, na wale watu wanaonekana hatutaXXXX hawaendi kuchagua viogozi. Kwa hivo wamama, wawekwe mstali wa mbele kwanza na vijana, na kuwe na mpangilio katika serikali, mtu akichaguliwa, wasingoje amalize ile miaka inamfaa. Kama hafanyii wananchi kazi aondolewe, kuna wakubwa wale ambapo hawana hesima ata na serikali, na wameaanza kufundisha watotot wetu siasa ile mbaya. Mtu kama huyo, yafaa itengenezwe sheria ya kumsika sababu sisi laiya, tukiwa mbali na serikali, hii nchi yetu itakuwa ya dhika kila wakati, na kuna watoto wasoma vizuri zaidi, ata mtihani yao wanapita, lakini, hiyo imekua mazoea wabunge wanaweza chukuwa hiyo majina ya wale watoto wamefanya vizuri wakienda kudanganya serikali ati hao watoto wanaenda kusomeswa bure. Lakini huyu mbunge, atachukua watoto wa matajiri kwa sababu ya kukula hiyo pesa ya matajiri na wale masikini watawachwa hivo hivo. Kwa hivo yafaa, kuwe na utumishi ule ambapo utalinda hao watoto masikini. Na wamama, katika kazi zote wamama wahusishwe. Kuna kazi zile ziko kwa office, na wamama wamesoma hawahusishwi, ata kwa gorovia, ata kwa mahospitali, kama sisi watu wa community health workers, yafaa pia katika katiba serikali ituangaliwe sana. Tunafanya kazi gumu, sisi ndio tunajua wale wagojwa wamegojekea katika vijiji, nahatujulikani mahari popote. Kwa hivo katika katiba, serikali yafaa iangalie masrahi ya wale watu wanasaidia daktari kufanya kazi katika vijiji. Na hiyo dio maoni yangu, na asanteni kwa wale walio nisikisa.

**Commissioner Lenaola:** Asante sana mama, jiadikishe pale kwa maoni yako tumeshukuru.
Pius Ouma yuko, Pius Ouma, Ouma Pius – Endelea bwana Mugambe.

**Mugambe** Habari zenu nyote? Kwa maoni yangu, mimi naitwa Were Mugambe, na nina pedekezo, na pendekezo yangu ni kwanza tuwe na decentralized administrative systems, mji kama Nairobi hauwezi kutoka town, sababu mahitaji ya Dandora ni tofauti ni ile ya Kariobangi, na ni tofauti na yale ya Westlands, kwa hivo watu wa Dandora , mashughuli ambayo nalipwa isipelekwe town, imbakie hapa hapa, kwa hivo councilor kama ni councilor ni wa Dandora ashughulikiwe. Mashughuli– naikusanywe hapo sababu mara mingi tunalipa na xxxx na pengine diposa zinaende kusafisha Westlands, na uchafu za Westlands zinakuja kutupwa huku. Kwa hivyo ningependekeza tuwe na decent lifes.

Administrative systems - mambo kama elimu, ni wengi sana vijana ambayo wako hapo wako katika huu mkutano wamesoma mpaka form 4, mara mingi najiuliza, mtu anasoma mpaka form 4 ile apate certificate ya kuwa gabbage collector? Kwa hivyo we should ______ (inaudible) our constitution, that basic education iwe atleast mpaka form 2 na lazima watu wazome mpaka form 2. Kama ni mzazi na mtoto wataona kama mtoto ana nia ama anapendelea kuendelea na masomo. Baadaye itamtoa huyu mtoto anaenda kuelimishwa masomo ambayo itamtayarisha kikazi. Isiwe tu kule kwenda shuleni, ni njia ya kuwanyanyasha wazazi walipe school fees, ili mtoto aje awe manamba au gabbage collector. labda anaweza kuwa akijifundisha kazi kama electrician, kutengeneza radio, TV ama vitu zingine kama anataka uwe gabbage collector aanze mapema ukiwa form 2. Na ile ambayo kwingine kutoka kwa wazazi, ata watoto wenyewe wataona kua kweli wanapendelea sana masomo upatiwe nafasi

aendelee, na sisi tunapeleka tu watoto shule ili tupatie wahidi biashara ya kuuza vitabu na watu wengine wafaidike na hiyo elimu haiwafai.

Na police station: Na ningependekeza kuwa kulingana na mahitaji ya watu, wawe na police station, na nikisema police station namaanisha iwe watu XXXX wafanyikazi wa serikali police wenyewe, kwa sababu mara mingi sisi tunalalamika kuhusu mapolice, na kusema ukweli, nikusema kuwa jinsi wanavyoendesha kazi zao, si vizuri lakini ata nao jinsi wanavyo tunzwa si vizuri, wakienda kama Kinyago wanafanya kazi kwenye office zingine tunakaa ni kama sijui nini. Kwa hivyo hao wafanyikazi, na mfanyikazi kama wengine wote wa Kenya watengezewe vicheo vya kazi vizuri, kwa sababu ata sisi laiya ndio tunafungwa katika hivi vituo. Wapewe nyumba nzuri ili tuwe na police wachache, wanalipwa vizuri, wanaishi vizuri, watuhudumie vizuri. Na xxx mpaka huduma nzuri ikiwa watu wenyewe wanahudumiwa vibaya na serikali na wakenya wote wanalipwa kwa hivo kulingana hitaji ya watu, kuwe na police station xxxxxx ama courts. Tangu nikiwa mdogo mimi huwa najua in Eastlands, mtu anapelekwa Makandara. Ata mbunge wetu mara mingi huko ni kama kwake nyumbani. Nimefikiria vizuri, kila constituency, kila constituency, iwe na court yao na hapo ikiwa constituency iko na wetu wengi sana kama Embakasi, iwe na zaidi ya moja. Kila mtaa kama Dandora, sasa unafaa uwe na police station zaidi ya mbili. Kwa hivyo tumepasuliwa tutakuwa na macouncillor wa wili. Kwa hivyo xxxx na sio police post, police station.waendelee vile vile na hizo police station ziwe na nyumba za hao wafanyi kazi wa serikali ambao wako huko dani. Na hapo kwenye police station kuwe na wakili ameandikwa na serikali ambapo kila mtu akije ama kabla ya kuingia kwenye cell, anapewa nafasi ya kuonana na wakili. Kila statement atapeana, anapeana wakili akiwa anasikia na still anaona. Nao police wakitembea watembee na orodha na vile ukishikwa, ukisimamishwa ndio utakiwa ukisign makato uliposhikwa, ukishikwa ulikuwa unafanya nini. Ningependekeza macouncillors, wasiwe watu wa vyama, wawe independent candidates sababu macouncillors wanachaguliwa kuhudumiwa magojwa, hakuna ugojwa wa DP au wa KANU au wa NDP. Maji, sewage ikifunga, ni shughuli ya councilor, basi hakuna sewage ya KANU, hakuna sewage ya DP. Wawe independent candidates, mtu akitaka kuwa parliamentarian sasa anaweza tuingia kwenye chama. Lakini civil candidates ni administrators, na sio watu wa chama fulani, wa chama kile kingine, wewe ni mtu tu, watu watachaguliwa kulingana jina lako na uwezo wake, zaidi ya hapo, mambo ya chama, unaona kama huu mtaa wa Dandora umenyanyashwa sana hivi miaka kumi tangu tuaanze multi party election sababu Dandora ilikuwa inaonekana kama area ya opposition. Pengine macouncillor wetu wangekuwa si wa chama hiki ama kile, hatungeumia saana hivo.

Hawa macivic administration, wawe na independent institutions to hold the civil candidate to administer their works. Nikisema hivi namaanisha, (kwa mfano, Dandora, kumekuwa na Councillor mmoja, wakazi wengi wa Dandora hawamjui councilor, hawajawai muona, miaka 5 zimeisha.) hii, wakazi wa Dandora hawajui wanalipa kiasi gani ya mshahara, kwa hivo hawajui kama wana pesa za kutosa ya kutengeneza barabara, ya kutongeneza street lights, kutengeneza hospitali; kwa hivyo mimi ningependekeza, hao macouncillors, wakisa chaguliwa, wawe kama ni Dandora, wawe na caretaking officers na hao officers wawe wanalipwa, hiyo ni kazi, wanasaidia macouncillors kufanya kazi ya hiyo mtaa. Na hao watu macouncillors wawe kila mwaka, kila mwisho wa mwaka, kama kampuni kubwa mingi tunazojua hapa kila mwaka wana Annual General Meeting (that is igekuwa councilor afanya mambaya kwa miaka 5 arafu ndio watu wamtoe shukula sana) huko dani vitu zingine za miaka tana

inatuchukua miaka 100 dio tuweze kurepair. Pengine ata hatutaweza. Kwa hivyo kila mwisho wa mwaka na maofficers zao, makanisa, na NGO wa hio city kuwa wanakutana wame-evaluate kazi iliofanywa muaka huo. Wakiona kweli huyu councilor na watu wake hawafai, wanafutwa kazi mara moja. Sio wagoje miaka tano, tunanyanyaswa miaka 5, ndio uchaguzi uje, mtu amejitajilisha yeye na bibi yake na jamaa zake, sisi tunabaki hapa tukiangamia; kwa hivyo mimi ningependekeza councilors wasio wameendesha mambo ya huku ni kama biashara yake personal yeye peke yake na rafiki zake kadha, kama wanangoja achaguliwe ata ingine au amekuja na team yake anayependekeza. Kwenye hii team kuwe na wamama, kuwe na vijana, kuwe na wazee. Kwa hivyo saa zile wana campaign wanaambia watu mimi nataka kuwa councilor, na huyu diye atakuwa xxxx wangu, huyu diye atakuwa treasurer, watu wenyewe wataona, kulingana na team anayotaka kufanya nayo kazi, kama anaweza kaa mtaa wao ama ward yao au vipi. Lakini mara nyingi mtu anajitokesha peke yake na hatujui kama anapatiwa pesa, ata ukienda kwenye mikutano kule charter hall ama kwingine, anapewa pesa za ward, watu hawajui, yule anazitumia, hatujui. Kwa hivyo kuwe na Estate officers kusaidia macouncillors kufanya kazi zao.

Ningependekeza kuwe na Community Police System – community police system dio itatusaidia pengine ata kusaidia wengi wa hawa vijana kazi. Sababu saa zingine unapata police ni mTarkana, anapelekwa kisumu, wanamtoa pengine kama Kodole, lugha haelewi, shida za kodole, huyo anaenda kama kuhudumia serikali na hahudumi mtaa wa Kodole, kwa hivyo community police system atamaanisha kuwa wale ambao wafanya kazi ya police pale ni watu wa hio mtaa wanaielewa, wanaelewa shida za hapo. Na wao wataweza kusaidia, pengine ata mchana ata hakuna aja sana ya police kutembea. Na police community system pia wao watu wanapewa huwezi pengine ata kuhudumiwa ambayo hamsimami. Mtaa kama Dandora, askari wengi mara mingi tunaimbiwa na hawa ndio wa kwanza kwenda kijificha chini ya vioski ili mtu anakuja na buduki na wewe unatumia mkuki. Kwa hivyo wao wanaweza kuwa licenced kutumia ata siraha usiku (licenced.). Pia ningesema allocation of resources – mtaa kama wetu ni mkubwa sana na watu wengi wanakufa ata njiani wakipelekwa Kenyatta, na pengina magojwa yangeweza kutibika. Kwa hivyo, hospitali kama hizi zetu ziwekwe credit, iwe ni Dandora, machakos Kenya, kulingana na population government should allocate resources enough in schools, hospitals, xxxx na mortuary services and the like. Nikimaliza namalizia ni kisema tujaribuni tutafute njia nyingine ya kueliminate harambee kwa sababu harambee are just propagating corruption. Kuna wengine ni viongozi na sababu ni masikini, hawawezi kuadhilia harambee na wapewe pesa, tunakataa, na wengine wana uoga wakuadhilia harambee pengine kwa sababu wamegrab, wameimba pahari, wanaweza kuedelea na harambee zote wakapewa pesa, tunathania kwamba kuwa hao ndio viongozi. Mambo ya harambee tujaribu tuone kama inaweza tolewa. Hiyo ndio kwanza inachaguliwa kulingana na uwezo wao kibinadam. Sio XXX wao kifedha. Asanteni.

**Commissioner Lenaola:** Asante sana bwana Mugambe,

**Commissioner Salome:** Asante sana bwana mugambe, yamekuwa maoni mazuri, tunashukuru, nina maswali mawili kwako, moja unasema kuwa madiwani wasiwe wanachama kwani wanatetea mambo ya afya na ata haina wanachama, kuna mambo ya masomo na kadhalika, Na wasema kuwa wana bunge ndiye wenye vyama. Nao wabunge hawa vile tunavyo elewa ni kuwa wanatumikia mambo kama ya masomo , yenye pia haina wanachama, na mambo kama hiyo. Kwa nini wawe wanachama na wengine wasiwe wanachama? Hiyo ni swali la ufanusi tu, ukiwa unaweza kueleza. La pili ni kuwa umesema bwana diwani akija ama XXX kuja kufanya campaign , aje na kikudi chake chenye atafanya nacho kazi. Na umesema hiki kikundi kiwe na

wanawake, na kiwe na vijana. Utatupa utaratibu zaidi kama unataka wanaweke wawe kiasi gani kwenye huu utaratibu, ungetaka vijana wawe kiasi gani? Kama twaweza kuendelea na hii ikikubalika kuwe kuna mama mmoja na kuna kijana mmoja, na kuna wazee thalathini. Kama unafikilia hii utatusaidia, ama unafikiria kunaweza kugawanywa je dio kila mtu akatia yeye mwenyewe amesha husishwa. Asante

Mugambe: Ningependekeza iwe asili ile italingana na idadi ya watu pale. Ikiwa wanawake ni wengi, wawe waakilishwe ma watu wengi zaidi, ikiwa vijana ndio wengi, bora watu hapo wawe wamewakilishwa sasa. Ni gumu kusema ni gani (50 50) , pengine utaenda kwenye ward zingine unapata asili mia themanne ni wanawake. Kwenye hii kikundi kuwe na wanawake, kama ni watu kumi, wanawake 8, lakini mhimu sana , ninaweza pendekeza kuwe na zaidi ya wanawake zaidi ya wanaume. Na mara mingi, wanawake wanatumiwa – kuna shughuli zote za kila siku na wanatumiwa tu, mambo inapadwa hao wanaitwa, jooni mpanguze meza. Kwa hivyo wanawake wapatiwe nafasi ya kwanza, na zaidi ningependekeza pengine ata hii ingine constitution kwamba wawe nominated, civic and parliamentary candidates wawe wanawake tupu sababu wanawake mara mingi hawana zile pesa na nafasi kama wanaume za kwenda kufanya campaign. Kwa hivyo nominated candidates, kwenye shughuli zote, zozote, wawe ni wanawake wanapewa hizo nafasi. Mara mingi bunge ni mahari watu wanaenda kutoa mapendekezo, kushauriana, ata kama inaweza its like school of debt, chama, hapo watu wanaenda kuwaza, sasa mimi sasa naweza sema sawa, mimi nawaza kiDP, mi nawaza KiKANU, mi nawaza KiSDP, mi nawaza KiFORD People lakini kwenye administration, maji ikikosa Dandora ama sewage ikosekane hakuna UDP, hakuna UKANU, ata ningependekeza kuwa civic candidates wasiwe watu wa chama. Ikiwa mtu anataka kwenda kutoa mawazo yake, baada pengine akitaka aende awe mbunge ili atuelezee kiuzima yeye anafikilio taratibu ni huu na yale mawazo yake yatatumika na macouncillor, aonyoshe utaratibu wa mambo. Mwisho ningesema kuwa military wawe kwa community and social services, kwa sababu nchi kama Kenya tunatumia pesa nyingi, kulipa watu wa majeshi mishahara, na wanapokea tu huko kwenye mabarracks, barabara zinapomoka huko na hatuezi kaona, kwa hivyo hawa watu waongeze ata umilitary wao wengi, vijana wengi wapate kaji lakini waje wapate misitu, watengeneze mabridge, watengeneze mabarabara, watengeneze hospitali, hiyo misharara ambayo wanalipwa Kenya tangu ipate uhuru ni karibu miaka 40, hatujaenda vita na mtu. Naonekana alipwa kwa hii miaka 40 na kazi ya maana ambayo alifanya sijaona, kwa hivo the military should be in all the social community services. Asanteni

**Commissioner Lenaola:** Asante bwana Were kwa maoni yako. Jiandikishe pale umetoa maoni yako ni kutume. Zarah Hamed, Zara, Mhesimiwa karibu, Zara endelea sema jina na utoe maoni yako.

**Zara Hamed:** Jina langu ni Zara Hamed , mimi tatizo linalo nisubua, ni kubaguliwa kama mimi ni muislam, kwa sababu mimi ni mzaliwa wa hapa. Na mimi wakati ikija tatizo kipande, mimi nikipenda kuchukua kipande, ama mtoto wangu, naambiwa nitoe cheti ya kuzaliwa ya baba yangu, mara naambiwa nilete ya mama yangu, mara naambiwa nilete ya babu yangu, na labda sina hawa watu wote. Serikali yenyewe- sisi kama waislam tuko hapa katika nchi Kenya lakini bando hatutabuliwi kama raiya wale wa kawaida. Kama hapa Dandora kuchukua kipande, mimi wanaona mimi labda ni mzaliwa wa Kibera. Sina haki kama mkaaji wa Dandora hapa niweze kwenda Kayole nipate kipande, nitaambiwa wewe, enda katika ile mtaa umezaliwa. Na hali

labda wale watoto ambao nimekaa na hao hapa wanatablikana vizuri sana. Kwa hivyo katika pendekezo langu kwenye hili tume ningesema, yule mtu yeyote ambaye amezaliwa hapa Kenya, na hali mna cheti ambayo inadhibitisha mimi ni mzaliwa, niwe niulizwe nilete ya baba yangu, ya babu yangu, ya nyanya yangu, na labda kwa mfano mimi sina hao watu wote ambao tunaishi na wao.

Na tatizo lingine pia ningesema – tatizo la wakaazi - kwa mfano unaona mtaaa wa kibera, kibera ni mtaa ambao umekaa kabila ile ya wanubi kwa mnda wa miaka 200. Serikali iwe ikipata uhuru tuliikuta hiyo kabira ikiwa hapo, na wakenya wakati wa hivi sasa serikali haichukua kama hao bando ni wananchi wa Kenya ata ijapo inawapatia mambo mengine, bando inawaita ni squatters. Hatuna haki na ata tuseme hao ni wageni, hakuna mahari pengine huyo mtu anaweza kwenda, maana yeye anajua mimi ni mzaliwa wa hapo, na wazee wangu na wababu zangu tuliwakuta wakiwa hapo. Na wala hiyo kabila halina yani ati reverse nyingine at serikali haitanitabua itanipeleka kwingine na ata kama nitapelekwa kwa nchi ingine, hakuna nchi inaweza kukubali watu ambao zaidi ya miaka 200 hawawajui wala hawajui asili yao wametokezea wapi. Nafikiri kwa haya machache nasema asante.

**Commissioner Lenaola:** Asha Ali Hussein, Ee Zara, jiandikishe pale Asha, arafu nitamita George Otieno, utamfuata huyu Asha.

**Asha Ali Hussein:** Nashukuru sana kwa commissioners wote, tunawakalibisha kwa mtaa huyu wa Dandora, Kinyago primary school, na waadikishaji wote wa kurecord, na mbunge wetu pamoja na wengine. Jina langu ni Asha Ali Hussein – na mimi ni mzaliwa wa Kenya kwa hivyo mimi ni mwanakenya. Ningelipenda, tuwe na malekebisho ya katiba, nisipitishe jambo hili kwa sababu ni ya wakenya, yaani, mwananchi wa Kenya anastahili kuwa mwananchi wa aina gani? Mimi naonelea mwananchi wa Kenya ni mtu ambaye amezaliwa katika nchi ya Kenya na mzazi ambaye ni mwanaKenya amezaliwa katika nchi hii ya Kenya, ata kama babu na mababu walitoka nchi zingine, na yule mama ama baba wamezaliwa Kenya, mimi ninastahili kuitwa mkenya. Na pia ukiadopt mtoto kutoka inje, na iwe wewe unamlea, ukweli ni ya , love enough ya ile mtoto inatoka kwetu. Kwa hivyo yule pia awe ni mwanakenya. Hilo ni jambo la kwanza.

Jambo la pili ningelipenda kusititiza unyanyasaji kwa wanawake, wanawake nafikiri most of the time waone wamekuwa wakishughulia kwamba wanawake ni viumbe viumbe thaifu. Lakini hatuko thaifu hifo, nafikili mambo yote mengi, inabebangwa na akina mama, na nchi ingalikuwa haina akina mama, sithani nchi ingesimama, kwa hivyo, kwa hivyo, katika malekebisho ya katiba ningeomba usawa kwa akina mama pamoja na waume. Kikazi, kimiaka, tuseme ugawanyaji wa xxxx. Wale wote wanapatiwa huduma ni sawa. Lingine, ningelipendelea, katika office ya kazi ambayo inahusu waislamu sana. Kazi ameandikwa na serikali, kwa kazi anataka mshahara wake kutoka kwa serikali lakini unakuta ambapo serikali hatunaye haki yake kwa waislamu. Tungelipenda, waislamu wenyewe wajichagulie kazi na baada ya kujichagulia katika hilo kiti, kazi mwenyewe na apewe na mamlaka, tuwe na judge ambaye anaweza kuhukumu katika shelia za kiislamu ingawa jia itakuwa ni moja, lakini hukumu, ikiwa ni hukumu na unatoa kutoka kutoka kitabu cha Koran , kwa nini mtu asihukumiwe katika haki yake, ya kiisheria,

ya diini yake.

Ya tatu, ningelipendekeza mambo kuhusu freedom of worship. Hii kitu inaitwa freedom of worship ningelibadilisha kidogo iwe freedom of religion. At least mtu anaweza kujichagulia, kama yeye anataka kuwa muislamu, ana wataka kuwa mkristo, lakini sio kama vile sasa dini zimekuwa nyingi sana mtu ata hajui mahari pakwenda. Sasa watu wanapotea sasa, kwa sababu ile kuzingatia ndio umepotea. Unapata ama kibanda mtu akiona ni biashara anaanza, anaona kuna freedom of worship. Sasa unaona unakuta watu wametumia that pigment vibaya. Wanaitumia vibaya sasa imekua ni kama biashara, unaona leo ata mtu akikondesha kibanda ya sukuma wiki anatafuta wazi wazi, anatafuta pesa katika jina la yesu. Pengina tu hio roho ya kujua kuhubiri, tayari wewe umepata kanisa. Na sisemi hivyo ati kwa sababu ninacritisize Christianity, apana, Mungu ni mmoja, na tafadhali mnielewe vizuri sana, unajua mambo yakiwa mengi sana, kuna mahari kuwa inaenda inaleta shinda. Kwa nini? Xxx sasa unakuta hizi dini, zimekuwa mingi sana mpaka watu wanakosa njia kabisa, na watu wanatakikana wawe na mwelekeo ya kujua wanaelekea wapi. Nafikiri ni hayo machache tu, sina mengi ya kueleza.

**Commissioner Lenaola:** Asante Asha, umesikika vizuri, jiandikishe pale. Pius Ouma, Pius Ouma, John Okero Okumu, Oh, sorry David ulikuwa next, samahani,

**John Otieno:** "I have a chair that don't worry". My name is called John Otieno, I'm a shoe shiner, shoes repair, that I want to talk some words. Kwa hivyo mimi, ukiangalia mbele unaweza sema ati mimi niko disabled, yaani sina mguu yangu. Lakini niko na kichwa yangu, na mkono yangu yanafanya mzuri, sasa kwa hivyo ndio natafuta kitu yangu. Sasa nataka kutetea that disabled person like me. Iko watu wengine hawana miguu wala mikono na hawezi kutafuta vile mimi naweza kutafuta kidogo. Kwa hivyo nikichukua vimbo zangu nipeleka kwa barabara kwa streets huko town, nitafutisha corner, iko watu wengine wanaitwa wa City council, wana interfere kwa somebody like me. Hata juzi walijaribu kunyang'anya mimi kitu yangu ya kupigia langi, sasa sina nguvu ya kutafuta, kwa hivyo sijui watu wanataka mtu kama mimi akae chini aombe watu nisaidia, nisaidie, nisaidie, na mimi ndio naonanga kama hizo ni ngumu na mimi. Kwa maana nikifanya peke yangu ata kama ninakula, naona kama niko na furaha, kwa maana Ok. Hakuna kitu ambaye ninatengeneza, unaweza kaa na furaha kuliko ukikula kitu ambayo mtu anakupa wewe. Sasa ninapendanga hizo by that hakuna mtu ambaye anaweza boast to me, niendelee vizuri na kazi yangu, xxxx mzuri niweke stool hapo chini, whatever I want, hakuna. Sasa, kuna watu wengi ambayo wako kama mimi, hao watu wengi wao hawana kazi, hana ujuzi ya kutengeneza ata viatu kama mimi, sasa, na ako na mkono, ako na macho, kichwa yake ni mzuri, kichwa yake haijaharibika, unaweze sena watu wengi kama mimi lakini ndio wanasema, kwa hivyo kichwa yake yameharibika, lakini mtu ambaye kichwa yake yako mzima kama mimi, awe ata ni mzima kama mtu anatembea, lakini ni vizuri apate pahari pengine ambaye anaweza kufanya kitu yake, kama kuuza. Sasa nasema watu kama City Council, ama county council wawache kuinterfere with somebody like that. Kwa hivyo mtu akitafuta, xxxxx kwa nyumba yake, ukule hapo, uweke hapo, ufanye kitu chochote hapo, upate nguo upate nini. Kwa hivyo mtu akikupa wewe nafasi ya tutengeneza yako unaweza kuona vile unaweza fanya, but there is no more, I'm so happy, Yah. God bless you so much.

**Commissioner Linaola:** Thank you George, goja kidogo nina swali.

**Commissioner Salome:** Asante sana George, hao ni maoni mazuri, Tunakutakia kila raheri na kazi yako lakini tungetaka wewe utusaidie, kutupa mapendekezo, ungetaka kuona watu walio na ulemavu wakisaidiwa kivipi na katiba yenye tunaweza kutengeneza wakatu huu? Umetuelezea vile city council askaris wanafanya, wanawafanya na vile wanawasubua lakini kwa katiba mpya ungetaka kuona kuwa mmelidwa kivipi ili muache kusubuliwa?

**George:** Thank you so much, I'm so happy – kwa hivyo ndio maneno kama hiyo ndio naona kwa watu kama hao anatengeneza usafi kwa town. Sasa kutengeneza usafi, sio kutupa visu vya watu za kutengeneza pesa ama kutengeneza mali, kwa maana hapa Nairobi kuisi ni pe? Ni pesa. Ukioga unaoga na pesa, ukifanya nini ni pesa, kila kitu ni pesa. Sasa kama kila kitu ni pesa na mtu anachukua kitu yako ambao unatengeneza nayo pesa, anatupa ama anaenda nayo, anaenda kumpa mtu mwingine, ama anaenda kutumia vibaya, something like that is not good.

**Commissioner Lenaola**: George, kwa maoni yako joo nenda pale ujiandikishe, tumeshkuru. John Okeyo Akumu, John Okeyo Akumu, Andrew odinya. Karibu mzee, chukua microphone pale, sema majina yako kamili alafu utoe maoni yako.

**Andrew Odinya:** Hamjamboni, mimi naitwa Andrew Odinya, chairman ya KANU Dandora B. Mimi nataka ongea upande wa Petrol Stations, sababu sisi iko hapa kusaidia wale wadugu yetu, hawajui kitu gani inaendelea. Ndio nampa hawa wanakuja hapa, kwa hivi heri tukae hapa kama tunajua tunasaidia hawa na nini. Mimi yale naweza ongea, ni upande ya election, yaani uchaguzi, nataka chagua chama, chief, area mtaa. Na pendekezo ya kwamba, hawa, msipochaguliwa na laiya, sababu kuchaguliwa na laiya ni hii, saa ile nafanya kosa, tutarudi sisi laiya chini tukae tujue huyu sisi ndio tulimchagua, tuangalie mtu mwingine tuweka, sababu ninaona ya kwamba, hapa Dandora, tuseme mtaa yeyote, ukishachagua mtu ata kwa welfare, yeye anafanya tu kivyake sababu yeye anajua yuko pale peke yake. Lakini kama umechaguliwa na laiya, saa ile anataka kufanya kivyake, sisi tutakataa, na tutaweka yeye chini, tutamuambia leo tunatoa wewe tunaweka Andrew. Sababu, hao watu mnachaguliwa, kitu ikitokea kidogo, jioni mtu anatoka chini anaenda kwa nyumba yake, nabeba kibunda ya pesa na mpa yeye, yeye nakXXX masikini saa zile anataka, hiyo ndio anampa. Mimi naomba, katiba ya saa hii iwekwe hiyo ichaguliwe na laiya.

Ya pili, nataka kuongea kwa upande yetu ya police, police, upande ya police ni hii, mimi ni mzee, natoka kwenda kununua mboga yangu, kufika kwa njiani, naambiwa kaa hapo, kukaa hapo, atakuja atembeze miiimi, kufika anaangalia saa na anaenda, anasema mzee uko na nini? Lazima nitatoa ata mia mbili, nitoe sababu sitaki kutembezwa kutembezwa mchana mzima. Na hiyo, mimi naomba, katiba saa hii, huyu anaitwa police, awekewe hatua hio bila kukosa, achukuliwe hatua kwa sababu anaangaisha laiya ile hana kosa. Hiyo ndio pendekezo yangu, upande ya police. Kidogo tu hivo, mi namaliza,

**Commissioner Lenaola:** Asante sana bwana Ondinya, kwa maoni yako, jiandikishe pale kwamba umetoa maoni. Tunamwita mheshmiwa Mwenje sasa aseme machache kwa maana ako na mkutano mwingine angependa kwenda. Karibu Mheshimiwa pale.

**Mheshmiwa Mwenje:** Mimi sitaki kuketi chini, nataka tu kusema mawili matatu nienda kwa sababu nina mkutano mwingine, na nimeona kuna haja nipitie hapa. Na kesho pia nitapitia Mukuru sababu constitutional review committee ile iko hapa, ilikuja hapa, na ilikuja pale Kayole na watu walikuwa wengi na wakatoa maoni yao. Lakini wakati tulienda kule kumuona bwana chairman, na commissioners wale tulikua nao, Muigai na wale wengine, tulikubaliana watarudi hapa sababu nyinyi hamkupata nafasi ya kupeana maoni yeni wakati ule. Embakasi constituency mnajua ni kubwa, na mpaka sasa si ndio tunaongoza katika Kenya mzima, kwa mambo ya voters, registration nikusema ata watu sisi ndio wengi, kwa sababu sasa tuko na 186,000 registered voters, tukilinganishw na Baringo ile iko na 42,000, kwa hivo tuko wengi, na kama mtaenda Baringo mara moja, mtatakiwa kurudi Embakasi mara sita. Lakini nafasi hii, tuliuliza ndio nyinyi mpate nafasi hii ya kupeana maoni yenu tena kwa commissioners. Na ninafikiri ni vizuri mumekuja, nilikuwa nafikiri wengi sababu watu wengi waliniambia hawakupata nafasi ya kuonyesha maoni. Lakini nataka kurudia ile kitu nilisema huko, tuna tabu kidogo kwa sababu nyinyi ambao mnapeana maoni, wengine wenyu mpaka wa sasa hamjaona hiyo kitu inaitwa katiba. Na hebu niulize mpaka sasa wale mnapeana maoni hapa, wagapi wameona katiba? Mmoja tu. Na mwingine pale, Ok wacha tuseme ata kama ni kumi, kama ni watu kumi na wale wengi hawajaona katiba, wanapeana maoni gani na hawaajui katiba ya sasa inasema je? Na ni mahari gani hiyo tunataka kulekebisha? Commissioners, mlianguka,sababu hamkuja kufundisha watu, hamkupatia sababu ya kutosa tufudishe watu katiba. Hio ni kweli? Sababu ilie mnapeana sasa ni makosa, ile mnaonanga lakini maneno ya katiba, hamsemi! Nikisikiliza wale wote wanaongea hapa, mnaonge mambo, tabu ile mnapata, tabu ya City Council, tunakuwa harassed na city council, mnasubuliwa na police, na ni kweli ata sio nyinyi ata mimi, ***(cheers)*** mnajua hio?

**Watu:** (yes)

**Mwenje:** Na hio ndio ile kitu iko kwa roho yetu, na ni kweli hio mnasema. Lakini wacha nimuambia, hawa mnawaona hapa wanaandika, hawaandiki hiyo, sababu hiyo haihusu nini? Katiba. Hiyo ni complains na labda ile committee iko hapa, ni complains committee.

Tuiambia macomplain yetu. Lakini ya katiba, ile tunasema, hakuna mahari inalekebisha nini? Katiba. Sifikiri nimeeleza hio muelewe? Sababu katiba ni ya hii mnaona hii mnaona mimi nina shika. Hili ni katiba, na katiba hii, ndio hawa wameitwa na mbunge, waenda wachukue maoni kwa watu, wajue ni mahari gani tunataka kulekembisha, ndio mambo hiyo iwachwe kufanya. Hii ingine ni complain, na tuna complains nyingi, juu ya serikali hii yetu, complains nyingi kubwa. Mimi mnasikianga nikisema bunge na pia nyinyi mnancheka, hiyo ni kweli. Lakini ni kweli pia, mambo haya, makosa hii yote inatokana mwishowe na nini? Na katiba. Sababu hio nguvu, hio, hio, ya hiyo mambo wanafanya, mwishowe imeenda ikatokana na nini? Na katiba. Mna nielewa? Katiba hii, matatizo hii, imetokana na kwamba, serikali ikifanya makosa, ni nani anatakiwa kushtakiwa? Nani mkubwa wa serikali? Si mjibu, nataka tuelewana, ndio nimuache mkielewa vile mtaambia hawa. Ni nani anaongoza serikali?

**People:** President.

**Mwenje**: Kwa hivyo serikali, serikali kwa hivyo ni nani? Ni President! si kweli? Sababu yeye ndiye amechagua mawaziri, yeye ndiye amechagua commissioner wa police, (yule alikuwa hapa bwana, huyu alikuwa anasema complain ya vile police wana shikashika nyinyi hapa ata saa moja, saa mbili, ukipelekwa kinyago huwezi kuwachiliwa mpaka utoe elfu moja; si ndio? Si hiyo ndio kawaida, wakitaka kulokota elfu mia moja na siku moja, ni kushika watu mia moja, jioni unawachiliwa na elfu moja.)

Lakini police hao wanafanya kazi chini ya nani? Ya nani?

**People:** Commissioner wa police

**Mwenje:** Commissioner amewekwa hapo na nani?

**Mwenje:** Na President. Ukitaka kushtaki yule alipatia hawa hiyo kubwa ya kufanya mambo, Unaweza kumshtaki? Katiba No. 14 hapa, inasema, sikizeni msomewe katiba NO. 14, inasema nini? (No crimimal proceedings, whatsoever, (whatsoever) shall be instituted or continued against the President while he holds office). Ati huwezi kusitaki nani?

**People:** President.

**Mwenje:** Ata akifanya nini, ata akiua, ata akifanya nini, huwezi kumshtaki. Hakuna kitu kinaitwa above the law! Hiyo ndio watu wanaitanga above the law. Kwamba huwezi kusitaki President. Kwa hivyo mngesimama mseme, clause No. 14 iondolewa, ndio President aweze kufanywa nini?

**People:** kushtakiwa.

**Mwenje:** kushtakiwa akifanya makosa. Na hio wataandika hapa. Watajua mnajua ni nini mnasema. Si kweli.

**People:** Ndio

**Mwenje:** Wagapi wangependa tuondoe hiyo? Mtu wote akifanya makosa ashtakiwe?

**People:** Noises, ashtakiwe, ata President.

**Mwenje:** Kwa hivyo, Madam Muigai, commissioner Muigai, andika. Hiyo yoote complain inatokana nakua huwezi kumshitaki nani?

**People:** President.

**Mwenje:** Na hiyo ataandika iletwe bunge tulekebishe – ata President akiua, akishtaki, akifanya nini kama ile walifanya pale juzi kwa watu wa matatu, afanywe nini?

**People:** Ashtakiwe.

**Mwenje:** Apana kushtaki Mwenje, badaala ya kushtaki yule ameua. Sababu yeye amezuiwa kushtakiwa sababu ya? Katiba. Hiyo ndio mnatakiwa muelewe ndio muweze kuwaambia waandike hiyo abadilishwe. Nimeona ingine hapa, kama ile Asha amesema. Dini, section 78 ya katiba hii, inasema, kama mtu anaweza kuruhishiwa kuomba na njia yeyote ile anataka, yeyote, kwa hivyo, ata wale wanaomba shetani, katiba hii inafanya nini? inawaruhusu. Nyinyi ni wakristiano na waislamu lakini huwezi kuzuia mtu kuomba nani?

**People:** Shetani.

**Mwenje:** Sababu katiba hii, imemruhusu, hiyo ndio angesimama aseme, sisi tukubaliane sheria iwekwe. Section 78 iwe amended iseme. "wanakenya wataomba tu, mwenyezi Mungu" awe ni kiislamu, ama ni kikiristiano lakini aombe nani? Mungu . ilekebishwe hio. Sababu mtu naye akitaka kujenga kanisa ya shetani, (mnasikianga devil worshipper?) akitaka kujenga kanisa ya devil worshipper pale huwezi kumzuia. Kama plot ni yake, lakini katiba yetu izuie hio. Na hio dio 78.

Ile ingine, kile kimeleta tabu hapa Kenya, ni mambo ya (mnaona leo mtu kama President, section 15 ya katiba hii, na ndio ninamwambia, tabu ile mnayo ni kwamba, hamuielewi, hamjafudishwa, katiba hii inasema nini.) Katiba hii section 15 inasema "There shall be a vice President of Kenya who shall be appointed by? The President. Sasa President akiappoint vice President,

si anaweza futa yeye kesho.

**People:** Ndio

**Mwenje:** Si ndio? Sababu yeye ndiye alimuandika. Lakini mahari kama America, President hawezi kufuta vice President. Ndio mnaona vice presient anakaa kama mtu hajui ata anaelekea wapi. Juzi ata akapelekwa kasarani, ata kiti hawezi pewa na hawezi omba sababu akionge kindoga atafanya nini?

**People:** Atafungwa.

**Mwenje:** Ndio unamuona ata anakaa Ndeee, hana nguvu sababu hakuchaguliwa, yeye alichaguliwa na President. Katiba hii tulekebishe, vice President na President wachaguliwe na nani?

**People:** Na laiya

**Mwenje:** Na laiyaaa, ndio hio unaweza kuambia mwingine (Were unakosea) Mimi ndio vice President wa Kenya hii, na nimechaguliwa na watu, ninakosea. Sasa vice President anaweza kuambia President namna hio? Juzi nilimuona akifanya mikono na mna (show of hand) , hio peke yake, karibu aondolewa kwa kiti. Si ndio? Sababu hana nguvi, ata afadhali Mwenje. Sababu mimi nitaongea ni mambo ya wananchi wamenichagua. Si kweli?

**People:** Ni kweli.

**Mwenje:** Lakini huo ataongea na kesho atafutwa anyang'anyw hio gali tatu, tafadhali ata kamwenje kama mimi. Kwa hivyo hio ndio kosa mngesema, section 15 of this constitution ilekebishwe tuwe tukimchagua vice President and President achaguliwe na laiya. Andika hio. Ni wagapi wamekubaliana na mimi kwa hio? Ile ingine, ile ingine, ukitoka kwa section 16 kutoka hio 15 ya vice President, uingie ya mawaziri, inasema hivi, (Ndio mjue mahari mngekuwa mkisema ilekebishwe ndio mambo iwe sawa, hii ya City Council na nini, hio ni complain; lakini ile wamekuja kuuliza hawa, ni mahari mnataka katiba ifanyw nini?

**People:** Ilekebishwe.

**Mwenje:** Na msiposema, hawataandika, na wakikosa kuandika, haitaletwe bunge tulekebishe. Kwa hivo makosa hio, itaendelea ata mwaka ujao. 16 inasema " there shall be such offices of ministers of the government of Kenya as may be established byyy Parliament." Mawaziri wanatakiwa mambo yao, wizara, inatakiwa inatengenezwa. (chief Karibu) inatengenezwa na nani? Katiba imesema na nani? Mawizara inatakiwa kutengenezwa na nani?

**People:** Na parliament

**Mwenje:** Kwa sasa, inatengenezwa na nani?

**People:** Na President.

**Mwenje:** Na President, President akitaka kesho kusema ameongeza mawizara , ataongeza, akitaka kusema imepunguzwa, inapunguzwa. Hailetwi bunge. Hio ndio moja mngesema tunahitaji iangaliwe kikamilifu. Iongezwe nguvu kwamba wizara la mawaziri (pengine mawaziri ni wengi katika bunge hii yetu) na wale wote wanawekwa kwa kiti y waziri, ni sababu bunge haiangalii, haina nguvu ya kufanya ile inaitwa veting; unajua veting ni nini? Veting ni tatumia lugha gani na kiswahili? Inaitwa nini? Veting – kuchungulia. Si ndio? Hakuna waziri amewekwa kwa kiti akishachunguliwa na? Na bunge. Namjue saa ile anachunguliwa na bunge, ni kusema anachunguliwa na nani? Na laiya. Sababu bunge imechaguliwa na nani? Mimi nilienda bunge nilichaguliwa na nani?

**People:** Na President..

**Mwenje:** kwa hivo ninasema kitu bunge, nina sema kwa niamba ya?

**People:** laiya

**Mwenje:** Yenu. Lakini mawaziri anachaguliwa na President bila kuchunguliwa na bunge. Kwa hivo ata mwizi atachaguliwa awe waziri. Sababu ni rafiki ya nani? Ya President. Ndio mnaona bunge yetu ina mawaziri wezi. Sitaki kutaja jina ya mmoja. Lakini ata bila kutaja si mnawajua?

**People:** Tunaelewa

**Mwenje:** Tena ndio mngesema section 16 iongezwe, kwamba mawaziri wachunguliwa na? Na. Bunge. Na iongezwe hapa. Wagapi wanakubaliana na hio? Wagapi wanakubaliana na hio? Apana hapa hawakubali. Nyinyi mnataka hio?

**People:** ndio

**Mwenje:** Mambo haya ndio mambo ambaye tunatakiwa kuichungulia sababu (eh najua mnafurahi lakini nataka mniskirizi, ndio muelewe – katiba hii mwishoe ndio itamletea matatizo, sababu isiolekebishw na mna hio, na itengenezwe namna hio, ile tabu tunasema sasa, ingali itakueko ata mwaka uja? Ata baada ya uchaguzi. Lakini sasa, tunaongea mataabu yetu, ni kweli inatokana na hapa, lakini ni lazima uambie hawa, mahari unataka ilekebishwe ndio iandikwe, sababu mahari watu wengi itaonekana wamesema, ndio hapo.

Kuna ingine moja sitaki kusema sana, ndio nimache na nyinyi mseme. Ata ingawa nimeona ni complains, naunajua hawa hawatamwabia hivo, wataandika tu, lakini watapeleka ile inahusu nini?. Kenya hii yetu, leo ukipata tabu nikienda niulize swali katika bunge, nauliza mawaziri. kwa ni mtu fulani – Njuguna Waithaka aliuawa Dandora? (si mnakubuka yule aliuawa Juzi.) Nikienda leo niulize bunge na nitauliza tukirudi, ni nani aliua Isaak Njuguna? Dandora, waziri wa security, (Sunkuli) atasimama anijibu ile atanijibu, lakini yeye atajibu ile itafurahisa nani? Yule alimuandika. Aliandikwa na nani? Na President. Kwa hivyo sitajibiwa vizuri. Kwa hivyo tungetaka yule anachagua mawaziri hawa, akae pale tumuulize swali. Katika wilaya, yule anajibu maswali ya serikali, ni nani? Nani anajibu maswali katika serikali ya wilaya. Ni Prime Minister. Si ndio? Sababu yeye ndie alichagua nini? Mawaziri hawa. Na yeye ndie answerable kujibu. Kenya yetu, President haendi bunge, hakujangi bunge, isipokuwa siku ya kufungua bunge na siku ya budget. Kwa hivo wale watu unauliza, hawawezi kukujibu vizuri; sababu wanaogopa nani? Kenya yetu imefika kiwango tunahitaji mtu ya kuja bunge, kujibu maswali, ya nchi yetu (prime minister) Kenya tuna prime Minister? Mngetaka tuchague Prime Minister, yule atajibu maswali katika bunge?

**People:** Ndio.

**Mwenje:** Kwa nini hamsemi hio? Mtasema hio, wagapi wanataka tuweke hio? Weka hio! Tunahitaji Prime Minister yule atakuja kujibu maswali ya serikali, kwa nini hii imefanyika? Kwa nini hii inafanyika? Kwa nini hii inafanyika? Na yeye awe pale ndio akijibu vibaya, wananchi wasikie, afutwe na wananchi. Lakini kama yule anajibu ameandikwa na President, utaweze kufuta ye wewe? Huna nguvu. Kwa hivyo tunahitaji mtu ule atajibu maswali y serikali. kwa nini? Nani amesema, wapi huyu

jaduong men – amesema – huyu, anasema wanasikwa hapa saa moja anapeana mia mbili, utauliza nani? Na police huyu amamuandika – tunahitaji yule amemandika aje bunge ajibu nini? Swali. Na huyo ndie anaikwa Prime Minister, tunahitaji prime minister katika Kenya yetu sasa (whether ikawa itakuwa mimi) (laughter from people) si kweli? Hio kiti ikija mtanichagua mara moja?

**People:** Sawa

**Mwenje:** Kwa hivo tunahitaji kwa katiba, ndio tuwe tukiuliza maswali haya. Kwa hivyo kuna aja ya nyinyi kuelewa katiba hii, mambo ile iko na ile tunataka kulekebisha. Ile inahitajika kulekebishwe, sababu tusipofanya hivyo, taabu hii itaendelea, na tabu hii itakuweko, na wale wengine, wale wanataka kuitengeneza, wataitengeneza. Ile ingine ningetaka kuwaabia commissioner wa kiwa hapa, Kuna wale wanasema tunatake katiba hii iendelee kulekebishwa mpaka mwaka ujao. Bunge iongezwa mnda. Ndio twendelee mpaka mwaka ujao. Na wendelee kutusikiliza wa kiandika. Wakiedelea mwaka ujao, kwendelea mbele, ni kusema bunge lazima iongezwe nini? Mnda. Tungetaka waandika, sisi tunataka kwenda kwa uchaguzi mwaka huu. Wacha wale wanaogopa kule bunge waogope. Nyinyi mlituchagua miaka 5 na tungetaka tukae miaka tano, hatutaki kuongezwa, ndio wale wabaya wafanye nini?

**People:** Waondoke

**Mwenje:** Waondoke, lakini wale wanaogopa watafutwa nafasi yao, wanaogopa uchaguzi, wanasema tuongezwe mwaka moja, Mimi nasema sisi watu wa Embakasi tuseme apana. Twende kwa uchaguzi ndio tuchagua wale watu wazuri anende nyumbasi, ndio ata serikali tunayo ienda nyumbani kwa sasa sababu imetusubua yakutosha. Mimi siogopi uchaguzi, naitaka sasa. Si kweli? Kama niuchaguzi kuna mtu ataondoa mweje? Ukweli ni , nataka waadike, watu wa Embakasi wanasema hawataki uchaguzi mwaka ujao. Wanataka uchaguzi mwaka mgani?

**People:** mwaka huu

**Mwenje:** Waandike hio. Na ya pili nayo, tuwaambie pia, tunataka mambo hii yao ya kuandika katiba, ikwishe kabla ya mwezi wa tisa. Ndio iweze kuletwa bunge tuipitishe iwe sheria, Si kweli? Mambo ya commission pia kusema iongezwe munda, tunakataa, ata hio. Kweli? Wagapi wanakubaliana na mimi? Hatutaki commission iongezwe muda, tunataka wamalize mwaka huu. Wakitaka kulekebisha ingine tutawapatia nafasi mwaka ingine tulekebishe. Lakini kwa sasa ilekebishwe hio. Kuna wengine wanasema, tulekebishe kidogo kidogo, tuweke Prime Minister, tuache hio ingine, tuache , tufanye nusu nusu. Sisi tunasema isifanywe nusu nusu, imalizwe yo?

**People:** yote

**Mwenje:** Katiba yote imalizwe iletwe tupitishe. Hatutaki hii mambo ya watu wachache wanajitengenezea. Ya pili na ningetaka hio iwe clause mpya, "President ambaye anayeondoka, alikuwa kwa kiti, awe banned kufanya campaign kwa watu wengine,

**People:** Ndio, ndio, hio ni sawa.

**Mwenje:** Ee, hio iwekwe? Wagapi wanakubari tuweke hio? President akiondoka, (unajua sisemi Moi) nasema yeyote atakuja, President yeyote, outgoing President should not campaign for anybody. It should be left to the public to decide.

**People:** Yes, yes, in agreement

**Mwenje:** Iwekwe clause mpya kwa katiba, hakuna mtu anazunguka kila mahali anasema oh, nitawachia nani? Unawachia nani kwani ilikuwa yako? (laughter) Si kiti ilikuwa ya laiya? Laiya wawachiwe wachague yule wanataka. Sio kuambiwa na yule anaodoka. Outgoing President should be banned from campaigning for anybody. Sisi ni laiya wa Kenya na sio wa mtu fulani. Ukipewa, unakalia hio mda umepewa. we at hamuandiki? Yes tukona haki ya kuona kile wameandika. Atatusomea tusikie kile ameandika, si ni kweli?

**Commissioner Lenaola**: Outgoing President not to be allowed to campaign for others.

**Mwenje:** Iko. Ameandika (clapping and laughter) sawa nakubali kama umeandika. Hio ni haki yenu, na sasa ndio wakati wenu wa kusema vile mngetaka. Lakini ni mbaya sababu hamkuweza kusoma katiba hii, na hamkuweza kufundishwa hii inasema nini. Nilikuja Dandora nilifundisha wachache, natulikuwa na wale tulikuwa nao tulifudisha wachache. Lakini bahati mbaya haikufikia kila mtu, sababu, commission haikutupatia pesa ya kutosa kuandika watu wakutosha kufundisha. (noises) kila mahari ingeandikwa. Kitu hamjui, nikikalibia kumaliza,

**Commissioner Lenaola:** Mheshimiwa please

**Mwenje:** Nikikalibia kumaliza ya mwisho, najua nimechukua muda lakini, kubuka nina mandate

**Commissioner Lenaola:** Unajua uko kwako nikakupatia dakika ingine mingi, kwa vile uko na watu wako. Sasa pia hao tuna wapa nafasi pia

**Mwenje:** Akubuke nina mandate kutoka kwenu, na yapili ata wakileta ni mimi nitapitishe bunge. Wanaweza kuileta niipige ikuwa bunge. Ya mwisho, ni hii, kile kinasubua watu wetu Nairobi hii ( hii ni ya Nairobi) ni sababu city council inaendelea kuharass watu, na ni askali wetu, wanaharass watu, kiost inafujwa na mtu alipewa kiosk. Na anafujiwa kiosk – sababu yule anakalia kiti ya Nairobi City Council, ama municipality, yule anitwa mayor, anachaguliwa na macouncillors, what hivo yeye hana aja na laiya, ana aja na?

**People:** pesa

**Mwenje:** na councilors kuwapatia maplots na nini na nini. Iwekwe kwa constitution ya Kenya kwamba mayor wa jiji la Nairobi na matown ingine atachaguliwa na laiya.

**People:** ndio, ndio (clapping)

Mwenje: Iwekwe kwa constitution ya Kenya, apana ile sheria Minister analete pale bunge anasema CAP 265 itakua amended. No, ingine kwa constituion, kwamba mamayor watachaguliwa na nani? Na laiya, Ndio akifuja kiosk mayor moja mnafuta yeye. Sasa nyinyi hamna nguvu kufuta mayor sababu yeye amechaguliwa na nani? (madiwani) Achaguliwe na laiya, iwekwe kwa constitution.

Na ya mwisho kabisa, hapa Kenya, tunatofauti ya masikini na tajiri, matajiri wanaonekana wana right kushida masikini. Masikini wale wanaishi manyumba hii – hii gitari marigu huko chini, na yule mtu anaishi Muthaiga, wanaonekana sii sawa. Inaonekana iwe restricted kwamba, watu wote ni equal lakini serikali serikari ikakuwa na emphasis ya kusaidia wale masikini wanaishi kwa shanties, kwa slums. (clapping) ata kama tuko equal kwa mambo ingine, lakini serikali iwe na nia ya kupromote hao watu wanaishi nini? Iwekwe pia kwa constitution. Natukiwa na mambo kama hio, constitution yetu itakuwa sawa. Lakini kwa sasa, nitamuacha muendelee na kusema maoni, ingine itakuwa ni complain, ingine itakuwa ni nini, lakini ukweli ni kwamba mjue tabu yetu inatokana na hii constitution, sababu wale walitengeneza hii walikuwa na nia ya iwasaidie, na isizaidie masikini ya

Kenya. Lakini zote tuko sawa. Isipokuwa ata tushinde, ata wakikataa, mbele za Mungu tuko sawa. Asanteni

**Commissioner Lenaola:** Asante sana mheshimiwa, tumeshukuru mheshimiwa kwa maoni yake, Ningependakusema mambo mawili tu, ili tuendelee. Jambo la kwanza, kwa maana wengine wamechelewa kuja, recording ya hii shughuli, linafanywa kwa jia tatu.

- recording – kuna hii wa kunasa sauti (neno kwa neno) na baada ye tukienda katika tume tutatlanslate neno kwa neno.
- Jambo la pili, huyu mama anaandika kwa shorthand; shorthand pia ni neno kwa neno. Tuna kijana anaandika kwa long hand, maana yake pia neno kwa neno.
- Na sisi hapa mawatume tunandika pia nene kwa neno. Kwa hivo kila jambo abalo mna lo sema hapa litakuwa recorded neno kwa neno.

Kwa hivo sio kusema pengine kama mimi sijaadika neno, nimepotea, halijapotea, tuko na jia nne za kurecord, na baada ye zote zitakuwa recorded katika tume.

Jambo la pili, yale maoni mmeyatoa, ni lazima myatoe kulingana na section 40 section 70 section 90 ya katiba ya sasa. Msungumze kulingana na mambo ambayo mnayo yasikia mna yajua. Mimi ni wakili, lakini si kila mtu ni wakili ama ni mbunge mheshimiwa Mwenje, na shinda zenu zikuwe lugha ya kingereza ama lugha dani ya kiisheria, mtasema shida zenu katika lugha mnaoielewa. Kazi yetu kama wanatume, ni kutranslate hizo mashinda na pendekezo kwa lugha ya katiba. Kusema juu ya police, juu ya mashamba, juu ya maplot, juu ya macouncillors , juu ya machief, hiyo ni lugha ya katiba. Na kazi yetu kama tume ni kutranslate hio lugha yenu, kwa lugha ya katiba. Naingine nimesema leo asubuhi ni , katiba ya sasa (ile mheshimiwa amawasomea) ni lugha yake ngumu, kingeraza queen alitutawala. Hata tukiwapa sasa hivi, hamtaelewa, namtatwabia hivi, katiba ijao iwe ni ya city langu. Ili kila Mkienya aelewe. Kwa hivo ni sasa ile katiba tuko nayo, ni ya shinda, kwa maana hatuelewi. Lakini tumesema hivi, katiba ya baadaye iwe je? Kwa hivyo maoni yeu mimi la mwenzangu mwenzanu tumesema hivi: myatoe maoni yenu katika mioyo zenu, uchungu wenue muutoe, lugha ya katiba abaki kwa tume. Tumeelewana? Tuendelee? Sawa sawa, dugu yangu Abdulah Mohammed. Ebu joo.

Abdulah Mohammed: Hamjamboni? Mimi Abdulah Mohammed. Yangi ni mazito kidogo lakini nitajaribu in fupishe. Kwanza mimi vile niliechola kipande inaotumika hapa Kenya na noti. Yaani mimi abdulah mohammed ndiye nilichola ile kipande inaotumika hapa Kenya na noti. Sasa sikizeni vizuri inayotumika hapa Kenya. Ni mazito kidogo, sasa wakati huo, 1971 nikiwa school, Starehe ndio ilinitangulia masamo yangu nikiwa mtoto wa tima ama mtoto wa kulewa na mama wa mbali. Nimelelewa hapa hapa Eastleigh kwa hivyo siwelezewi mengi kuhusu Eastlands, nimejionea mwenyewe. Sasa, kwanza nitashkuru tume, imejitolea kuja hapa kusikia maoni yetu ambazo hazingelizikizwa. Mambo ninayo yasema ya noti, si yangu binafsu, labda kuna wengine wenu pia mmefanya mauradhi furani na mmejaribu kuyatulizwe na kuwa ni gumu. Tusema kazi ya pesa, matumaini yangu ya kuchola noti, ilikuwa vuke mbeleni ilikuwa 1971 hadi (tusema tangu uhuru) 1963. Tangu uhuru noti ilikuwa ya kumi hadi 1973. Nayo nilikuwa nimeichola 1971 hapo tulibadilishia wakati wa ayati marehemu mzee kenyatta. Lakini vile nilikuwa school nilivyotoka school nilikwenda jeshi. Nilijaribu kutafuta kazi kama laiya, sikufanikiwa. 1972 yaani niliandika mabarua ya kutafuta kazi ( applications for employment) lakini hazikupata kama laiya. Sasa niliamua niende binafsi jesi.. Huko jesi wakati

wa mazoezi, mwaka ule ule 1972, mwili ulinikauka ikabidi nipate discharged. Sasa msione ni statement yangu mwenyewe, nilisemavyo

**Commissioner Lenaola:** Abdallah ningependa, ungetoa maoni juu ya katiba ,yako ungesema juu ya katiba lakini si mashida zako, tungeomba, tunakuelewa lakini nasema tafadhali nenda katiba,

**Abdallah:** Ni mazito na jaribu kufupisha,

**Commissioner Lenaola:** Tumpe nafasi? Tuheshimiane,

**Abdallah:** Waona wakati ule katiba haikuwako, nilijaribu kufuatia hio kazi ya hizo noti, na dio nimemuambia ya kwanza ilikuwa kubadilisha hili noti inaitumika, kutoka ile picha ya marikia, iwe ya picha ya mkenya. Arafu ya pili ilikuwa nikibainia Kenya wenyewe tutajichapishia pesa, yaani, zilikuwa zinachapishiwa ng'abo. Sasa vile tume wamejifikisha hapa, nimejaribu kumuandikia ata rais (hatuko hapa kumstaki Rais) niliona mheshimiwa Mwenje alisimama akashtumu vikali. Rais si wao, kunainiwa, lakini nimejaribu kuandika barua kwa jia ya posta na hazifiki tuseme, na yuko mama mwingine secretary labda wanasoma ofisini, niwazuri wanasema huyu jamaa aabishe, anapinga. Unaona, na si mimi peke yangu kuna wengine pia labda na kazi la kabla hii. Yaani I have notes ni za xxxx yaani amekujwa, vilivyo, hata mama mwingine alikuwa hapa akasisitiza utumiaji wa pesa hapa Kenya umekujwa, tusema wanajiinua wao kwa wao matajiri. Century tuseme. Na huku kando labda pesa haiwafikii. Wananchi, kitu ilioko, na nyenyekea tume mwasikiza, nawanyenyekea sana, mfuatie kazi hii, kama Kenya mjue mchague maRais, yaani ata kama ni kwa Rais mwenye nyinyi wenyewe; Mjue kama pesa inachapishiwa hapa, mnaona it is a way of a complete errudication. Umasikini uko mwinge, mfuatie hii kazi

**Commissioner Lenaola:** Ya - tumeshukuru

**Abdalla:** Pia nyumba, unaona kuna upande ya nyumba ningepitisha. Dandora wakati huo zikijengwa, ilikuwa gumu, ilinibidii niandike barua kwa United Nations.

**Commissioner Lenaola:** tumesikia sasa hayo, natuone kama umeandika hio barua tutaichukua.

**Abdallah**: Na si harari mwananchi kujenga kutumia pesa akiwa nchini kwake.

**Commissioner Lenaola:** Asante.

**Abdallah:** Kutumia kama million, hivi, tutafute njia katiba ifuatilishwe huko,

**Commissioner Lenaola:** Asante

**Abdallah:** Ata kama ni kwa Rais, waandamane na bwana Lumumba, waangalie kama nyumba watu wanaweza jengewa. Ona za Dandora zilijengwa ovyo ovyo hapa, watu wanalipa kodi za juu na labda wewe ama mimi mheshmiwa, tungelipenda tunjengewe self contained. Mtu nyumba yake bila kulipa makodi katika nchi yake. Nimazito.

**Commissioner Lenaola**: Asante sana, mambo yako imekwisha tumeshkuru.

**Abdallah:** Ya mwisho, ya mwisho tafadhali niruhusu,

**Commissioner Lenaola:** Basi la mwisho

**Abdallah:** La mwisho tu, sasa bwana mimi nikiwa mlelewa hapa westlands tangu 1958-60, kabla uhuru wenyewe, nimelelewa hapa. Tume ilikuwa imepanga watu wanaweza kuongea kidogo ama kuandika adhi hari (adhi hari yaani ni appeals) for constituencies. Sasa nimeandika nimeonelea vile nimekaa miaka miingi hapa, labda tungelikuwa na (tusema constituencies 7) unaona, Westlands pekee yake sasa. Nairobi yenyewe inakama constituencies tisa. Sisi tuwe na constituencies 7, waona.

Tatu, vile niliona uchumi gumu mtu kuipuka, kama tuseme, Eastleigh unaona kuna waislamu wengi lakini hayawezi kuivuka kama mbunge. Wakiristiano, yaani ni wengi tuseme. Sasa tujaribu katika hio saba , tatu wanaweza pewa waislamu na huku tumewacha nne kwa wakiristiano. Si unaona vile wako wengi. Na pia hii inaweza kusaidisha bila kuimpa mbunge mmoja kazi mingi yaani overburdening an MP. Yaani kama Mwenje sasa tusema anasimimia kubwa kabisa. Lakini ata 7 ni kubwa kubwa, vile tuseme, Dandora ukiwa na miili 7 , si ndio, Mihang'o na iwekwe na kama Kayole, na umoja, labda na Jomo Kenyata airport.

**Commissioner Lenaola:** Naona dakika zako zimeisha, nilikuongesha za mwisho

**Abdallah:** Naona, na pesa kuwa ikiwa itatolewa kwa wabunge, hapa na pale

**Commissioner Lenaola:** Ni sawa, malizia, tume (noises) jiandikishe pale na upeana barua yako pale ndio iwekwo kwa record. Asante. Eh cira peter, peter ciru, john lotich. Arafu kabula Ebu telewaneni, kabla lotich kuja, joo joo bwana lotich . Nasikia watu wanasema niliwafuta kwa list, Mimi nafuata list vile list inakuja. Kwa hivyo sitaki mambo ya rigging, kwamba ati unataka nikuite mbele na wewe ni mtu wa nyuma. Wale wameingia asubuhi mkaenda, nimewaita mara tatu – nimewaita mara gapi? Kama hauko na kupita naenda kwa mwingine. Tustrive uniambie ati niite bwana niite bwana. Usinikujie hapa mimi nafuata list vile imeenda. Na vile ulikuja nina kuita. Tuelewane? Tufuate list juu katiba ni kitu ambayo ni kisheria kubwa sana., hatuwezi hatuwezi cheza na katiba bwana. Lotich endelea.

**Rotich:** mimi nafikiri nimeshukuru sana leo, maanake sikuelewa katiba ni nini, lakini ameleta kidogo hapa, ametusomea mbili tatu, tukaelewa kidogo katiba in nini. Kile nilikuwa nataka kuuliza mimi, ni habari ya squartters. Squatters hii imetusubua mwaka mingi sana, nahii wakubwa wetu nafikiri squartters hawataki kumaliza kitu kinaitwa squartters, Hao ndio wanataka kusukuma mbele ndiowapate sahari ya pakukulia. Tukifuata tutoka muaka wa 1970, sisi tumekuwa squartters, tumekombolewa, squartters, tumekuja 1980s squartters, tumekuja 90s squartters. Haiishi kitu inaitwa squartters. Waswahili wa corner yetu, anasongesa hapo keso ndio apate kukulia. Kwa hivyo kwa maoni yangu hapo, ingeangaliwa hapo ikiingizwa kwa katiba hakuna kitu inaitwa katiba kwa wakubwa kuelendelea mbele nayo. Ingekua squartters hapo kumalizwa mtu amepewa hakuna tena kuitwa squartter. Hapo pahari yake iwe kabisa . Hakuna kuhamiswa tena, ati huko hutaenda mbele uende bari utatolewa huko, unapilekwa huko; Kitu ya pili, mimi ningesema, ni upande wa security.- Kitu inaitwa security, sisi wenyewe, ingawa tulifuja sheria, kuna - tunasema police, ( police kweli inatusaidia kidigo,) ata sisi tunasaindia. Yasemekana mwananchi ndio anabeba sheria, sisi tumefuja sheria maro mingi sana, kama police mwenyewe anakuja, sisi nafuja sheria , kulingana na vile yeye naye anakuja. Manake police akikuja, yeye mwenyewe anakuja kukusaidia yale yeye anakuja kutusaidia, nawe sasa hakuji kukusaidia, anakuja na jia zake zingine. Sisi naye tunapelekana naye kisheria. Hiyo dio mimi naona saa ingine mwizi ndio huyo, tunakamata tunaichoma, shauri tumeona tukipeleka ata police, kesho utaona iko hapa. Nafikiri ata hapa mingi sana tumetumia sheria tukichoma lakini tungetaka katiba asema. Ata police, ata laiya naye awekwe kwa katiba kusema ata hio sheria kidogo kawekewe nao nguvu laiya naye atumie hio sheria. Apewe kidogo, ndio laiya naye apate nafuu kidogo, maana ke sasa kama police anakuja akichukua yeye akipeana , naye police akipeleka pale, wanatoe kidogo, akawachana naye huko, sisi laiya, akikuja sisi naye tunakamata tunaifinya naye hapa, tunaimalizia naye. Kwa hivyo katiba naye ajue, sisi, zile katiba tutaunda zitasemekana ata laiya ndio huita police, sisi naye tuwekwe tuwe police, Hata laiya mwenye iko wapi, awe police. Police ile tumeandika awe macho na laiya awe macho ya police. Police akikosa, laiya ana right ya kwenda

kumuambia , bona umekosa: Naatibiwe saa hio hio. Na laiya hapo. Bona hukufanya hii kazi, kwa nini yeye anawacha hiyo kazi? Na laiya unaona wewe napigwa hapa, police ndiyo ile, kidogo na ile kijana alikupiga ndio huyo ametokea. Kwa nini wewe laiya, apana sasa sisi tutumie nguvu? Tufunje hio sheria sasa. Na sasa sisi tupewe hiyo sheria basi tuingizwe ata sisi laiya, tuwe askari ingine dani. Hio ndio tutapata nguvu zaidi, maana ke sisi wote tukiwa police, hatuoni mtu atakuja kusema ati mimi ni police, lakini tufuate kile kitapitishwa ni kisemekane kama mna ile maneno yenu mnfanyanga, Mkifanya baya, ushikwe na sheria na laiya, upelekwe police, police achukue hatua, upelekwe mbele uwekwe kwa court. Hio ndio itakuwa Rais. Na ile ngumu zaidi, angepewa chief. Ama wazee wa mtaa juu angetumika zaidi kuliko police. Samahani, nimekuja hapa zamani sana natumetumia miaka mingi sana hapa, tukitumia kama youth. Na hio ndiye ilikuwa sheria moja ilikuwa chama ni moja, tukafanya KANU youth, na tulifanya kazi mingi sana. Hatukuona wizi kama ya leo. Watu nabomolewa nyumba naingia dani, police ndio huo, iko na buduki ati sasa utamuambia nini. Si iko naye? Nafikiria ile sheria ingine tulisomewa hapa ya kusema maneno ya Rais, sijui katiba. Tulikuwa hatujaelewa kabisa maana yake ni nini lakini vile imesemekana kweli Prime minister iwekwe, mimi naona hio ni kitu moja mzuri. Prime minister akiwekwa dani ndio itakuwa kujibu maneno ile ingekua mbele huko. Na ile kitu ingine ningeongeongeza kidogo kwa hapo, maneno ya kusema ati wabunge, wapitishe sheria bila attorney General, ningeona, wote wangeingia pamoja na AG limiwe dani, ipitishwe iwe kitu moja wa pamoja lakini sio kupitishwa na bunge halafu iletewe Attorney General tena, ama itakua Attorney General liko dani ama itakua nje? Maanake hii sheria hatujasoma. Inakuanga dani, ama inakuanga nje? Hapo dio hatujajua.

**Crowd:** Bunge.

**Rotich:** Wanakuanga kwa bunge. Kwa hivyo hii sheria ipitishwe kwa bunge, hakuna aja ati kwa Rais dio apitishe, kwa hivyo ipitishwe kwa bunge. Asante sana. Nafikiri hio inatosha mimi.

**Commissioner Lenaola:** Asante Bwana Rotich, tumeshukuru, needa pale ukajiandikishe. Lukas Makokha, halafu Omolo Kennedy yuko? Kennedy Omolo, Omodi Amolo, utamfuata huyu Bwana Makokha. Majina halafu endelea.

**Makokha:** Asante sana macommissioners kwa kunipatia hii fusa, lakini kwanza ningependa kulalamika kidoga kwa sababu, (singependa kujitangaza lakini itanibidi kueleza hivyo). Mimi ni mwenyekiti wa haki na amani, catholic church hapa dandora, na tulikuwa tumeulizwa na Arch dioceses office tujiandikishe na tume ili tupatiwe hizo XXX za kufundisha wakiristo pande huu. Tumejaribu kujiandikisha, na tumefuatilia maneno kwa mda mrefu sana, paka sasa hatujaadikishwa. Kwa hivyo hiyo imeturudisha nyuma kidogo. Kwa hivyo hiyo dio lalamiko nilikuwa nalo.

Sasa kwa maoni yangu, yakwanza ningependa , kwenye katiba, tuwe na elimu ya bure. Hii elimu ya bure tukiwa nayo, iwe ni lazima kwa kila mtoto, na tukiwa na hii elimu ya lazima, kwa kila mtoto, nafikiri hawa machokola tuko nao huko mjini ambao wanatusubua subua kila wakati, hawawezi kuwako. Kwa sababu badala ya kwenda kule town wangekua wamelazimishwa kwenda shuleni. Kwa hivyo hii elimu ya lazima iwe kwenye katiba.

Na pia, ningependa kuongea kuhusu ardhi. Nilikuwa naonelea kwamba, ardhi yote ya Kenya, ingekua ni ya serikali, kwa sababu kuna wengine ambao wamenyakua ardhi kubwa zaidi, unakuta mtu mmoja yuko na acre million mojo, elfu moja, na unakuta mwingine hata pahari pa kujenga nyumba hana. Kwa hivyo nilikua naona , hii ardhi serikali ingechukua, iwe mikononi mwa serikali, na kama ni mimi Makokha, nitapatiwa mahari kujenga, nitajenga tu lakini hio sehemu iwe ni ya serikali, sio yangu.

Watu wengine wamechukua hio fusa kwa kunyakua kila mahari.

Halafu, ya tatu, nilikuwa na pedekeza , tuko na vyama vingi vya kisiasa, na hivi vyama vingi vya kisiasa, tumeona , nyingi zao ni kama za kiukabila. Sasa nilikuwa na pendekeza hivi vyama vya kisiasa, ziwe na, na National outlook, wawe na representative kila mahari, isipokuwa na representative kila mahari, hicho chama hakifai, hakitufai sisi. Kwa hivyo vyama vya kisiasa, zinatakikana ziwe na wabunge karibu kila mahari dio itabuliwe kweli ni chama kweli cha siasa. Na pia nikuwa kwenye sehemu hio hio ya siasa kidogo, nilikuwa nimeonelea kwamba, tumekuwa na mara nyingi watu wanahama vyama vya kisiasa, defections, hio nikuharibu pesa za uma, na nilikua naonelea , wale wabunge ambao wanachaguliwa na pengine chama cha NDP, halafu kukifika kabla bunge halijaisha, dio huyo amehama ameenda Ford Kenya, mtu kama huyo apigwe marufuku kabisa, na wakati mwingine asisimame tena kama mbunge.

Na, ya nne, pia tuko na wanakenya wengi, ambo hawana hata mahari pa kujenga nyumba, na tuko na sehemu kubwa zaidi, abazo tumeweka kado ati, ni national parks, tunafunga wanyama huko, sasa mimi nauliza, mnyama ni mhimu zaidi kuliko binadamu? Sasa nilikuwa naona , hawa ambao hawana ardhi, sehemu abazo wanaweza kuishi, pengine wanyama hao, hata tunaweza kuwachija ama tuwatoe tuwapeleke mahali pengine, ili binadamu apata pahali pa kuishi, hizo National Parks hazitusaidii kwa mara nyingi. ***Interruption***

**Commissioner:** Bwana Makokha, unajua saa hii tunafanya recording ya hii maneno, natukipiga makelele ya makofi, katika hile kichombo, napiga makofi tu, kwa hivo record ya Kinyago ni makovi tu, hakuna maneno. Tungependa maneno si makofi sana. Kwa kivyo tafadhali makelele kidogo tuweke chini na makofi tuweke chini pia. Edelea

**Makokha:** Nimeshukuru, Na pia, nilikuwa na pendekeza , bunge,iwe na mipango yake mwenyewe, yaani wajipangie ni wakati gani watafanya uchaguzi, wakati gani pengine yafaa waende kwa rxxxx, kitu kama hicho. Kwa sababu huwa mara nyingi tunasikia , sijui, the solution parliament, hiyo inakua ni kama siri ya mtu ambaye anaweza kudissove parliament wakati wowote. Inatakikana ijulikane bunge lenyewe limejipangia, ikifika 31st December, bunge litakuwa limeisha. Nainajuliana ata sisi tujue ata 3 years ama 5 years in advance, bunge litamalizika wakati huu, natunajua wakati huo tunaenda uchaguzi. Lisiwe ni siri ya mtu mmoja. Binafsi.

Na pia, nilikuwa na pendekeza , hawa viongozi wetu ambao wanachaguliwa kama pengine ministers, ama machairmen wa parastatals, kuwe na board nyingine itakuwa hio ni kazi yao, ya kuchagua hao watu. Tusimuachie Rais diye atakuwa akifanya hiyo kazi kila wakati, pengine anaweza kutuchagulia wale watu abao hawafai, lakini kwa vile yeye ni Rais, na vile abavyo nimesikia mmesema yeye ako above the law, akiwa above the law sasa mtafanya nini na amesha mchagua mtu? Ni mtu abaye hafai lakini sasa utanyamaza tu, unaumia, huyo mtu anakuumiza lakini hakuna kitu utafanya. Kwa hivyo Rais asiwe anachagua mawaziri, asiwe anachagua wenge viti wa hizi parastatals. Na pia kumalizia, macommissioners, ni mapedekezo yangu , hii katiba mkiiandika, muiandike kwa ile lugha abayo inaeleweka. Kwa sababu kama hii katiba tumeonyeshwa, mimi nimeisoma mara nyingi sana, lakini kuna sehemu nyinyi zimeandikwa na ile jia ambayo pengine lawyers ama advocates ndio wanaelewa

hizo sehemu, mtu kama mimi ata unipatie katiba nisome ata nisome mwaka moja mzima, nauniambie kwamba nikuelezee inasema nini, nitashidwa. Kwa hivyo naomba, katiba iandikwe kwa ile lugha, ambaye mtu yeyote anaweza kuelewa kwa urahisi. Nimeshukuru, Asante.

**Commissioner:** Asante bwana Makokha, hatuna maswali, isipokuwa ningependa kukuelezea , chama chenu cha haki na amani ya Catholic Church, ilipewa jukumu ya kufanya masomo ya kilaiya, nchini kote Kenya. Nimeshtuka kusikia nyinyi hapa Dandora hamkuenda offisini kubwa, mkapewa hili jukumu. Kwa maana tuliwapa barua, na wakafanya masomo katika kila nchi mzima. Na ni hapa pekee yake, tumesikia hamkupewa barua.

**Makokha:** Ndio, hataaa (Tries to anwer)

Commissionner: Sikutaka tuwe na dialogue, nakuelezea tu, lakini nimesikia maneno yako, nitapeleka mbele.

**Makokha:** Asante:

**Commissioner:** Jiadikishe pale, Amodi Omolo, David Chege yuko, David Chege, Edelea bwana omolo.

**Amodi Omolo**: Asante sana , mimi naitwa Amodi Omolo, I reside in Gitari Marigu hapa, since 1989, what I wanted to say, these officials have said, but mostly by Mwenje. Xxxx the constitution should be made accessible to all in a language that everybody can understand.

***Noises from the crowd (interruption)***

**Commissioner:** Tafahalini tuhesimiane, nilisema asubuhi ya , huu mkutano ni mkutano wa amani, na tungependa kila mtu ako nahaki ya kusungumza lugha anaipenda. Huu si mchana abao nyinyi mnapatiwa habari, habari si kwenyu, habari ni kwetu, na mtu akipenda kusungumza kivyake kwa kingereza, mkubari aseme hivyo. Kwa maana habari si kwenu sana, hatukupenda sana nyinyi msikie, hii ni habari tume ifanye nini? Kwa hivyo akisikia atasikika vizuri kwa kigereza, mpeni nafasi, akisikia ni kikikuyu, aseme hivo. Lakini habari itumwe kwa nani? Kwa tume, kwa lugha ambaye huu angependelea. Kwa hivyo tafadhali mpe nafasi. Yako ikifika sungumza, sungumza kijaluo ukipenda, lakini huyu asungumze kingereza kama ana? Anapenda. Tuheshmiane.

**Amodi Omolo:** Poleni, iko, watu wengine watasema mimi najilinga, na iko neno lingine siwezi kuongea kwa kiswahili.

**Crowd:** Noises … Ongea kwa kisungu,

**Amodi:** Sawa, mimi maoni yangu ni hivi, hii constitution review, what I wanted to say has been said mostly by Bwana Mwenje, sana sana concerning Office of the President. I'm not saying the President Moi but the office (moi akikufa the office will be there). We have seen that President has been given so much power, such that he can do anything, na unajua kama una boma, na huna watoto, na wako ni wezi, na wewe ni mwenye boma ukifanya makosa, wengine watafanya tu. So, we want that, the President akifanya makosa, should be in XXXXXX, xx should be packed. Should be given atleast meanimal powers. You find that when the President has committed an offence, na watu wake kama ministers, anajua ata akifanya makosa, anajua

hati mkubwa atakubali na yeye. Tuseme pointing the ministers, when a minister is currupt and the President is corrupt, we will have no power, to tell the minister that "umefanya Makosa". Again curruption, we find that corruption in Kenya is high and we know very well that we are number (I think we are No. 4 in the world). Tuko Number nne kwa ufisaji, sijui No. 2, tunajaribu, this has become because our leaders have been given much powers. Another thing, you find that some of these rich people, the acquire wealth in bad ways, like you find a minister has grabbed a plot, and he has been found that alifanya makosa, na akipelekwa kotini, the judiciary, the attoney general of the court, he will be left free. And I'm saying tha the judiciary should be xxxx, should have no influence with other executive powers like the registrator, the executive, and the rest. Sisi wadogo ata ukifanya makosa, na huna pesa, utafungwa tu kwa ajili hauna uwezo wa kifedha. Nafikili hapo umesikia vizuri.

Another thing which has been said – Education for all - Hio sitarudia.

Water – unajua maji ni uhai, na hii I will talk about it when I have reference from rural people. When you go to Western, you find that were some XXXXX which were dumped. I think the government revise this, so that at least we should hav water, free water.

The police - I think these people are not trained well, and I can see the commissioners, and some people here are learned. I think the police, if dealing with the public, ni mtu anatakiwa ajue kusoma akili ya mtu (psychology), at least you should have little knowledge. Ukipata mama anatoka kwa duka, na unaona amefunga shuka, na amebeba maziwa, unaweza je kuuliza mama unatoka wapi? You should read some people's pshychology, ata kama wewe ni mwizi, unaweza kufaa nguo, ufunge shuka, uende uimbe? Kama yule mzee alikua amesema maneno ingine hapa. Unaulizwa, mzee umetoka wapi? I think the policemen should be given more time, they should be trained enough. Hiyo ndio kosa tuko nayo kwa police.

Land issue - Hii ni shida zaidi, umepata watu wamesha ongea juu ya maneno ya shaba, kama juzi sisi watu wa Dandora, I think there was a problem across here. Kama ni serikali, at least they are out to protect the poor. Why did they allow some people to come up, waunde chama, to tell people they are giving land? And yet they know what they were doing. Up to now, some people lost money here about 700 shillings. Tuseme kama mama anauza chang'aa hapa, how long will it take a policeman to know? Kwa nini waliwacha watu, some people to take time, waende waunge, wasema we are giving poor people land? The government was reluctant. That thing should be allowed to take place. I'm blaming the government on that.

Another thing, I think there should be bit a code of conduct, ethics, you find some ministers or the government officials, I think there should be code of conduct ethics that controls them. Mtu yeyote si mzuri kuchaguliwa awekwe kwa offisi, not that because he has money. Hii dio inatuletea shida sana. Me most of the day I wanted to talk, Nimeshaongea na office of the President – Na hii constitution inatakiwa iandikwe kwa lugha kila mtu anaelewa, kama ni kijaluo, kikamba, kitaita, in a layman's language, kila mtu asikie. Asanteni sana.

**Commissioner:** Thank you very much bwana Omodi, kwa maoni yako you were very clear. – please register that you have given your views. David Chege Ng'ang'a, David Chege Ng'ang'a, Dikens Ouko, Dikens Ouko, Harrison Mraba uko? Utamfuata. Edelea bwana

**Dikens Ouko:** Asanteni sana, kwa kunipatia nafasi kidogo ya kusema maoni yangu kuhusu constitution review. Mimi kwa jina naitwa Dikens Ouko, natoka sehemu ya kasiburu Kabodo. Hapa Nairobi, nafanya na Lyold Masika Management. Niko na jambo kidogo tu, niko na jambo mbili. Jambo moja ni mambo ya security halafu ya pili ni economy.

Kwa upande wa security, tunaumia sana, na tulaumu serikali yetu kwa uhai ya watu vile tuko. Kila pahari kuna lalamishi tu ya security. People are not secured, tumeishi tukiogopa, tumeishi tukinyang'anywa kwa manyumba, hio dio wizi, natuko na serikali, ata saa hii tunaongea hapa, mimi najua tuko na serikali wametulinda hapa. Tunapigwa kwa njia, tuko na serikali,serikali hao wenyewe, mtu anatoka kazi saa moja, mtu kama mimi, ata karibu niharibiwe kazi, unaambiwa, (police wa Kinyago wanajua vizuri sana, intruding areas, ile areas ziko mbaya) ambaye wanaweza kwenda kulinda, kusaidia laiya, unakuta police anangoja watu wakitoka kwa matatu tu, anajua huyu ni mtu ametoka kazi, anamwambia mzee we enda kaa pale, na tena, hakuna ata kitabrisho ama nini, wanatumia lugha, ati ukitaka kutoka, unaweza ongea. Dakika kidogo lorry inakuja wewe unapelekwa Kinyago. Siku moja, ata mkubwa wa police alishangaa sana mimi kunikuta dani ya police cell, na nimelala, I was supposed to be on duty, infact ni bala (hiyo muandike sana) mtu ametoka kazi, wewe unashikwa, na wanajua vizuri pale watu wako na makosa wako, they don't want to be concerned about that one, wanataka pesa yao tu ya kwenda kula na bibi yao kwa nyumba. Hatuna police Kenya. Unanyang'anywa kila kitu kwa nyumba, unapigwa, unafanyiwa nini, na serikali iko. Ni serikali gani? Tuko na mainchi mingi saaana especially Uganda, umewaisikia vile wamekuja kutoka wakati wa Amini mpaka sasa Uganda imekua ni nchi, lakini sasa wewe, ati ata kwa matatu huwezi onekana na shilingi 500. Hiyo ni mbaya, serikali wajilekebishe na walinde laiya.

Jambo la pili, ni mambo ya economy – Economy pia, serikali ya Kenya inajua ni idadi ya watu gani wako nayo kwa Kenya, na hao watu serikali wanajua vizuri sana hawa watu wanaweza kula namna gani, na kwa nini shida ziko sehemu zingine na serikali iko? Unakuta cucu, cucu iko nyumbani ama Nairobi, na ananunua sukali kama vile Moi ananunua sukali imagine ndiyo hiyo cucu ana nunua sukali. Cucu atapata pesa wapi? Ya kununua sukari, na kwa hiyo bei. Kwa hivyo serikali waangalie masirahi ya binadaamu. Kama vile imesemekana hapa sasa, street children, infact, hawakukuwa mbeleni, saa hii wako, wametoka wapi? Serikali wanaona ama hawaoni? Wanaweza saidia ama hawawezi saidia? Lazima wajue hao machokola ama street children, hao ni watu wa Kenya na lazima wasaidiwe, wasidiwe kwa kila aina ya usaidizi, ata kama ni chakula, infact wanahaibisha ata watu hapa town. Unakuta chokola anakukibisha ata na mavi, kwa sababu umemkatasa pesa, whats that? Policemen are there, hata hawataki kuangalia. Kwa hivyo mimi ni hayo machache nilikua nayo kuongea kwa wakati huu. Asanteni.

**Commissioner**: Asante sana bwana Omodi, thank you very much please register,- Kuna swali, kuna swali,

**Commissioner Salome:** Asante sana bwana Dikens Ouko kwa maoni yako. Mimi niko na swali moja la ufafanusi, ningetaka utupe mapendekezo yako juu ya vile tunaweza kutumia kuhakikisha tumesaidia watoto wenye wako kwenye mtaa. Wewe unaona wangesaidika je, ama jukumu ya serikali ni gani na jukumu ya wananchi wenyewe kwani watoto wanatoka kwetu sisi, tuna jukumu gani yenye tungeweka kwenye katiba?

**Omondi:** Lile ningetaka kujibu hapo kwa hawa watoto kusaidiwa, ni jambo la kwanza, kuna shule ya masikini, hao watoto, wangefunguliwa shule fulani, waambiwe lazima uende shule, na hiyo shule iwe na kila aina ya kusaidia huyo mtoto, na sheria iwekwe huyu mtoto akipatikana, anashikwa anapelekwa shule, hiyo ndiye jela yake! Akipelekwa shule anasomeshwa, ata na kiboko, ata na nini. Na huyo mtoto akitoka hapo tena apelekwe ata kama ni course, ata kama ni wapi apate kusaidika. Akitoka hapo si anaenda kwa kazi yake? Si atakua mtu mzuri? Na tusipofanya hivyo, hawa watoto ndio wanatunyang'anya hapa jiani, kwa sababu sisi tumewanyima funza yao yakuendelea kama wananchi.

**Commissioner:** Asante sana bwana Ouko. Mulamba, Teresia Kinyua yuko? Teresia utamfuata bwana Mulamba, halafu baada ya Teresia tumuite chief Mutunga atoe maoni yake. Edelea, jina na maoni yako.

**Harrison Mulamba:** Jina langu ni Harrison Mulamba, ningetaka kutoa maoni kuhusu uchunguzi, kuna hizi proffesion international inaruhusu kila mwananchi wa nchi yeyote ulimwenguni awe na transport licence, wanaziita mobility rights. Ningepedelea hii katiba mpya iweke hili jambo manani. La pili, ningependa juu ya natural resources, tuseme kama ni maji, msitu, mxx, wakati wa sehemu, popote pale watoka po waweze kuwa na share kidogo kuhusu ile resources kwa sababu utapata vile mambo ya livyo sasa, wengine wananyanyasa. Sina mengi sana, ni haya mawili, maelezo kamili yatapatikana kwa barua. Asante,

**Commissioner:** Asante Mulamba, peana memorandum yako, asante kwa kuchukua mda mfupi, mama Kinyua, halafu baadaye bwana mutunga

**Tape 3**

**Teresia Kinyua:** Asante, Kwa majina naitwa Teresia Kinyua na nimekuja kutoa maoni. Mwanzo ningependa, kuongea juu ya wamama, wamama wengi huwa wamepata pesa kidogo, wakati ameenda kufanya kibarua, anafikiria badala ya kuenda kibarua, aende aweke boga pale, akiweka mboga pale, kuna watu wengine huwa wanakuja wanamdhalau, akitaka kuchukua zile boga, atachukua nahawezi lipa hata dululu, sababu hana mahari anaweza enda. Akikimbia kama ni kinyago ama marahi pengine, si ni hapa tu, hapo ni nyumbani, anachukuliwa hatuwa na anarudi muda wa dakika tu kama tano unamuona hapa amerudi.

Ingine ningetaka kupendekeza hivi, hapa kuna watu wengi sana wameajili watoto wasichana, na ukienda kwake, inaonekana ni kama ni adui, ni kama umekuja kumnyang'anya kitu ya faida sana kwake, kwa sababu umemchukulia mtu ambaye anamfanyia kazi, ukienda kureport, hiyo inachukuliwa kwa sababu alitoka hapa akaenda nyumbani, akachukua mtoto wa watu, akakuja

kuajili hapa, tunaambiwa, si walisikizana nyumbani na wazazi, haya, wacha afanye kazi na kama si hivyo arudishwe nyumbani, lakini mimi ningependekeza hivi, mtoto kama huyu akipatikana, achukuliwe apelekwe shule kwa sababu mahali alitoka, hakuelemishwa, sababu kama angeelemishwa, hangekuja hapa kufanya kazi kama hiyo, angekuja aajiliwe kazi ambaye inaweza kumsaidia, sababu watu wengi ambao wanaajilia hawa watoto wasichana, anakaa naye nahamlipi hata dururu, na huyu mtoto asiongee. Mimi ningependekeza hivi, kukipatikana mtu ambaye ameajili mtoto kama hajafikisha miaka 18, anachukuliwa hatua.

Kitu ingine ningetaka kusema, sisi wamama huwa tumembaki nyuma sana, na hata, saa hizi mimi ningependekeza hivi, wakati wa uchaguzi sababu unakuja, tujaribu kusimamisha wamama, sababu wamama wako na shida sana, na hao ndio wanajua wenzao wale wako na shida. Tujaribu kusimamisha mama mmoja, ama wawili, yaani wamama wawe wengi kushinda watu wengine tunaenda, kuwa wale wamechaguliwa na ni mwanaume, ukienda kwake, anakwambia mambo abaye, hujawai sikia na masikio yako tangu uzaliwe. Anakwambia mambo machafu, mambo ambayo haitakusaidia kwako nyumbani, kama ulikuwa unataka usaidiwe na masomo ya watoto, anakwambia kwanza, utatimisha vile mimi nimesema. Kwa hivyo mimi ningeomba, kama kukipatikana mtu kama huyo, afukuzwe kama ni bunge, ama afukuzwe mahara amechaguliwa, tuchague mwingine immediately.

Ingine ningeomba hivi, sisi wazazi, huwa tumezaa watoto wasichana, na vijana, vijana wengi mnaona huku mitaani, ni kwa sababu masomo imekua ngumu, ukipeleka mtoto wako shule, mtoto yeyote yule ameanda shule, zile pesa unaitishwa kwa shule, ni pesa ambazo hautaweza kutoa, sababu mahali unaenda kuuza sukuma, hujaruhusiwa uuze sukuma hapo. Ikifika jioni, unaenda kabla pesa haijapatikana, mahari unaenda tena, kama ni town, dio huyo unafukuzwa, ukienda kila mahari hakuna mahari unaweza simama hivo utafutie watotot wako. Unajiuliza, kwani mimi sio Mkenya? Wengine wale wamama wako na shida kama hizo, ni wengi sana, na hao dio majority ya Kenya watu wale wako na shida ya kusomesha watoto wao. Kwa shule kama ni secondary, zamani, ulikuwa unaona watoto wengi walikuwa wanaenda shule kwa sababu serikali wakati huo ilikuwa inaangalia, lakini wakati huu, hatujui kama ni serikali imeisha ama kumeenda namna gani? Sababu unakuta, secondary ambayo imekukalibia sana, huna zile pesa zinaitishwa, na ukienda kupeleka malalamishi yako, unaambiwa, enda mahari unataka, na hakuna mahari utaenda, utaenda wapi? Kila mahari ukienda, unaambiwa leta hii, ukienda kila mahari, unaambiwa lete hii. Mimi nitaachia hapo, na nitasema asante.

**Commissioner:** Asante Teresia Kinyua, jiadikishe hapo, asante kwa maoni yako. Japheth William Mumi, sorry, chief, samahani, chief alikua next. Utamfuata chief. Edelea chief. Majina halafu utoe maoni yako.

**Chief:** Mimi naitwa Mutung'u, chief wa Dandora. Macommissioners, na wale maofficers mmekuja nao, na wananchi kwa jumla, hamjambo. Watu wengi wanafikiri, labda hana shida ama haoni vile angetaka mambo ya poleshwe. Mimi mwenyewe niliachwa na wazazi wangu nikuwa mtoto mdogo sana. Nilikuwa na umri wa miaka 13, lakini, mimi niliweza kujilipia karo ya shule, kwa sababu wakati yule, secondary school, tulikuwa tunalipa shilingi 200 (tuition) lakini siku hizi, mtoto kama huna shilingi

elfu hamsini, hawezi kuingia form one. Na vile kulivyo, watu wengi sana hapa Kenya kupata hio shilingi elfu hamsini, ni gumu sana, na una watoto wawili, watoto watatu, Hawa watoto, hawatasoma, na labda hawa ni watoto welefu, ambao, wanaweza baadaye kusidia nchi hii. Kwa hivyo, vile ambavyo ningependekeza, ni kwamba, elimu, iwe hakuna mtu hatapata elimu kwa sababu hana karo, education should be affordable to everybody, na isiwe ni primary school peke yake, iwe hata secondary, na university yule mtu ambaye ataweza. Halafu, tuna shinda ingine, kama hapa Nairobi, kama unataka kugawanya ardhi, labda unagawanyia watoto wako, ama watu wamenunua shamba wanataka tugawanya, ili kila mtu awe na kipande chake, ukienda city hall ndio upate clearance certificate, unaweza kuchukua hata miaka mitano, lakini, ukienda kama hapa Kiambu, ama Machakos, ama Kajiando, you can do it within a day. Zile sheria ambazo ziko kwa Nairobi City Council, are a cake (retrogressive), hakuna maendeleo itafanyika. Kwa hivyo, tungependekeza, tuwe na sheria ambayo, (kama ni huo ugawanyaji wa ardhi), vile inavyo fanyika, Kiambu, Kajiando, Machakos, and other districts, ifanyike ata hapa Nairobi, kwa sababu hata sisi, tunataka kufanya maendeleo, na bila hiyo, itakuwa gumu sana. Halafu, kuna shinda ya maji, na mali zingine, unaona ya kwamba, utaona kama hapa Dandora sasa, ni sehemu nyingi ambazo hazina maji, lakini utapata kuna watu ambao wamekata hiyo mifereji, wanaosha magari, ukienda outering, maji inatililika tu, kuna kuwa na mto, na mfereji, ya city council. Ni kwa nini tunaachilia mali yetu inaharibiwa, kisha, hayo maji, sisi ndio tutalipia tu, si ni kweli, kwa hivyo tungetaka equitable distribution of our natural resources ndio watu wasitumie hio mali bure, hari wengine wanawalipia.

Tukiangalia mambo ya child labour, kama alivyosema mama, tuko na shida kubwa, ya child labour, lakini kama mimi, vile nilivyofanya, kama sikufanya hiyo child labour, singesoma, what are we going to do about it? Basi, turahisishe mambo kwa masikini, na watoto wa masikini ili wasiende kuhangaika kutafuta kazi ndio waweze kula. Kuna jambo lingine, kuna watu ambao, wanajitafutia, lakini, itafika wakati,huyu mtu hawezi kutafuta tena. Pahari kama Africa kusini, mtu akifikisha miaka sitini na tano, hata kama alikuwa ameajiliwa, hata kama hakuwa ameajiliwa, anapata pension, inawezekana hapa? Kwa hivyo, hata mimi ningependekeza, tufanye namna hiyo kwa sababu, watu wengi hapa, hata mtu wa miaka sabini, themanini, bado anakondesha nyumba, hana mapato, huyu nyanya ama babu, tutamuache afe kwa sababu hana mapato? Lakini kama tungekua na pension, tusema kama shilingi elfu tano, hivi, huyo nyanya, ataweza kujilipia nyumba, ataweza kula, na maisha yatakuwa ni sawasawa, halafu, kila siku tunaona kwa gazeti hata kwa TV, fulani, ako na shinda ya kiaafya, tumchangie, fulani, ako na shinda ingine, tumchangie, na kama ingewezekana, kila mtu angepata huduma ya afya, na apate bila malipo, kwa sababu, watu wengine, wanakufa tu ovyo ovyo, kwa sababu akienda hospitali, ile galama amboyo inatakiwa, haiwezi, na huyu mtu, labda ni mtu anaweza kusaindia nchi. Kwa nini tusimpe hiyo huduma, ndio tupate kuendelea?

Ninatangazo moja tu ningetaka kusema - Kesho registrar of persons (wakupatiana kitaburisho) atakua kwa office yangu, kwa hivyo wale ambao wamepotesha vitaburisho, na wale ambao wamefikisha umri wa miaka 18 basi watakuja pale, wachukue vitabrisho. Halafu kwa kitabrisho, utaona, mtoto ni lazima awe na kitabrisho ya mzazi, na pia, awe na birth certificate, ama school leaving certificate. Hapa kwetu Dandora, utaingia hapa, dumping site, kuna watoto huko, hajui mama, hajui baba, hakuingia shule, hata clinic hakuenda, kwa hivyo, hana hati yeyote ile, na kuna watu ambo wanamjua, kwa hivyo, pia ningependekeza, hata ingawa, hatungetaka tuwe tunapatia kila mtu kitabrisho, turahisishe, hivi , mtoto akiwa ni atima, asionekane kama anazurimiwa ati kwa sababu hana hati, lakini tutafute njia ya kuhakikisha yeye ni mkenya, ndio apate

kitabrisho ajishikie basi yeye ni kama wengine.  Ni asante sana, nashukuru.

**Commissioner:**  Asante bwana chief, goja kuna swali, shika tu microphone.

**Commissioner Salome:**  Asante sana bwana chief na tunashukuru sana kutukaribisha kwenye kikao chako, mimi nina swali moja tu kwa hio pendekezo lenye umefanya la mwisho, ungetueleza pendekezo hilo kwa kinaganaga kuwa tungefanya je, umesema watoto hawana maadishi, ama hawana documentation, ingefaa wapatiwe kipande?  Sijui kama ni jambo lenye umefikiria vile tungeweza kuliwasilisha, ama ni jambo ungetaka kwenda kufikiria halafu ukatuandikia, ama vipi?

**Chief:**  Vile abavyo ningependekeza, tuna veting committees, na hizo veting committees, sana sana tunafanya veting kwa wale watu, ambao wametoka katika boarder districts, lakini, wale hawana cheti chochote cha kuonyesha ni wakenya ama walizaliwa lini, tungechagua wazee, hapa nyumbani, watu amboa wana heshima yao, tuchague wazee, akina mama, na vile vile vijana, ndio waweze kukaa, na kudhibitisha ya  huyo mtoto, ni wa kwao, wanamjua, wanajua familia yake, wanajua route, na labda vile hawatakuwa na haja, ya kupendelea, mimi naona hiyo ingekuwa sawasawa kabisa.

Commissioner:  Asante bwana Mutung'u kwa maoni yako, jiadikishe pale, Japheth endelea, halafu, Robert Mwangi, endelea bwana

**Japheth Mumia:**  Hallo, Asanteni sana, I'm not going to seat down because I was born to stand lakini – As my wishes, ya.  I'm talking communication

**Commisisoner:**  Sema majina yako.

**Japheth Mumia**: Japheth Mumia Osuli -  I'm talking communication,  I very much appreciate if you enhance the freedom of people here. You came here to look for the minds of our XXXX which is very good. Don't overlook as if wasting time just now, we are using XXXX what to do, but this is what is unique in the area, not only Dandora, let it be in Nairobi worldwide, I'm sorry, I just wish that what you can do, look for the poor people now, they are here, nobody have even a single cents in his pocket.  He is going back, he came to his duty, to know that XXX you cannot work when they are not here.  Can you help these young, these widows? Help widows, halafu the transport, transportation vile ilisemwa, huyu mwanamke natoka hapa naenda pande gani, anakuja kusimama hapa, anaona we, mama you are looking so smart, like you are looking now, you are so smart, (interruption) what I want to say is only one thing, its only that we see the way to communicate, progress, and how we can go on and on and get these people.   Ya ya.

**Commissioner:**  Asante sana, jiadikishe pale, asante kwa maoni yako.  Nicodemus Otieno, Japheth, needa pale bwana ukajiadikishe. Nicodemus Otieno, Charles Atula, Charles Atula, Destation Diga, Destation Diga, Iran Ngaira, Iran Ngaira Karibu.

Iran Ngaira:  Asante sana tume, nawasalimia wote wanachi wa Kenya wenzangu, Hamjamboni? Mimi nataka kutoa maoni,  Jina langu ni Iron Ngaira Shipendi.  Mwanzo nataka kusungumzia kuhusu constitutions.  Hii constitution, wananchi wa Kenya, tumenyanyashwa, ama tumekosa kujua ni kitu gani tunatakiwa tufanya, kwa sababu hatujajua sheria inasema nini.  Kuna shida,

ama kuna shinda imetokea mahari, lakini hujui, ni sheria gani, utasimama nayo, ikusaidie. Kwa hivyo maoni yangu ni kwamba, kama hii constitution ama katiba, waanze kuifunza kuanzia mashule, watoto waelewe constitutions wanapokuwa, kwa sababu, watu wengi tumekuja kujua constitution ni nini wakati review imeanza. Hata ukiuliza mtu, umulize katiba ni nini, mzee ambaye, ni mzee, haelewi, kwa hivyo ni mapendekezo ama anapendekeza ya , hii sheria, ingelikuwa vizuri, ipelekwe kwa mashule, ianze kufundishwa kutoka mashinani ya shule.

Jambo la pili, ningetaka kusema nchi yetu ya Kenya, ni nchi ambaye kufika saa hii hatuwezi tukalia economy ni mbaya, ama tuko na taabu ya economy, lakini shinda imetokea ni , ile lasimali tuko nayo, haijatumika vizuri, kwa jia hii, kuna kitu inaitwa taxation, ama tax, unapata mwananchi ambaye hajiwezi, mwananchi ambaye ni masikini, labda amepata nafasi kidogo, ya kuweka kitu kama kioski, huyu ndio anatoshwa usuhuru, lakini mwananchi ambaye ana uwezo, tuseme tajiri, wacheni tuseme hivyo, huyu ana kitu inaitwa tax free, sasa unapata ya , ile tax ambayo tunapata Kenya, inatoka kwa wale watu masikini, ambaye hawana kitu, na wale watu wamejiwezesha, ambao ndio wanatakikana tutoe mali kutoka kwao, wana kitu inaitwa tax free ambayo imeturudisha katika hiyo hali. Kitu ingine ambayo imeletea hiyo hali katika Kenya, ukiingia katika companies ambazo zinatakikana ziwe zinatoshwa usuhuru, unapata company zingine hazitoshwi usuhuru kwa sababu hii company ni ya furani wa furani, amejulikana katika high office, na ukipata mzuri, huyu ndiye mtu mzuri, ambaye angetoa tax mzuri isaidie uchumi ya nchi yetu ya Kenya. Anapoimport vitu kutoka nje, yeye, vitu zake zinafanyiwa tax free, kwa sababu yeye, ni mkubwa, na huyu mdogo, amenyanyaswa katika njia ya kuwa yeye ndiye anatoa tax. Nikisungumzia hapa mahari tena, unapata ya kuna companies katika nchi yetu Kenya ambao zinakuwa runned na foreigners, unapata tax ambayo, inatoshwa a foreigner, kulingana na sheria ya Kenya, iko tofauti, iko juu kidogo, na indegeneous, hiyo iko chini, hiyo ni sawasawa, lakini tumepotesa uchumi ya nchi hii, kuna ujaja, ambao umekuja, unasikia kampuni fulani, imeuziwa mtu fulani, mwanakenya, lakini ni ukora, ionekane ni indegeneous, lakini mwenye anarun hiyo company is a foreigner, abapo sasa inchi inapotesa usuhuru katika njia kama hiyo. Kwa hivyo mapendekezo yangu ni hii, kama constitution inaweza kuweka machinery mzuri yakuangalia mambo jinzi company za Kenya zinakuwa run na tunavyoendeshwa ili tukapate kupata tax ambayo inasaidia sisi katika nchi ya Kenya.

Nikitoka hapo, nataka kusungumzia kuhusu, mambo ya macommissioners, - commissioners wa Kenya, ambao wanashikilia kitu fulani fulani, unasikia commissioner fulani, commissioner utume fulani, wote ukiangalia (mimi nasikia wanakuanga presidence appintee) Mimi ningependekeza hivi, ni vizuri, wawe appointed na President, lakini subject to approval by the parliament. Kwa sababu parliament ikiapprove, mimi nitajua, nina mwakilishi pale, ambaye ameakilisha, amekubaliana ya huyu commissioner, ametoshana, ama ametosha kuwa commissioner katika ile office ambayo amechaguliwa kwa sababu unapata, mtu akiwa ni President appointee, na anataji tu President appointee, akifanya makosa, hakuna mwananchi ako na swali juu yake, ama, yeye mwenyewe kwa hiyo kazi anafanya, hana freedom ya kuifanya hiyo kazi kwa sababu hataki kwenda kinyume cha matako ya yule alimchagua. Kwa hivyo President appointee, lakini subject, to approval with the parliament, naona itakuwa mzuri.

Jambo lingine, nataka kuongea kuhusu constitution yetu ya Kenya – kuhusu amendment, ama kuamend, naona hii sheria yetu ya Kenya ama katiba yetu ya Kenya, ninapoitazama haina security, kwa nini nasema haina security? Tangu ilipowekwa,

imebadilishwa mara mingi sana, na unapata wakati inabadirishwa, mtu anaibadilisha, in his own interest, katika mambo ambayo itamfurahisha yeye. Kwa hivyo, mimi ningependekeza hivi, ya kama sheria vile tunavyo (vile tunakaa hivi, tunatoa maoni ya kubadilisha sheria, si niukweli:?) kwa hivyo, sheria kama itabadilishwa, irudishwe tena kwa wananchi, (tuwe na refurrundum) wananchi totoe maoni, tunataka hii sheria ibadilishwe kwa njia gani? Isiwe ya ni mtu fulani, anasimama tu na anasema " hii sheria imebadilishwa, Rais amesema hii sheria ibadilishwe, nainabadilishwa bila sisi wananchi kujua ya inabadilishwa namna gani. Inakuja inaumiza sisi wananchi, na tunahitaji hio sheria ilinde sisi wananchi. Kwa hivyo, hayo ndio maoni yangu, nimesema asante.

**Commissioner:** Asante bwana Gaira, umechukua muda wako kabisa, na umemaliza asante. Hakuna swali ulikuwa very clear, jiadikishe pale. David Irungu, David Irungu, Ibrahim Ahmed Ibrahim Ahmed, Charles Atula, Charles Atula, utamfuata Ibrahim, joo joo ibrahim, halafu Atula.

**Ibrahim:** Hamjamboni nyote ambao mmehudhulia? Wakubwa kwa wadogo, ni zote tuko hapa kutoa malalamiko yetu kwa pamoja, ili, yarahisishwe katika mpangilio wa katiba. Jambo la kwanza ni, katika jamiii yangu ya kiislamu ambayo inatimsha asili mia takribani kama arobaini hivi, au hamsini katika jamii ya wakenya. Kwanza nitaingilia upande wa mahakama ambayo tunayakilishwa na kadhi mkuu wetu. Tukiangalia, saa hizi tunavyosungumza, kadhi wetu, anatakiwa awe ameretire, (awe amejihusuru) lakini kutokamana na matatizo ambayo , yako dani yake, ndio imekuwa hawezi ku-retire, kwa sababu wa kumridhi ama wa kuchukua mahari pake, kwa sasa hapatikani, na mpangilio wa kumteua, imekuwa ni shinda. Hivyo, tungeomba , kadhi wetu awe atachaguliwa na kikundi cha wasomi wa dini ya kiislamu, sisi tunawaita "jumuia tula hulamaa" . Pia, kuna matatizo mengine inapatikana katika office hiyo hiyo ya kadhi, mfano, kuna masilahi ya waislamu talaka na ndoa, ndio nauridhi, mara mingi ndio imekua kazi ya kiasuruhisha, halafu mfano wa kasuruhisha case, kisa watu wakawa hawakuridhika na case hio, huwa wanakwenda, katika mahakama ya rufaa. Wanapofanya hivyo, mara nyingi utakuta inagongana kwa sababu, katibe mahakama ya rufaa, yule ambaye atakuwa anaamua hio case sasa, atakuwa sio muislam, na akiwa hivyo hawezi kujua yale matatizo ambayo yanaikunga jamii hiyo, hapo moja kwa moja inatakiwa ni matatizo. Kwa hivyo tungeomba, kuwe na mahakama ya rufaa, na yule atakuwa katika hio panel ya hio majudge awe pia ni muislam.

Pia tukija katika uhuru wa kuabudu, kuna sherehe zetu ambazo ni za kiislamu, tumepewa moja pekee yake, nayo ni ile inaitwa Idir Fitr, nayo hiyo ukiangalia, imekuja kwa Presidential decree, ni kw amri ya Rais kwa mfano, tukieleza namna hio, hii, mfano wazee wetu wanatuambia mwaka wa 1975, walikwenda kwa hayati Mzee Jomo Kenyatta wakamuomba ndio akawapatia. Naye Rais wetu alipoingia, huyu mwingine Moi, pia naye, akaiendelesha. Je akija mwingine anaweza sema siitaki, na itaondolewa. Kwa hivyo pia nayo iwe dani ya katiba.

Jambo lingine, ni wanawake wetu wa Kiislamu huwa waruhusiwa kujifunika, kwa jina lingine tunasema "hiyabu" . Hii imeleta matatizo makubwa sana katika nchi yetu, mmoja wapo ni kule baathi ya watoto wa kiislamu wanafunzi kufukuzwa katika mashuleni mwao, na wale ambao wanafanya kazi kutoruhusiw kufaa hivyo. Hii inakweda kinyume na mafunzo ya dini yetu, na

tungeomba hii iwe dani yake , wanawake waruhusiwe kujifunika vile inavyotakikana, kuhusiana na mwenendo mlua wa dini yetu.

Nikitoka hapo, nitakwenda katika maswala ambayo inatukuba zote, kuwa pamoja, mfano serikali za mtaa, mimi nasugumza hivi kwa sababu nimefanya mkazi wa hapa siku mingi, natumekuwa tukiona matatizo ambayo yanatupata. Tukiangalia wakazi wote wa Dandora tutakubaliana, mwaka wa 1992, tulikuwa na councilor ambaye alikuwe ko, mpaka wa sasa wengine hata hawaambiwi councilor mwenyewe, na huyu alioko sasa wengi wetu pia hatumjui. Hii nikutokamana na matatizo ambayo , katika kipengele cha katiba imekua ni vingumu kumjua councilor wako kutokamana na kazi au shughuli ambazo anatakiwa kuzifanya. Mfano ata mbunge wetu hapa, wengi wetu tunamjua wakati kuna shinda, wakati kuna matatizo, mfano kama yale yaliotokea nduta mbunge wetu ndiye mbunge wetu anafanya nini? Anatokea. Lakini bila kuwa na matatizo humoni, hivyo tungependekeza hawa mamayor, na vile tunavyomchagua councilor wetu, iwe moja kwa moja, na mda wa miaka miwili, mimi naona hio ni kipindi ambacho kinafaa, Na kwa mda huo, ikiwa mfano councilor wetu hapa, hatuoni anafanya kazi namna inavyo takikana, basi kuwe na mpangilio wa kumrudisha nyumbani. Mpangilio huo pia utumike pia kwa mbunge, ikiwa mbunge wetu anaonekana pia hafanyi kazi yake namna inavyotakikana, pia neye arudishwe nyumbani, na kiwango cha elimu cha councilor iwe ni atleast iwe in form 4 na kuwe na mashariti maalum ya kumchagua councilor, na mbunge pia, mfano, tabia zake zijulikane, na maadili yake yajulikane, isiwe tu ni kumchagua councilor yeyote ambaye atatujia anatuabia anataka kuchaguliwa, basi ajitokeshe tuwe twampigia kula, apana, ingaliwe tabia zake kutoka nyuma huko, alikuwa ni mtu wa aina gani? Na mbunge pia, aangaliwe vile alikuwa, ni mtu aina gani, kwa sababu mfano kama hapa Dandora, sisi tumepata matatizo mengi kutokamana na kumchagua councilor ambaye tabia zake hatumjui, leo tumeumia sana, mfano tukiangalia, ni mashamba magapi hapa imegawanywa? Ni mengi sana, na wengine ata wamepotesha maisha yao, lakini utakuta councilor, yeye huangalia wale ambao wako karibu na yeye. Mfano, macouncillor wetu, tumekua tukiwaona, wanaoperate katika mabar au sio? Katika vilabu, kuna wetu wengi sisi hatuingii katika vilabu, au namna gani? Sasa inakuwa ni vigumu, unaona, inakubidii yaani ukiuke maadili fulani, ili ndio uweze kumfikia na wewe upate mambo kama hayo, na masirahi mengi ambayo sisi wakaazi wa hapa wanatukuba, hatuwezi kuyatatua kwa sababu ya nini? Councillor huwa hatumuoni, wala huwa, wengi wetu hata hatumjui, na ikiwa tunamjua pia anatupuuza, kwa hivyo, hiyo pia iwekwe councilor tumrejeshe nyumbani, kwa kipindi cha mda kwa mfano miaka miwili hivi, tuone kama hakuna kitu atakuwa ametufanyia, basi tuwe tutamrudisha nyumbani. Tukiingia kwa upande wa vyama, tuwe na idadi ya vyama, tusiwe na idadi ya vyama 46 kama sasa tulivyo navyo. Tuwe na idadi kwa mfano, 3 ama 4, tukiwa na vyama mfano nne peke yake, ama vitatu, vitajihusisha na maendeleo ya wananchi au wanachama wake kwa ujumla, lakini kwa sasa, kila mtu akiwa ataruhusiwa awe na chama chake, basi moja kwa moja itakuwa ni vurugo mbayo kwa mfano tunaiona kwa hivi sasa, kwa hivyo vyama mimi naomba viwe vitatu, na vikiwa vitaongezwa, viwe ni vinne peke yake, iwe jitajihusisha na masirahi ya wananchi. Nikimalizia, kuna mambo ya mali ya asili, (natural resources) kwa mfano, kama miti, maji, na mambo kama hayo, mfano ukiangalia

Dandora yetu hii, utakuta hamna miti ya kutosha, na mi nakubuka, mwaka kama wa 1985, nakubuka nikiwa mdogo, niliwahi kuona miti ikipadwa na serikali ya mitaa (city council) kwote huku, lakini baadaye, nyingi katika hizo zikawa zenye kutolewa, na zilitolewa kwa njia ya ufisaji kwa sababu zile nafasi zilizokuwa hizo ziwepo, zikawa zinajengwa (yaani zile open spaces). Kwa

hivyo iwe ni katika katiba , mfano watu wamezunguka sehemu moja kama nyumba kumi hivi, wawe ni lazima kuwe na mtu katikati yao. Kama sehemu zingine za nchi zingine, hiyo ni katika sheria, lazima kuwe na mtu, ukiangalia huku kwetu hakuna, ni miti michache sana, na hiyo in katika kulinda mali ya ardhi. Na pia maji, iwepo, kwa watu wote kwa ujumla, isiwe tu ni kwa watu maalum, na kuwekwe sheria kuwe na mpangilio maalum wa maji, , kuna sehemu maji yanatiririka ovyo ovyo, ata hapa Dandora, kuna sehemu zingine hazina maji, na zingine zina maji. Na zile sehemu ambazo hamna maji, yanazuiwa na zile sehemu ambazo , maji yanakatwa, ama kama vile chief alivyzungumza mbeleni, yanaharibiwa, kwa hivyo iwe kutakuwa na mpangilio maalum katika katiba ni sheria, ikipatikana mtu kama huyo atachukuliwa hatua kali. Kwa sasa sina mengi, isipokuwa ni hayo, asante.

**Commissioner**: Asante sana, umechukua dakika zako kumu, tumeshkuru, goja kuna swali, Ibrahim

**Commissioner Salome**: Asante sana, Ebrahim Ahmed, swali langu ni moja, ya kuhusu udiwani, na ile miaka miwili yenye ulisema, sikuelewa unataka kuwa unataka wawe wakichaguliwa kila miaka miwili, ama ulikuwa unataka baada ya miaka miwili achungunguzwe akiwa hafai dio arudishwe, ama atolewe? Na pia kama ni kuhusu utoaji, tungetumia utaratibu gani kutoa?

**Ibrahim:** Kuhusiana na mayor, ni kianza, iendelee hii ya kuchaguliwa kwa miaka miwili, moja kwa moja, na kwa madiwani, macouncillor, iwe kwa miaka miwili ndio tumuangalie, apewe muda wa miaka miwili aangaliwe, Je, amefanya kazi yake namna inavyotakikana? Akiwa hakufanya atolewe. Na utalatibu utakayofuatwa, warudiwe wale watu ambao walimchagua huyo diwani, waulizwe, hio ni kama referundum, waulizwe, ama wenyewe wameona yule councilor hafai tena, basi watafanya kama kula ya maoni hivi, basi wale watakaoshinda, ndio kula yao ichukuliwe, na diwani huyo awe ni mwenye kutolewa na kuchaguliwe mwingine. Sawa.

**Commissioner**: Bwana Ibrahim jiandikishe pale, Otula, halafu, Wanjiru Kirimi yuko? Wanjiru Kirimi, Wanjiru kirimi, Mary Muthoni, utamfuata, Endelea bwana.

**Otula:** Habari zeni nyinyi nyote? Kwanza ningechukua fusa hii hushkuru mwenyezi Mungu kwa kutupa huu wakati, ya kutoa maoni zetu kama wana Dandora, na wanaEmbakasi, tena nitashkuru wanacommissioner wale wamechukuwa wakati wao kuja kutusikiliza, pia ningesema, wakati huu tuko na fusa mzuri sana yakutoa maoni zetu, wakati wa lancasta, mkubuke mababu zetu walikuwa wanataka kutoa wakoroni, na ndio sababu walipatia President wao, powers nyingi, tusisahau, na leo ni sisi wakenya, powers za President, sipunguzwe, siziwe kama vile zilikuwa zamani, apewe kiasi, naye, achaguliwe na laiya, na asiwe ni mbunge wa eneo lolote Kenya. Pia makamu wake, achaguliwe pia na laiya, na asiwe pia ni mbunge wowote katika Kenya. MPs, ama Wambunge kwa jumla, wakichaguliwa, wasiwe wakienda mbungeni, wanajiongesha msahara vile walivyotaka, wakirudi huku, wanasema ni serikali haifanyi kazi, nao hawafanyi kazi, juu wakienda pale wanaangalia mimi nilikuwa na pajero sasa nahitaji macedez. Kwa hivyo sisi kama laiya, ni pesa zetu zinatumika, tukatae, vile wenzangu wamesema, tuwaangalie, ikiwa kazi yake ni kwenda kunyanyasa wananchi, tumkatae. Pia kwa councilors, au mayor, ningependa mamayors wote wa nchi yetu ama jiji

ya Nairobi, Kisumu Mombasa, Eldoret, wachaguliwe na laiya, na makamu wao (Deputy mayor) pia wachaguliwe na laiya, na wasiwe ni councilors wa ward yeyote, katika hizo jiji ndio sababu watakuja kufanyia kazi kwenye jiji hilo kazi, juu akiwa ni wa ward fulani, ataangalia hasa, kama sasa tuseme ametoka Dandora, atasema Dandora, lazima tuwe na hii na hii akisahau ya , yeye ni Mayor wa jiji la Nairobi. Tena, ningependa, tuwe na katiba nne, wafanyi kazi wa serikali, ama mfanyi kazi wowote, juu hizi imetuletea shinda mingi kaa hapa Kenya, juu unapata mtu ni PS, naye ndiye ako na business kubwa, kwa hivyo itaenda ikitokea, wafanya biashara wale wa chini, hawawezi shinda hiyo tender, juu yeye ako juu na anaharibu mambo na huko juu, kwa hivyo, wasiwe wafanya biashara. Wafanya biashara, wawe ni wafanya biashara, na wafanya kazi wawe ni wafanya kazi. Hasa kwa wambunge, nilishtuka kama mbunge wetu anasema, commissioners wale wamekuwa appointed kureview the constitution, wamefanya makosa, hasa kwanza kwangu, ni wambunge walifanya kosa juu ni hao wariwaajiri, na hawakuwaeleza wataenda kufanya nini. Kwanza tungepewa constituion sisi kama laiya, wanakenya, yule mtu ako above 18, tungepewa constitution, tujue inasema nini, ndio tukikuja huku, tunajua tunabadirisha nini ama tunaongeza nini, ama tunaongeza nini, ama tutatoa nini. Kusema ukweli ata leo unaona watu ni wachache, juu ata hawajui, hasa katiba ni nini? Na ina umuhimu hani katika nchi yetu. Wengi, ata vile aliuliza, wachache sana wamesoma hiyo constitution, kwa hivyo, sio makosa ya laiya, ama makosa ya commissioners, ni makosa ya wambunge wetu, they are our representatives, wanatufanyia nini? Ata tuwe na shida gani, hawakuji, wanakuja tu wakati kuna shinda kama vile mwenzangu amesema, pengine anataka aonekane anawatetea, sio kuwatetea, ni kuwanyanyasa, kw hivyo, sisi kama laiya wa Kenya, hasa wa Dandora, tujie haki zetu, wenginge wamesema, macouncillors tukiwachaguwa, wanaenda kuangalia makabila zao, ama familia yao, ama ni wanadandora? Tusiwe na macouncillors wale wakienda, wanaangalia sasa kama hapa tunakaa saa hii anasema pale ndio nitaend kujenga gorova yetu. Tuwe na watu waaminifu, tusiwe tukichagua wageni kutoka nje, juu akiwa na pesa, hajawai kaa Dandora, juu ako na pesa amekuja kuwapatia shilingi mia tano tano, mnampatia kula, tunataka wale wakaaji, vile mwinging tu-vet, tumjue anatoka eneo gani la Dandora, na anaelewa shinda zetu? Ata mpaka wambunge huko nyumbani, wasiwe wale wanakaa Nairobi, ikifika wakati wa uchaguzi, wanarudi pale kuomba kula, yenyewe hawaelewi ata shinda ya wale wako nyumbani.

Tukirundi kwa wakulima, ukulima iko na shinda kubwa Kenya, taxes iko juu, na ndio mnapata vitu kutoka nje zile na mbei la rahisi kushinda zetu hapa Kenya. Serikali letu, unajua serikali letu ni sisi, na hao tumewachagua, tusiwe pengine tukiona mtu moja ndie serikali, mtu moja hawezi uuda serikali, tukiwa corrupt hapa chini, inakuwa corrupt mpaka juu. Kwa hivyo, sisi kama wakulima ama nini, tungependa, taxes ziwe chini kwa fertilizer, isiwe iko juu, tunanyanyaswa zaidi. Ukienda ata saa hii ukikunywa chai kuna VAT ie. Tax.. Wengine wanafikiri hawalipi tax, hakuna yule halipi, tunalipa wote. Kwa hivyo taxes ziwe chini. (interruption) Judges, ministers, na other parastatal managers, ningependa, wawe vetted by parliament, isiwe ni Presidential appointees, wawe wanaenda bunge, wambunge wanachuguza mwenedo zao, vile ya commissioners wa kurekebisha katiba ilifanywa, tuwe na watu waaminifu, sio wale wakienda pale, anadance to the tune of his appointee (yule alimchagua). Nafikiri tukifanya hivyo kwa constitution yetu, natuongeze ya , education iwe free kwa primary, na tusiwe na watoto hawana wababa, ni vibaya sana, juu ndio inatuletea hii shinda ya watoto kuwa chokola, kama mama amepata mtu mtoto, huyo mtu lazima awe responsible, na iwe in the constitution, na kama mama hataki kusema alikuwa na wengi, pia awe wazi kusema baba ya mtoto ni nani, na wewe ukitaburikana ni wewe baba ya mtoto, take the responsibility, tusiwache watoto

watangetange, wanatangatanga juu mababa wametoroka, wamewaacha akina mama peke yao. Asanteni.

**Commisisoner**: Otula, kulikuwa na swali lakini umejibu katika kusema maneno yako ukajibu swali. Kwa hivyo hakuna swali sasa, jiandikishe. Iko wapi, Wanjiru Kimani, Mary Muthoni, Mary Muthoni, basi joo, halafu Victor Omondi. Victor Omondi, Utamfuata.

**Mary Muthoni**: Habari zenu wananchi, kwa majina yangu naitwa Mary Muthoni, mkaaji wa Dandora. Niko na maoni kidogo, kuhusu katiba yetu ya Kenya. Ya kwanza, ni laziwa katiba yetu izingatie haki za walemafu, watoto, hasa katika constitution ya Kenya, hakuna haki ya wamama, kwa hivyo ningetaka haki za wamama, ziwekwe hapa katika constitution yetu. Ningetaka, usarama ulindwe katika Kenya yetu, ni kwa sababu siku hizi, hakuna usarama ule ambao uko katika Kenya yetu. Tukiangalia katika mahali tunapoishi, ukienda unashikwa ovyo ovyo, halafu ukienda katika mahari kama Westlands, huko Muthaiga, ukionekana ukizurula,uonwe kama ni mtu hivihivi, unashikwa mara moja unapelekwa jera nahujui ni nini umeshikiwa. Ya tatu, wanawake, wahusishwe katika kazi zingine, kuna kazi zingine zinasemekana wanawake hawawezi wakafanya, lakini siku hizi, wanawake wamesoma, wako na kila kitu, na wanaweza kufanya kazi zote ambazo zinafanywa na wanaume. Serikali yetu ipigane na ustadi, tuseme kwa mfano, ukienda katika police station uko na shind yako, ukipena shinda yako hapo kabla uandikishe statement, unaulizwa kama uko na kitu kidogo, hiyo kitu kidogo dio imeleta shinda katika Kenya yetu, uko na shinda, na tena unaitishwa kitu kidogo. Jameni tunataka kuuliza, jamani tuko katika Kenya huru? Ni kwa sababu tukiwa Kenya huru, huna haja uitishwe hongo, na unapeleka malalamiko yako huko. Ya nne, kuwe na freedom of worship, hii uombaji imeleta shinda, ni kwa sababu wengine wanaomba mashetani, na hata hao ndio wanaleta vivo nyingi katika Kenya. Watu wengi wanaangamia kwa sababu ya uombaji, wengi wanasema wanaomba Mungu, na vile manene ingine wanafanya sio hakika sio wakenya. Kwa hivyo ningependelea, katika katiba yetu, mtu akitaka anataka kuanzisha kanisa, achunguzwe sana, ni kanisa ya aina gani anataka kuanzisha, isiwe ni ya kukula watoto wetu. Ya sita, ni undanganyifu, katika Kenya kumejaa undanganyifu ata ikiwa iko katika ufisadi, udanganyifu umejaa, na umejaa katika hawa watu wako na pesa, kwa sababu tusema ukienda kuuliza kazi kama wewe ni msichana, unaenda unaambiwa kazi iko, kuja jioni, na ukiingia jioni, kumbe sio ile kazi ulikuwa ukitarajia unaitiwa kazi ingine. Kwa hivyo ni vizuri ni vizuri, watu sasa haswa wale wako kwa maoffice wawe wakielezea ukweli, kama hakuna kazi, wanasema hakuna, kama iko, wanasema iko, na utapewa kazi saa hio. Ya saba, ni kupiga kula, sisi kama wapigaji kula, kuna wengine hawaruhusiwi kupiga kula, kama wale watu wako jera, na ni watu wazima wamefikisha miaka, ni watu wako na utu wao, na hawaruhusiwi kupiga kula. Ningeomba katika katiba yetu ya Kenya, hao watu wako katika jera, waruhusiwe kupiga kura ni kwa sababu hata hao wako na haki yao, na ni lazima wapeane maoni yao huko. Ata kama wa sasa tunapeana maoni yetu, ni vizuri ata kwenda huko kwa jera, maoni yao wapeane huko ni kwa sababu wako free. Na kama mahospitali, hawapewi ruhusa ya kupiga kula, na kuna wengine wanajisikia ni ya wangetaka kupiga kula kwa sababu hao ni wanakenya, na wangetaka kujichagulia, yule wanataka awaongoze. Ningetaka siku ya kupiga kula iwe public holiday, ni kwa sababu wengi hawapigi kula kwa sababu wako maofficeni, wengine hawapigi kula ni kwa sababu wako kazini mwao, iwe ni sheria, yule ambao hatapiga kula, awe akipelekwa kotini kwa nini hakupiga kula, ni kwa sababu watu wale hawapigi kula ndio wanatuletea mashinda hapa Kenya, kwa sababu tukichagua mtu wanasema sisi ata hatukuwa tukimtaka, na ni kwa sababu hao

wenyewe hawakuhudhulia katika kupiga kula.

Ingine ningetaka kusema, katiba itolewe na iandikishwe kama vile wanaweza kujisomea hao wenyewe, na hio katiba ikiandikishwa, tupewe iwe distributed kwa vikundi, mashule, makanisa, ndio kila mmoja aweze kusoma sheria na aweze kujua katiba in nini. Kwa sababu watu wengi wanakosea, na hawajui kwa nini wanakosea, kwa sababu hawajui sheria ni nini, hawajui katiba ni nini, ata hawajui ni nini inawasimamia. Kwa hivyo ni vizuri, watu wote wajue sheria ni nini, na katiba ni nini.

Kitu ya tisa, ni katiba ya baadaye, ichapishwe na lugha zote. Hio nimesema.

Kitu ya kumi, ni katiba yetu ya Kenya, ichunguze wale wanaofanya mabiashara, ni kwa sababu wengi wetu tunafanya mabiashara katika hapa Kenya, na sisi dio tunathulumiwa zaidi, na tuseme watu kama Asians, dio wako na makampuni kubwa, na ndio wako na pesa zile nyingi, ijabokuwa hizo pesa zao, hawaweki hazina katika Kenya yetu, wanapeleka kwao, katika nchi za kwao, kwa hivyo zinazaa huko kwao, na huku kwetu hazizai, kwa hivyo ningependelea, kama mtu mkenya anataka kuweka biashara yake, ama nini, awe huru ya kuweka biashara yake. Na huyo mtu mAshian ameweka biashara hapa Kenya, achunguzwe, aonekane hazina yake iko wapi, kama haiko hapa Kenya, aende akafanyie biashara kwao. Asanteni kwa hio machache.

**Commissioner:** Asante Muthoni kwa maoni yako. Sijui kama kuna swali, hamna swali, umejipendekeza vizuri, tumeshukuru. Victor, halafu Athunus Openda, utamfuata, Jina halafu endelea.

**Victor Omondo**: Hamjamboni nyote? Kwa majina naitwa Victor Omondi Odero, mimi ni mkaaji wa Dandora, natoka katika kikudi cha Dandora Pricing Youth, Vile niko hapa, ningependa kutetea vijana sana, kama swala langu la kwanza. Ningependa serikali, ama katiba yetu ya Kenya, iweze kupatia vijana (nikimaanisha vijana, namaanisha mtu wote ako zaidi ya miaka kumi na nane mpaka 45 years – huyu ni mtu ambaye bado ako na nguvu, ambaye anatumikia serikali) Kwa hivyo ningependa serikali kwanza, itie mkazo, ama izingatie vijana sana, wanaume kwa wanawake, mjaribu kuangalia vile vijana wanaweza kaa kwa sababu, sisi vijana ndio tuna nguvu ya kufanya kazi, ama tunaweza kusaidia serikali kwa njia zingine, ijawapo wanatuhitaji.

Swala langu la pili, ambayo ni mhimu pia, ni upande wa medical, upande wa medical ningependelea, ama hospitalini, ziwe bure kwa sababu kila mkenya anatoa ushuru wake, ukinunua mkate, unakatwa sumuni, kila kitu ushuru, kwa hivyo hata ukiwa mgojwa, ambao ugojwa si kupena kwa mtu, ningependa serikali, izingatie hio, ili iweke medical effect free for all, kwa sababu ukiangalia pande kwingine unapata mtu ni masikini ambaye hata hawezi kuafford kujipatia hata card ya hospitali, na kitabo hapo awali, ulikuwa ukipelekwa hospitali, kulikuwa ni free, baadaye ikakuja PAYE na hawa wabunge wetu.

Jambo lingine na pili, ningesema police, police should be reformed. Jambo la tatu, free education for all, watu wote wapewe masomo ya bule, wazima kwa watoto, kila mtu apatiwe masomo ya bure. Kwa upande mwingine, ningependa kutetea

walemavu, serikali ama katiba yetu ya Kenya, iweze kutabua walemavu watu, wasiwaache tu hivyo, ati kuwa hao ni watu hawajiwezi. Walemavu ni watu wanajiweza isipokuwa labda hawana mikono, vile mwenzetu alivyosema. Kwa hivyo, katiba yetu ya Kenya iweze kutabua walemavu wote na iweze kuwasaidia vilivyo.

Upande mwingine, ningependa kuongea about upigaji kula, ama voting. Ningependa kupendekeza hii pendo iwe pendekezo langu, kuwa kula, wakati tunachukuwa kula, serikali ama katiba ikubarishe kila mkenya, ingawapo ulichukulia kula yako Embakasi ama Dandora, ama wapi, popote ulipochukulia kula, ikiwa unaenda tafadhali, ***(interruption because of the hot sun)*** upande wa uchaguzi nilikuwa ninasema, katiba yetu ya Kenya, ituruhusu, mtu yeyote pahari alipo, ingawa uko na kula kwa mfuko, hata ulichukulia Embakasi, ulichukulia Ngomongo, ukiwa umeenda nyumbani hata Kiambu, wakati wa uchaguzi upatiew hio furusa uwezo kupiga kula yako popote ulipo, na uweze kuchagua mbunge wako popote ulipo, si lazima ukuwe ati wee mkaaji wa Embakasi, na kupigia kula yako ati upigie Embakasi, we na siku ya kula ati upatikana Embakasi. Ningependa hio pendekezo langu pia, liweze kuweze kufikishwa hapo.

Upande wa budget kuu ya serikali, ningependa budget ya serikali ambayo ina deal na sisi wakenya wote, budget ya serikali yetu ya Kenya ifanye vile tunawezafanya kutoka kula za maoni, serikali itumie commissioner wake, kukuja kuuliza watu, ni nini ingependekezwa kupandishwa juu ama kusukishwa bei ama nini. Wahusishe laiya wote, vijana kwa wazee, watoto kwa wasichana, watu wote, kujenga budget ya Kenya.

Elections, President, ama Rais wetu wa Kenya afaa kuchagua tume la uchaguzi kwa sababu wakati amechagua mtu yeyeto, mtu kama Paul Ghai, mtu kama tuseme mtu kama Mswako, upande wa judiciary, hiyo inaongeza XXXX katika nchi yetu, kwa sababu utapata watu wote wamechaguliwa na Rais, lazima wafanye kazi ya Rais. Kwa hivyo ningependa pia upande wa ukula huko, ikuwe ni laiya wanahusika ama parliament, wahushishe watu wengi.

Upande wa mahakama, ambapo ningependa kuongeza kidogo, the Attorney General anafaa, ama ningependelea, achaguliewe na makanisa, NGOs zote, na laiya wote wa Kenya. Kwa sababu huu ni mto mmoja ameshika nafasi kubwa sana, hapo ndio roho ya serikali iko, kwa sababu inapata, ikiwa huyu mtu mmoja amechaguliwa na serikali, ama amechaguliwa na mtu mmoja, huu mtu atapendelea, ama atakuwa anasalimiwa pande moja sana, ambapo sisi masikini, ama vijana wale wawajiwezi ama wazazi hawajiwezi, kupata haki na ukweli itakuwa vigumu sana. Kwa hivyo pande hiyo wa judiciary ningependa Attorney General achaguliwe na makanisa, laiya, ama Parliament. Halafu kuna equal distribution plant, kwa sababu Kenya twajulikana ati kuna squarters, Kenya hakuna squarters, kitu ingefanya serikali iwe na mpangilio mzuri na ikizingatiwa katika katiba, kila mkenya ana furusa ama ako na ruhusa ya kuminiki shamba, kwa hivyo kila mtu, serikali itafute kiwaja mzuri, ipatie kila mtu fusa ya kupatia kila mtu kiwaja kidogo, kwa sababu hakuna kitu baya, kama unapata mtu mmoja anaminiki shamba 500,000 acres na mtu mwingine hana shamba, halafu tunasema kuko na squatters. Shamba hiyo ya mtu mmoja na anaminiki shamba kubwa kama hii, ni vizuri igawanyishwe natika wakenya ambao hawana shamba. Asanteni kwa machache.

**Commissioner:** Asante Victor kwa maoni yako tumeshukuru, jiadikishe pale, nilikuwa ni memwita nani mara ya mwisho? Athunus Openda, endelea, halafu, kuna mtu mlemavu, mtu mlemavu? Kwa hivyo karibu utamfuatia Openda, halafu nitakuita wewe baada ya dakika kidogo tu. Endelea.

**Athunus Openda:** Asanteni sana, mimi yale ni nayo, ni yale wenzangu wameshayasugumzia, na mimi nitaenda juju. Jina yangu ni Athunus Openda, mimi naongea juu ya MPs, tunawachagua, wanaenda huko, wakishafika huko, tena hatuna jukumu ingine yeyote, na hiyo ni contract between sisi na hao. Kwanza ningependekeza hivi, tuwe na uwezo wakati ambao hawatekelezi majukumu yele ambao tuende huko, tuwaite, na ikiwa twapata ambao hawawezi, tunaweza chagua wengine, badaada ya kuongoza miaka mitano ndio sababu inaleta corruption, wanakula, wanakula, wanajua 5 years is enough to eat with my children, my family, that's all. Ata bado miaka 5 mkikosa kumchagua, atakuwa tayaari ametosheka. Vile vile, madiwani na mamayor pia tukiwafanya namna hiyo, kwa maana tunawachagua waende huko kutuakilisha, si kujiakilisha huko na marafiki zao. Na pia ata mishahara pia, kwa sababu sisi diye tumewatuma huko, tutakuwa tukihusishwa kudetermine pia mishahara yao iko namna gani, badala y kujiongeza huko, wanatuacha tukiangaika hapa na pale.

Jambo lingine ni xxx rights, ningependa kama mambo kama security, health care, water education, shelter, food and employment, iwe kama ni mahitaji ya kimsingi, kila mtu mkenya yote anahitaji kupewa na serikali. Hakuna aja kusumbuka kusoma, kufika huku kuja hapa hakuna kazi, tunaangaika huku, kwa nini tunaenda shule kama serikali haina mpango ata kiti?

Jambo lingine, ni disadvantaged groups. Serikali kwa wakati mwingi inaimba, inaimba kuna pesa kwa wale ambao hawajiwezi, hapa hapa miaka nenda miaka rundi, na hizo pesa sisi hatuzioni. Kama kwa mfano, kuna wakati pesa zilichangwa millions of shillings to the disabled people with disabilities, mpaka sasa sijui kama zina fanya kazi ama ziko wapi? Kwa hivyo hatiba yetu izingatie haya mambo yoote, imake sure kuna mipango thabiti kuhusu wale ambao hawajiwezi, na wale ambao hawajiwezi, kwa mimi nasema ni watu with disabilities, poor people, and landless. Hivi majuzi, jambo lingine, vile mmeona Kenya hakuna kazi, watu wanafutwa kiholelaholela hapa na pale, serikali yenyewe ndio ya kwanza sass kufuta watu, kuna malipo ya uzeeni, mtoto wa miaka ishilini ana thelathini hufutwa kazi, halafu ikiwa kama ulikuwa umesfafe pesa yako karibu 100,000, ukienda huko kuitisha, unaambiwa uongoje miaka ingine thelathini ufikishe miaka 55. Kuna watoto wakufudisha, wakusomesha, sasa sijui utagoja thirty years ndio upate hizo pesa uweze kufundisha watoto. Kwa hivyo ningependekeza katiba, ifeel hii malipo ya uzeeni, iwe kama akiba, savings and credit (kama bank) ambaye wale ambao wameachishwa kazi wanaweza kwenda atoe akope, afanyie business yake, badala ya kuongoja miaka mpaka uzeeke labda wakati huna hata meno ndio unaenda kuchukua pesa.

Jambo lingine, ningeongezea, ni constitution amendment, kutengeneza katiba vile hapa tume mumejua ni jambo la too expensive, linachukua muda, linapoteza sana, sio jambo la busara baada ya kutengeneza halafu liende huko for few people, mame people waanze ku-amend, that will be.. sasa inapendekeza hivi, vile wenzangu wamesema, anything, any clause in the constitution to be amended should be brought back to the people to go through, through the refurrundum, or in whatever method, not through

BBC disintegrated committee, ambaye inakuwa represented with all groups. Ikipitishwa na wananchi, ndio sasa MP concerned kila constituency halafu inatoa pendekezo ile jambo ambalo lingebadirishwa, baadaye sasa MP ndiye analipeleka huko parliament for further debate, kama hii, ikifika huko parliament kama currently we have 210, ikiwa constituency zote mingi ya hizo zimependekeza hio kitu ibadirishwe katika katiba, basi dio inaweza kubadirishwa hata MP, lakini nimekataa, about hiyo isibadirishwe hata kidogo. Hiyo ni maoni yangu na mimi nimependekeza katika system of governance. Katika Kenya, tunaonekana kama hii ni jambo la wazi, watu wanafanya XXXX based on tribal lines. Hakuna chama ambao kiko katika kila mahari hapa na pale, na sasa utaona for the last, more than 20 years, watu was Kenya wameteseka sana kwa sababu watu wanang'ang'ania tu uongozi, wanauda vikundi watawale, siwafanye mabadiriko, wanataka tu watawale, ile aongeze kabila yake huko mbele, because of this, na hatuoni dalili wakenya kubadirisha, kwa maana inaonekana kama ukabila katika Kenya umekuwa ni kama tanga (kutoa ni ngumu). Mimi kwa maoni yangu, naona kama sasa kutatua hii tatizo, basi leta tuwe na "get your system" ndio kila mtu aende kwake atawale, kama ni Kibaki atawale huko Central, mwingine atawale awache huko ndio watu watosheke, tuwe na maendeleo badala ya kupigana miaka na miaka tu, huko juu na sisi naendelea kuteseka.

**Commissioner:** Point mbili za mwisho bwana Openda

**Openda:** Haya, because of that, because political parties are normally based on tribal lines, then I recommend, it will be possible, to have independent candidate, badala ya kukua mara ukuenda kama huko DP, hawezi kunichukua anachukua marafiki zake. Nikitaka kuXXX mimi nienda kuXXX kama concillor ama niende kama parliament, hakuna mahari popote naweza kupita, lakini kama ningekuwa na uwezo, ningejisimamia mimi mwenyewe, nipambane na wengine. Ni haya tu asanteni.

**Commissioner:** Asante bwana Openda, jiadikishe pale naupeana hii memorundum ndio itusaidie kwa record yetu. Karibu dugu yangu, halafu Josephat Nyota yuko? Josephat Nyota, Nyota, Robert Kaondo.. Endelea endelea, sema jina, halafu utoe maoni yako,

**Benson Mutuangita:** Habari wananchi wa Kenya wote? Kwa jina naitwa Benson Mutuangita, mimi ni mwanabiashara hapa Dandora, Mimi nafikiria, hii watu wa constitution review, ni kama Jesus ama XXX, Yesu alitumwa hapa duniani na Mungu, huwa kama walikuwa wenye dhambi, na nyinyi Mungu amewachaguwa hapa Kenya, kwa sababu watu wa Kenya wana Shinda ya kutosha, shinda imeingia hata kwa mifupa, Nafikiri nikiongea hivi, mtu fulani atafikiri, sio mimi naongea. Nchi hii yetu, sio wakubwa kuanzia chine kwenda juu, nchi hii yetu wananchi hawa ambao wanafanya kazi ya kujenga nchi, na hawa wananchi wanapata shinda sana, kwa hivyo mimi naomba sheria ikitengenezwa, wacha kusema habari ya President, ya DO, ya Chief, ya nani, ya nani, hata wakati wakale, wakati hatukuwa na waongozi, hatukukaa, nataka sheria iangaliwe kwa mwananchi kawaida wa chini, ameumia sana, na we unaonge hivi na hivi na hivi, Nyoka ikija hapa tutapiga miguu? Tutapiga kichwa ikufe, kila mtu anajua Kenya, wacha kupitia bali na hapa na hapa, shinda zile ziko, hasa kama corruption, corruption imeenda mpaka kotini, na bila kulekebisha koti ya Kenya, wacha Mr. Chunga alikuwa anakataa juzi, bila kulekebisha hata tupange sheria gani, hakuna kiti itaendelea, Kwa hivyo NO. 1, ningewauliza hata hao majudge, whateveve, whatever, mpaka police, wote wafukuzwe, na mtu akipatikana na hatia, aende ahukumiwa. Saa hii naongea iko na watu, ni watoto wa watu? Bona hao sio watoto? Bwana

Chunga ambao wanasema hakuna corruption? Tumeona, kuna mtu fulani najua, case yake ilianza miaka na miaka na miaka na miaka, na mpaka waleo haijaisha, kuna mtu aliimba viazi pale, alifungwa na akatoka, hakuna corruption XXXXXX? Imefika mahari mbaya sasa, nimewaambia shinda imeingia kwa mfupa, na nyinyi wenye katiba mjue, nyinyi ndio Moses ama Jesus, if you are not concerned with people, even if you are not concerned with this country, kutakuwa na conflict, kondoo wameingizwa na chui, kwa corner lazima wapigane sasa, inafanya mtu akwambie ilikuwa ilikuwa, kwa hivyo, mimi maoni yangu kubwa ni hii, sitajitetea kwanza, nitatetea wananchi, shinda kubwa, ni hii ya mwananchi wa chini wa sukuma, wa viazi, wa madazi, sababu pesa yatumika, ata wengine wamesema hapa, pesa yatumika, na hawa watu wengi wanaondoka wana wave hiyo tax.

Jambo lingine la kuuliza hapa, na wengi wasikie, najua wengi watasikia vibaya, serikali ya America ata wapi, imetengeneza Ministries ambozo zinahusiana na kila kitu. Unaona mguu moja kutoka hapa, nakuwa ni mwito fulani, anaanza kuuza mashamba, I pocket the money in my pocket, why? Procedure iko, si iko procedure? Ile ambao ministry ikitaka kupinduka hivi, ata najua city council haina jambo yeyote, inapewa sehemu kidogo ya city. Hawaaminiki kwa sasa XXXX , imekuwaje sasa? Mi naona watu hapa hapa hapa, hapa tuko saa hii, kazi yao nikuuza mashamba na kuweka pesa, pia hiyo ni corruption moja kwanza kubwa sana. The land is a very XXXX issue ambayo inawezatajirisha watu mara moja. Nafikiri wengi mumeona hapa, si XXX alikuwa hapa? Ni kweli? Kwa hivyo naomba hii katiba, kwanza land iangaliwe zaidi sana.
Kuna watu wengine wako na na powers sana, askali hapa anaweza toa wewe mapua, DO ata nywele za masikio atatowa wewe, kuna DO nilisikia huko Kiambu alinyoa watu nywele, Hizo sheria ziko powers zote, kwanzia DO, mpaka hiyo mkokoro yote, sababu jioni wewe unaweza kuwa President, ama whatever, Si wewe ni mama, ama we ni kijana, ukienda kununua XXXwee unakuwa somebody special, wacha ile mnasema VIP, nani VIP hapa duniani? Nani VIP? Yote hakuna mtu VIP, sababu watu wote ni moja, Mungu aliumba mtu mmoja, na hata hao viongozi mnaita nani nani, MP, councilor, whatever, hao wamechaguliwa na laiya iwasaidie, si kwenda kunyanyasa, kwa hivyo, mimi naomba, kile ningatakia sana, ni ile corruption ikuwe cleaned, ndio mtu akikosa, ata akikojoa kwa kitanda, anapelekwa kotini na anashtakiwa. Kwa hivyo, corruption ikiisha hii XXXX zitaisha.

Jambo lingine naongea – walemavu, hapa Kenya ni kama maiti, haki, beggars zote walemavu, hakuna mtu amejali, ata unaambiwa kule kwa tinga, hao si watu walizaliwa? Nani alisema uzaliwe bila macho, bila masikio, bila miguu? Hata wewe saa hii, anybody who is strong here anaweza kubecome disable, ata nani ata nani, kwa hivyo, ninauliza sheria iwe imetengeneza, iwe inaangalie walemavu. Mimi sitaki kuongea mengi, lakini Kenya, powers, ikiwa ni kutoka police, ikiwa kutoka ni wapi, kuwe na democracy wananchi wache kuishi nchi hii ya police, si ya Rais, si ya mtu officerji, ni wananchi unawaona hapa. Kwa hivyo hizo powers zikatakatwe, mtu awe normal person. Na court corruption ziangaliwe, ziishe kabisa, iikiisha, ikikosa, likikojoa, likojoe kitanda, ili ikikojoa, kesho niko kotini. Ndio unaona mnalia hapa, elimu, police, nini, sababu, kuna watu kesho apana sitakiwa. Kwa hivyo imalize corruption, point zangu hizo namaliza. Asante sana.

**Commisisoner:** Matua kwa maoni yako, basi wacha akuletee register ujiadidishe pale.

**Mutua:** Hakuna swali nimjibu?

**Commissioner:** Swali hakuna, umejieleza vizuri, umejieleza vizuri hata aja ya swali.,Asante sana N. N. Kamau, N. N. kamau, Omondi Okello, Omondi Okello, Isaak Mwangi, wewe ndiye nani? Highlight your memorundum in five minutes, pick out the most important points.

**Omondi Okello:** My names are Omondi Okello, I represent Jirani Mwema, Basically, we have a memorundum, which I think we had represented, so I think I will just highlight some of the areas there.

The 1st issue is supremarcy of the constitution, in our view, we believe that the constitution, should not be changed by parliament, but rather by a refurrundum, that's our 1st view.

On political parties, we believe, that political parties should be minimized, we should have many parties, because we believe many are formed along tribal lines, if they are minimized to about parties at a given time, and conditional set where a party can be registered and another one registred, then it would bring order in registration of political parties. We also believe that appointments in public offices should be done by the President but vetted by the parliament, and we believe that contesters for parliamentary seats, should be of O' level standard of education. We also believe that Prime Minister or President as the case may be, should be impeached through special tribunal where necessary. When we come to the Local Government, we believe that mayors, and chairmen should be elected directly by the people and councilors should have a minimum of O' level of education. There is one which we also want to highlight here (it has been said by many people), concerning basic rights and in Dandora we find that it has been notorious for police especially using section 5 of the constitution, we believe they have been capitalizing on us a section that gives them power to to arrest somebody on suspicion, for this, they have been using to harrase people, so we believe that this section should be made in a way so that it will be difficult for police to harass innocent people, and only arrest people who are criminals. We believe that, during the process of election, the incubent President should not be in power of election, and a chief justice should be incharge, while the President, after 13 days should be able to give power to the incoming President. Those are the summary of our views.

**Commissioner:** Thank you very much, there is no question, I think you were very clear, give your memorandum and register again. Ouko, halafu, Rose Mueni Makau, Rose Makau, Utamfuata, baada ya huyu.

**Paul Ouko:** Mimi kwa jina, naitwa Paul Ouko, na mimi nataka ongea, juu ya disabled. Naona mambo mengi imefanya disabled wanakuwa masikini zaidi, President wetu alichangiza pesa, ili kila mlemavu asaidike. Na hizo pesa haiwezi kusaidia disabled, kwa sababu baadaye President alichagua wale ambao ni able bodied, dio apatiwe pesa. Utaona watu wengi wanaogoma town, na hizo pesa zilichangwa ili zisaidie disabled, na unakuta, wale ambao si disabled, wanakula hizo pesa. Sheria lazima iwekwe, disabled analipa hizo pesa wenzao.

Na pia mimi nataka ongea, juu y mortuary, serikali inafanya biashara, na wale ambao wamekufa, kwa nini? Mtu amelala pale,

sasa akilala siku moja, iko pesa juu yake, na yule ambaye amekufa, alikiwa analipa kodi. Na kwa nini serikali hawezi, yule awekwe pale, atolewe aende azikwe tu, bila kulipa chochote?

Mimi nitaongea juu ya police – police pia wananchi sisi ndio tunawajiri, kwa pesa zetu, na unakuta police anakuja kushika suspect, na akiingia kwa nyumba, mara moja amepiga huyu suspect mbele ya watoto na bibi. Na hiyo inakuwa tabia baya, Ningetaka sheria, police akija akuambie unatakikana pale, sio anakupiga pengu, ama akupige mpaka ulale chini. Hiyo sheria lazima iangaliwe. Unakuta kuna watu ambao walizaliwa sijui walizaliwa namna gani? Unakuta mtu mmoja ako na plot karibu mia na kitu, kama yeye ndiye alizaliwa hapa Kenya alikuwa sijui namna gani, ingefaa sheria iwekwe, mtu moja, plot moja, si mtu mmoja plot nyiingi ati kwa sababu ako na pesa. Hata wengine ambao wanazaliwa sijui watapata plot kutoka wapi ikiwa mtu mmoja ako na plot elfu na kadhaa? Sheria ingewekwa, mtu moja na plot mo? Moja. Si kwa sababu niko na pesa nikisikia plot ingine pale, nimekimbia, kwa sababu niko na pesa, na wewe je? Si mtu mmoja amezaliwa hapa Kenya, kila mtu ako na right, yakupata plot, mtu mmoja plot mingi. Hiyo sheria iwekwe. Tena, treatment, hata mimi na shangaa, unakuta watu siku hizi wanakuf tu kwa manyumba, kwa sababu gani? Serikali waliintroduce, cost sharing, na cost sharing kwa masikini, atalipa nini kwa hospitali, yule anaogopa tu kwenda kwa hospitali, huko akalipe maelfu ya pesa, na yeye ni mgojwa, sasa lazima anakufia kwa nyumba, alafu ambebwe na mkokoteni, kwa sababu hakuna ambulance, unakuta anambebwa na mkokoteni na serikali iko, serikali inafanya kazi gani? Yakuzaliwa wananchi, na kuzaliwa wananchi lazima ajitolee. Watu wanalipa husuru, kama sio hivyo watu wasilipe husuru. Kwa sababu hakuna, unaona zamani watu hawakuwa wanakufa kama waleo, wengine wanasema ni ukimwi, sio ukimwi, ni kukosa tu pesa ya kwend hospitali unakufa tu sababu hauna namna ya kufanya. Sheria ingewekwa, watu wapate free treatment. Hivyo tu ndio maoni zangu, Asanteni.

**Commissioner:** Hamna swali, umejielezea vizuri, jiandikishe kwa maoni yako, asante kwa maoni yako. Rose, halafu Gladys Wambui, Gladys Wambui, utamfuata tu, Endelea Rose, majina yako halafu utoe maoni yako.

**Tape 4**

**Rose Mueni Makau:** Mimi naongelelea kuhusu, lakini ile ningeongea kwanza saa hii ningeongelea kama mkubwa wa police angekuwa hapo, lakini ameondoka, na ningeongea kama Mwenje yuko hapa na ameondoka, kwa sababu wakati wa jumamosi, juzi, mimi naongea kuhusu Gitari Marigu, hii Kinyago, juzi jumamosi, nilikuja kuitwa kwa nyumba yangu, saa sita, saa saba usiku, kuna mama alikuwa anakufa hapa akikuwa mgojwa sana, na sikukuwa na pesa, na yule mama, mtoto wake ni mtoto wa miaka kumi na nne. Sasa vile nilikosa pesa nikapata mia saba, nikaona magari haiko nikakibilia police Kinyago, kwenda Kinyago, nikakuta mkubwa, mkubwa karibu anipige, nikamuomba, nisaidie, gari ya police nitoe mtu kijijini yetu na ni mtu mgojwa, Huyo mkubwa alikuwa hapa saa hii, akaniambia niende nimbembe na mgongo nipeleka hospitali na hapo kuna faida. Hio ni haki? Na ukikuwa na shinda, unakimbilia police, mkubwa ndiye ningependa anijibu, lakini ameondoka.

Ya pili, mwaka wa 1989, tulikuwa kule kijiji ya Kinyago, mwaka wa 1989, huyu mheshimiwa Mwenje ametoka hapa, alikuja akatutoa kule tulikuwa, kwa maplot zetu, akakuja kututupa chin ya sewage, na hii chini ya sewage, tuko hata wasasa, mama kama huyu hana mguu, hana pahari ya kwenda kujisaidia. Na ya pili councilor Mwangi, naye amekuja hapa, hatuna choo hapa chini, na sewage yote wakati mwingine, imekuja kama inatobolewa, sasa maji yetu ya sewage inatelemka chini kule tuko, na

watoto wako wengi kule, na hii kijiji, ni watu wengi wako na ugojwa wa TB, na ni wamama wengi wale hawana kitu ya kujisaidia kujenga choo. Mwangi councilor wa hapa, akakuja tukamuuliza, ma-sewage imetobolewa, tutafanya nini na tu tuko na shinda ya choo? Wengine kama mama ya choo, mtu akifika anakwenda mtoni, anachukua kasuku anakwenda kwa choo kwa sababu hana hata la kufanya. Councillor akasema tutafute pahali atatujengea choo, na ni hapo, mwaka hio yote hatujamuona, na tukitoka na nyinyi tuandamane, hata saa hii, hizo sewage zote zimefunga, zinaenda kutuletea chini, mimi nauliza, tutasaidiwa na serikali, ama tutasaidiwa na nani?

Ya pili, watoto wengi hii kinyago, ni masikini tupu, ile ziko hapa, watoto ni kama elfu tatu wale hawasomi, wale wako hapa, wengine hawana mama, hawana baba, mzazi wake ni mzee amewachiwa na mtoto wake ameshindwa, tufanye nini? Wadugu, kuhusu hao watoto? Tunaomba usaidizi yasiwe sewage xxx kuja kwa manyumba. Kwa saba imetokea huko, city council wakakuja wakiitomboa, kuitomboa, wakawachia hivo hawakurudi kuja kutengeneza, na wale wako huko, sio wanyama, ni watu wako chini ya sewage. Au sio hivo serikali itutafutue, pale tunaweza kwenda, tutolewe chini ya sewage, kwa sababu sisi wote ni watu, kama wale wengine.

Ile ingine nauliza ni kusema, mtuulizie mtu wa serikali, mkubwa wa serikali, tutakwa tukifanya nini, akija hapa anakuja kushika chang'aa, na hiyo chang'aa, ndio inasaidia watoto. Akiambiwa, sababu watoto hawaendi kuimba, wakishika watoto, wakija, badaala ya kuongea na yule kijana vizuri, anaenda kumpiga, na kumuweka pengu, wakifika hapa, anamnyang'anya ile pesa, ile mtoto ameanza kujisaidia nayo. Na hiyo watoto wanajisaidia kwa sababu, hawataki kuimba, hawataki kufanya nini, ukifika pale juu, usiku huwezi kutelemka kijijini, juu ya askali, mnafanganishwa tai, mnafunganishwa coat, mkifika pale ni mia tano tano, elfu moja moja, kwa hivyo mtuongelelee kwa police tuwache kushikwa ovyo ovyo, na mtuongelelee kwa serikali tuondolewa kule chini mavi, kwa sababu sisi ni watu kama wale wengine, na watoto hapa ni zaidi ya elfu tatu, hawana makao, ni kama chokola, na sina mengi ya kuongea.

**Commissioner**: Asante sana mama Rose, neenda pale ujiadikishe, mama karibu, uko sawa ama tukuletee microphone karibu? Halafu, Stanley Macharia, Stanley Macharia, Stanley Macharia, Alice Kalundu, utamfuata mama Wambui,

**Gladys Wambui:** Muriega? Nii njitagwo Gladys Wambui, na njikaraga Kinyago, na ninjikarite miaka miingi muno tundu, ni miingi, onandari umwe waguthamio ni Mwenje na guku, ngirehwo guku ngirwo ikaraga hau ninguka gukuiga handu hega,

**Commissioner**: goja kidogo mama, mpatie akutafutie

**Translator:** Kwa majina anaitwa Gladys Wambui, anasema ni mkaaji wa hiki kijiji cha Kinyago, na mmoja wa wale watu ambao walileta na Mwenje katika kile kijiji.

**Wambui:** Ninduraga ngietereire Mwenje oke agitwire riu ni hindi tugugithamio, na tutire twamuona no okire gugitwira tumucagure ringi, na turi o kianda, na ndehota guka gutwira aturute guku riu, atutware kuria mai matakiri, arenda tuikare o guku maiini na tumucagure o ringi.

**Translator:** Wakati mwingine hatumuoni, huwa anakuja tu, wakati anataka kula kutoka kwetu, na hakuji kutusaidia kutoka

kule kijijini atupeleke mahari pengine.

**Wambui:** Niumwe wa kumenya tuokire guku ciana iri nyinyi, na riu ciana icio ina miaka makiria ma miaka ikumi na itano, na irioguku itire githomo, itiri wira, itire giakuria, irathumbuka o na manyina mao, nimwiraga kumenya atuheiri o mundu room imwe imwe, turi thi-nii wa guthinika na ciana icio tondu riu ni ng'ima, niirenda gukorwo iri na micii yao, na itiri wira, riu no thirikari yugage ciana icio, ni mikora, na ti mikora ni thina, ni kwaga wa gwika, makambiriria gwicariria kiria mundu angihota kuria.

**Translator:** Tulikuja hapa tukiwa na watoto wadogo, na sasa watoto wetu wamekuwa wakubwa, wangine wako na miaka kumi na mitano, hawana kazi, na unakuta huyu Mwenje alitupatia room moja moja, na sasa watoto wetu hawana kazi, na kwa hivyo wanaambiwa ni wakora, na wanaanza kuhangaishwa.

**Wambui:** Angikorwo ni kundu kuria thirikari yatwira ni igutuhe handu tugaikare, tutiri na munyiti mbaru ati ciana icio ciheo handu o mundu room imwe na ndakaheo igiri, ni getha ihote kwi ikaria na kwirugamirira, matingitikira kumahe, no githina gia kwendia, na gwika maundu maria mangi, nacio ciana icio ihangaikage.

**Translator:** Hata kukawa na fuza ya sisi kupelekwa mahali kupewa mahari pa kuishi, hakuna mtu ambaye anatusaindia kupata jambo lili, ni kuachiliwa tu ati hatusaidiwi watoto wale wapate ata ingawa ni room moja moja ni kuwachaliwa tu kunakuwanga kuhangaika.

**Wambui:** Nikuri na ciana irambiriirie mufano wao, marore kana no mahote, kwinyitirira, nyonaga mgikuwa mahuti haria makite kawanja kao, makarutaga mahutu guku thiini wa andu, makaheo tuthendi tunini, na nigetha ciana icio cione kindu giakwirugamirira, ndiri ndirona murugamiriri ucio tuthurite, councilor, tutiri turamuona oke ameri atiriri, riu ciana ici tondu ni mwethiurururukiria hahari, mukwend atia? Tukwenda utuongerere mbeca na ithui tuhote kuruta wira, hatiri

**Translator:** Kuna vijana ambao wamejaribu, wanajikusanya, na kuanza kuokota takataka hapa na hatujaona mtu yeyote, hawa wakubwa hata kama ni councilor, ama yule tumemchagua, kuja kuwasaidia, ata kuwaongeza, wale vijana pesa, hatujawaona hata kidogo.

**Wambui:** Riu no mokire, na uhinga wao, utuku moke mamaingiririe maundu maria matagiriire meke, na nigetha makanyitwo, makahurwo, makohwo, na uguo ni kuherithia aciari, aria mokire na ciana icio, no gutumithia na turi ngurumo, no kuo tuthiagira cioro ta cukuru, tutiri cioro, tutiri ki, tuikaraga o uguo nakuu kianda kiu.

**Translator:** Kazi yao tu nikuja usiku kwa ujaja ujaja na kuaanza kurokota wale vijana na kusema ni wakora, na kuwathurumu, na pia kuja kule kwetu kwenya hatuna choo, tunajisaidia kw kasuku, kwa sababu hakuna cha kufanya.

**Wambui:** Nii ndahoya thirikari iria iguka, akorwo ni ikwenda wega, yambe icagure aanake acio anini aria othe mahingitie kuma miaka 14 kinya 20, macagurwe mambe monio kuria meguikara, na mawira maria marirutaga, na nigetha waganu uthire.

**Translator:** Mimi ningeonelea, serikali iangalie hawa vijana, ambao wana umri wa kuanzia 14 hadi 20, watafutiwe mahari pa kwenda ili huu umahaa ambao wako yaishe.

**Wambui:** Tondu, ugima wao ni uraiga nimekwenda micii, na mwana ekwira ithe ni ekwenda mucii ni kuguranirwo

aguranagirwo, riu tondu niekwenda mucii, na ni muciari mwinake ri, na ringi ona ndari ithe ni akuire-ri, ringi ni muthuri wina ciana mutumia niakuire ri, e gwika atia? Mwana ucio ekuhangaika, nayo thirikari yugage ni kumaramara na niguthina.

**Translator:** Hao vijana wanataka kujenga mji, na kawaida, kijana akitaka kujenga mji, baba yake huwa anamsaidia kupata bibi, sasa ningeonelea hao vijana wasidiwe, ili wajirufaishe.

**Wambui:** Uguo niguo woni wakwa wa vijana, na nigetha, waganu uthire Kenya, mambe thirikari yambe inyite uhoro wa ciana icio kuma miaka 14, ciambe icaririo uria ciguikara, na njira iria yagiriire. Undu uria ungi ngwendaga gucoka kuga, ni atumia aya akuru, rika ria kuma miaka mirongo mugwaja, niangi muno na guku kianda, na andu acio marikia kurwara, matirona mbeca cia guthii thibitari, marakuira o nakuu, makuira nakuu ukaigua nio acio uraigua Wakaburi etwo agateng'era kwi borithi, thii ugire ngari tumutware mortuary, aathii muthigari ucio munene, ekwenda mbeca cia ngari iyo, na ucio wakuwa, ndari kindu o naringi ni ng'aragu ya muraga.

**Translator:** Hawa ndio maoni kuhusu vijana, ningependa sana asaidiwe, nikihusia jambo hilo lingine, ni hawa wamama ambao ni wazee, kuanzia miaka 70, na ambao wengi wako katika kijiji hiki na ambao wana shinda mingi, ambao kama tulivyo aambiwa na mama wakaburi, wanakufa tu kwa sababu ya jaa, na hawana watu wa kuwasaidia,

**Wambui:** Nitugucokeria mutumia ucio wagwitwo Wakaburi ngatho, ni tondu niwe unganagia aria othe makua naguku thiini, aria mataramenyekana kuria mari niwe umenyaga kuria mari, agagitwo agagithii guthumbuka na guku eguthii guteithika,

**Translator:** Ningemshkuru sana huyu Mama Wakaburi, kwa sababu yeye ndiye anahusika sana na hawa wamama, ambao wanapata shinda kule chini, hao wamama wazee, wakifa yeye ndiye anawashuhurikia.

**Wambui:** Nao atumia aya anini, nio metagwo tene kang'ei, ni aingi tondu athuri nimakuite, magatigwo mari oiki kianda giki, matiri mbeca ciaguthii guteng'erania na kaju na guku, maremeirwo ona guku tondu matingiona ona shilingi igana ria guthii guteng' erania na kaju.

**Translator:** Na pia kuna hawa wamama wachanga, ambao kwa kikwetu wanaitwa kang'ei, ambao mabwana zao wengi wamekufa, na wengi wanakufia pale kwa sababu hawana hospitali la kukibishwa katika hospitali za City council,

**Wambui:** Nii ndahoya thirikari, iririkane uhoro ucio wa andu aria athini, mahote guturuta na guku kianda, matuonie handu hangi tungihota guikara, maririkane atumia acio matangiona muhei, ona mangiheo shillingi magano matano magathukume, no mariire matingihota guthii. Matihota kuhaica matatu haria, ati magire manyeni na guku, matihota, makuaga uguo, tukuagira na guku kianda. Nii ndahoa thirikari, ituteithiririe hanini tutige gukua uguo taindo itari bata.

**Translator:** Mimi ningeomba serikali itusaidie tupate mahari pa kwenda, tutoke huku chini, ambapo hata mtu akipatiwa mia

tano, hawezi panda gari kuenda mahari popote, atatumia zile pesa kula, na mbado shinda ziko mingi, wakipata shinda wanagojeka, na wanakufa tu pale pale kwa sababu hawana mahari pa kwenda.

**Commissioner:** Jambo la mwisho mama

**Wambui:** Ni ndanina uria ngugaga.

**Translator:** Amemaliza yale alikuwa anasema.

**Commissioner**: Goja kuna swali mama,

**Commissioner Salome:** Ni thengiu muno mama ni uhoro ucio watuhe mwega, niwatuhi uhoro wa ciana cia anake, no ndunatuhe uhoro wa ciana cia airitu. Mureka atia na ciana cia airitu na mathina mao ni mariku? (Can you translate my question first)

**Translator:** Commissioner anauliza mama, mama ametwambia sana kuhusu shinda za hawa vijana wanaume, lakini hakutwambia shinda za wanawake.

**Wambui:** Shinda cia airitu acio nicikoretwo iri shinda nene muno muno, ni tondu arata ao riu niacio uraigua ngiuga anake, na matiri na wira, riu mathii guthaka nao nakuu ukareherwo mwana, riu mutumia ucio ndireta kang'ei, akomete na ciana icio na haha kianda, itiri githomo, ina haha, ***(laughter)***

**Translator:** Hawa wasichana, nao wana shinda mingi, kwa sababu marafiki zao, ni hao vijana, ambao nimezugumzia, na hao wasichana ambao nimeita kang'ei, wanaenda wanachezacheza na hao vijana marafiki zao, na mwishowe unakuta wametuletea watoto huku. Sasa wamela na huku chini, hawana cha kufanya, Shida tu.

**Wambui:** Riu ndakihoa thirikari yambiririe kumenya uhoro ucio, tondu atumia mena thina muingi muno, na marakuwa o uguo biu biu tondu gutiri mbeca cia gutwara mwana ucio thibitari, na niarwarire, ukona ni gakua,

**Translator:** Sasa naomba serikali iangalie sana hizi shinda za wamama kwa sababu wako na shinda mingi, watoto wanagojeka, wanakufa, na unakuta hakuna la kufanya.

**Commissioner:** Asante sana mama, jiadikishe pale, halafu tumeshkuru kwa maoni yako. ***(interruption)***

**Wambui:** Kia muico nii ndirera thirikari, igerie gutunyitira anaake, mone mawira, mone gwa guikara, na nigetha ona airitu acio mahuruke mone athuri.

**Translator:** La mwisho ningeomba serikali isaidie vijana wetu wapate kazi na ili hao wasichana wasaidike.

**Commissioner:** Thank you very much for your translation. Alice Kalundu,

**Alice Kalundu:** Kwanza nawasalimia nyote, hamjamboni? Jina langu ni kama vile mimesikia, naitwa Alice Kalundu, nikiwa mwalimu katika ujezi wa taifa katika shule ya none formal ama community school, Mimi upande wa kwangu, upande wangu ningeongelea kuhusu, hii none formal schools ama community schools – Watoto wote wale waka hapa katika Dandora, ni wengi sana wale ambao ni chokola, na hawa chokola wamezaliwa na watu ambaye ni sisi wazazi wao ni sisi tuko hapa.

Mwanamme ambaye ako hapa hawezi kuniambia hakuna matoto wake ako hapa, ni wengi watoto wao ni chokola, ata bila kujua, kwa sababu sio lazima, awe wa bibi yako. Sasa ile jambo ningependa serikali iangalie, sana, ni upande wa masomo wa hawa watoto, na nikiingilia sana, city councils, sijui kama hapa kuna mtu wa city council? Nafikiri wako, naona mmoja pande hii. Ni kwamba, ndio tuchukuwe hatua ya kusianzisha, machokola walikuwa wengi sana hapa Dandora, lakini wengi, sasa nikiwa na % kidogo ile tumechukuwa kwa hizo informal schools, wale wamebaki ni 75%, tukiwa na shule more than 300 schools ambao sio za city council within Dandora location, record niko nayo. City concil, wameanza kutuharass zaidi, kwa sababu wanakuja wakiitisha licence ya 15,000/- per year, na hao watoto ambao tunasaidia, mtu hawezi kuraise 300 per month. Kwa hivyo ningeomba serikali, upande huo muangalie city council. Saa hii nikiongea, nikiangalia kuna mwalimu ako pande ile, jana alikuja kwangu kama mtetezi wa watoto, akanionyesha hio barua amepewa 48 hours amefunge hio shule kwa sababu hana licence. Anaonyoshwa certificate ile ya self help, ambayo ndio tuna-register nayo katika community, anakatazwa anaambiwa alete trade licence. Tunashangaa serikali, kama tunafudisha watoto machokola, tuki-rehabritate, ama tuna trade? Can you answer me! Are we trading? We are not trading, when you see me here I would like to stay in a self contained room, but I cannot, because I'm helping the poor, I'n not there to make money. I'm there to help those children not to go back to the streets, but, I'm not allowed by our government especially city council, that one we are going to refuse, even from now. Two weeks ago they came to my school and they were asking me to give them 15,000, I told them, my good friends I'm not trading, I'm helping you your job, this is your job, you are supposed to be having so many schools in this place as you know the population is so big, but you can't, and we cannot allow chokolas to come and start collecting gabbage here. We have to help them, and they were born, they have to get their education, and that's what we are fighting for, and when we are fighting for that we are fighting for the lives of children. I don't know what kind of lives of children the city is fighting for when they are coming to arrest us. The people who are helping them. Infact I wanted you commissioners to write that to them, that they have to help us, we need their support so that we can educate them, we are not doing our job, that is their job, and they have to appreciate.

Second, the other thing is that wasichana, kwa nchi yetu ya Kenya, wasichana wamenyanyaswa sana, especially upande wa inheritance, wakati wana-inherrit mali ile ya baba yao, wasichana wameonewa sana, utaona mtu ni Minister, katika jamii nyingi, sijui zingine kama zingine ziko anje? Ama ni zote ama ni namna gani, lakini kwa wakatu huu tunapigania kw guvu, kwa sababu siwezi kutupwa inje kwa baba yangu, kama sina mahari pakwenda, napigania kwa nguvu nakaa ki-nguvu, lakini watoto wangu labda ni kikufa wanapata shinda, kwa hivyo ningependa, serikali ipitishe kwa hii katiba, mpya ya , kila mtoto mwenye amezaliwa ni mtoto, kama awe ni msichana, awe ni kijana, ako na right ya ku-inherit ile mali baba ako nayo. Natukifanya namna hiyo nafikiri tutapunguza mambo mengi kama umalaya, utaenda upate msichana wa minister anapiga umalaya kwa sababu kwao akienda ndugu zake hawataki kumuona na macho. Anaenda anaambiwa we enda ukaolewe, labda kwenye alienda, alienda akakosa kusikizana na yule bwana anamuoa, amemrudisha kwao, sasa hakuna mahari pakwenda, na ananyimwa haki yake, ndio anaingia pale town na kwenda Frolida, kujitafutia, sasa hapo ndio analeta mtoto ambaye hatakikani, kwa mboma na anapata ukimwi na anakufa. Kwa hivyo sasa hapo, serikali muangalie sana, kwa kutetea upande huo. Asanteni,

**Commissioner:** goja kuna clarification

**Commissioner Salome:** Asante sana Alice Kalundu, na nina furaha kusikia wewe ni mwalimu, kwani tayari, ata sheria yenye iko urithi wa kisawa kati ya watoto wasichana na wavulana, ni vile watu hawajui, hio sheria tayari iko, ata kitabu kizuri kinasema, watu wangu hunyanyaswa kwa nini? Kwa kutojua, sasa sisi pia tunanyanyaswa

**Alice:** Ningeomba pia, basi kama iko, ifundishwe kwa kila mtoto ndio aweze kujua haki yake.
Commisisoner: Asante sana Alice kwa maoni yako, tumeshukuru, jiandikishe pale, Peter Omuega,

**Peter Omwega Okabira:** Hamjambo commissioners, na wanaDandora? Mimi ni maoni lakini ni kama malalamiko, majina yangu ni Peter Omwega Okabira. Maoni yangu, kwanza ni kama malalamiko kwa sababu, serikali yetu sijui ni kushindwa ama ni kuchoka, lakini unajua hata mzee akichoka sana, ni mambo mengi yanampitia bila kujua ni nini anafanya, sababu ni hii, mimi nimeona, wakati wa Kenyatta, wakati Masinde Mulilo alipiga kula na wambunge akiwa minister, aliondolewa waziri, sababu yeye ni wa serikali na amepiga kula na wambunge. Nikaona wakati mwingine, wakati wa Dr. Onyonka, Dr. Onyonka, alikuwa suspected ameua, alisimamishwa kazi, akafanya kesi, aliposhinda kesi, ndio akarudi tena akateuliwa kama Minister, lakini serikali yetu ninashindwa, imekuwa namna gani kwa sababu unaona mtu ni waziri, na ako na kesi kotini amezingiziwa, na anaendelea kuwa kwa serikali tu, anaendelea kuchukuwa wazi kuwa mkumbwa wa serikali, Hiyo ni ajabu, hiyo ni malalamiko, sababu tukilia corruption, corruption hii iko kwa serikali, ata XXX ya Office of the President, kwa sababu President ndiye huappoint ministers.

Ingine, ningeomba, hii katiba ambaye sasa tunashuhurukia, ningetaka ata AG awe anachaguliwa, sio appointee wa selikali, sababu atafanya vile President anataka. Kama President ndiye amemchagua, si atafanya kazi yake? Atafanya ya laiya? Pia hata ministers ningetaka wawe na wambunge kama inawezekana, sababu, hawa wote, ambao ni ministers wanakuwa appointed na President, watafanya kazi ya muajiri wao sababu, hawataona makosa, ata wakifanya nini, mwaajiri wao tu ndio anawajibika, ndio wanajibikika, lakini sio kwa laiya. Kama wangalikuwa wanachaguliwa na laiya, ingekuwa ni kazi rahisi kwa sababu, mtu anajua akikosea anajua hawezi rudi tena. Sasa sababu wanachaguliwa, wanateuliwa na President, inakuwa mtu anafanya vitu zake, ata sio ile anafanyia laiya.

Ingine, hii serikali mimi na shindwa, sababu ni serikali yetu na imeshindwa kwa sababu, hata usalama wenyewe hakuna, especially area ya Dandora. Sijui kama police wale wako hapa ni wakufanya biashara, ama ni wakulinda maisha ya laiya, kwa sababu Dandora, hakuna usalama, kabisa kabisa kabisa, unaweza nyang'anyiwa hapa, hata saa ingine unaweza toka kwako kwa nyumba na urudishwe sasa tuende tukachukue mali kwako. Na serikali yetu iko, tumewahi kulalamika, tumefanya nini, tunalia usalama na ni kama (sio Dandora pekee, ni area zote), sababu Nairobi mzima sasa hakuna mahari iko usalama. Mimi na shidwa, hata huko nyumbani marisaf, pia imekuwa hivyo. Tungetaka katiba ile ambayoinatengenezwa sasa, sana sana iangalie usalama kwa mwananchi, izingatie usalama kabisa sababu, usalama umekosekana Kenya mzima, sio Nairobi pekee yake, ni Kenya mzima tuko na shinda ya usalama.

Ingine, hawa watoto machokola, hawa watoto machokola ni watoto wetu, hatuwezi watupa, na sisi, tunatoa husuru kwa serikali ilioko, kwa nini hii serkali haiwezi kuwatafutia rescue centers na iwaandikie waalimu, na iwalinde kwa sababu tunatoa kodi, hata hawa siku kidogo, hata pia hao wanatoa koti sababu wanafaa, wanakula, pia hawa ni kama wanatoa husuru. Serikali haiwezi kuwatafutia rehabilitation centers? Au rescue centers wakae huko waondoke kwa mastreets, hiyo naomba tafadhali, muandike hiyo na msema watu wa Dandora kitu wanalia sana, ni hawa watoto watafutie rescue centers na wafanye nini? Wakae huko. Ndio hao nao wawe laiya wema. Nikimalizia, yale mambo mmesema, mtoto ni mtoto, kusema kweli mtoto ni mtoto, hakuna mtoto wa kiume na wakike wakati huu, sababu mmeona, siku hizi hata wasichana wetu hawaolewi. Msichani anaweza olewa siku mbili, siku ingine ako kwako, sasa wewe utamtupa? Ataenda wapi? Hiyo pia, ningependekeza, kama ni uridhi wa mali wapewe haki sawa na wale wafulana. Yangu ni hayo tu, Asanteni.

**Commisisoner:** Asante sana bwana Okabira, jiandikishe pale. Teresa Akinyi, Teresa Akinyi, Akinyi, ameenda, Patrick Wachira,

**Patrick Wachira:** Habari zenu nyote, mimi naitwa Patrick Wachira, na jambo la kwanza lile ningetaka kuuliza hii commission, ni ya , next time mkija hapa ama mkienda area zingine, mkuje na mahema mingi, kwa sababu tumechomeka na jua huko mpaka mambo ile tulikuwa nayo imepotea, kwa hivyo, ama tuko na social halls nyingi sana hapa, hazitumiwi, wale waliorganize tukutane hapa, mngeongea na hawa commissioners tukutane kwa social halls dio atleast watu wawe comfortable. Kwa hivyo next time pahari mtaenda, mjaribu. Sasa mimi langu la kwanza, la kwanza ni kuongea mambo ya katiba, vile mmesikia na vile nimesikia wananchi hapa wakiongea, yenyewe hatuelewi mambo ya katiba kabisa, hata mi nikiwa mmoja wao. Siku hizi ndio najaribu kuisomasoma kidogo na vile imeandikwa na hii lugha ya ma-lawyers na nini, huwezi elewa kabisa, kwa hivo ningeonelea, kama kunaweza badirika, watu waitwe mahari kama Uhuru Park wawe wanafundishwa, wafundishwe kama wiki mbili mfururisho, katiba tunataka kubadirisha namna gani na inakaa namna gani, lakini sasa tukija hapa, Dandora tuko watu wengi sana, wengi, mlisikia Honourable Mwenje akisema, wale registred voters ni 186,000 kwa hii constituency yote, lakini tuko wengi zaidi ya hapo. Mpange mpango mzuri, hawa ni watu wachache sana, ni wachache lakini pia wanaweza represent hao wengine, kwa hivyo mjaribu watu wafundishwe kabisa wapelekwe huko Uhuru Park ama Nyayo Standium, ama Kasarani, wafundishwe kabisa, halafu tuendelee, because, ata sasa wakati uchaguzi ukifika, inaweza kuwa hatutakuwa mmemaliza hii mambo yenu ya kubadirisha katiba. Lakini ningeomba tu pia, tufanye uchaguzi, ata haitakuwa imeisha, tuendelee na uchaguzi.

Lile jambo lingine ningetaka kuongea juu yake, ni mambo ya hawa watu inasemekana ni above the law, sisemi mambo ya Head of State, sisemi mambo ya nani, nasema mambo ya watu wale wako above the law, hata ministers, hakuna minister hata mmoja ushawai kusikia amekuwa accused halafu akafungwa ama amepoteza kazi yake, baado hio mambo tunataka tumalize kabisa.

Jambo lile lingine, ni mambo ya elections, term ya mtu ikiisha, hata kama wewe ni minister ama wewe ni councilor ama ni nani, ikiisha imeisha, mambo ya kurundi tena, hakuna, hio miaka tana, kama itakuwa tano, hata katiba ikibadirishwa, kama hujafanyia

wananchi kitu, sasa wewe kaa kando, patia wengine nafa? Nafasi. Mnasikia akina mama wakilia hapa vile huku kuko kubaya, yenyewe kuko kubaya, na sio kitu ingine, ni kwa sababu ya kupatia viongozi kazi, ile hawawezi. Mambo ingine ya election ningetaka kusema, hata kama ni MP ama ni councilors, akisha-defect, kutoka kwa ile chama alikuwa, ati kwa sababu ndio aende KANU ama aende DP ama aende Safina, hakuna haja ya yeye, ama serikali, iende kwa By-election, kuna yule mtu yule alikuwa No. 2 yake, serikali inaspend alot of money, ma-millions kuwa na By-elections, ambayo ile pesa ingekuja isaidie wamama kama hawa wanalia hapa chini, na hio ni mbaya, kwa hivyo ningeomba hizo by-elections ziishe kabisa.

Tena ile ingine ningetaka kuongea, ni mambo ya hawa MPs wako, ama wale wakubwa wakubwa wako, kuna pesa ikifika wakati wa elections, wanapewa pesa kiasi fulani, ati ndio wakuje wafanye campaign, hizo pesa ndizo zinaharibu watu hapa, na wana-forcewa ku-elect the wrong people. Wewe ukiwa hujaenda kwa hio, wewe sio MP, naunataka kusimama kwa hiyo kiti, huna hiyo pesa, wale unaona wakizunguka huko usiku, wakiwapatia mablanket, sukari, nini, halafu, hio ni kununua vote yako, kwa hivyo hio pesa wanapatiwa ya kuja kufanya macampaign hapa, iishe, mtu atumie akili yake ya kutafuta votes, sio kununua, na mimi nataka kuwasihi wananchi wenzangu Dandora, mimi nimeishi hapa Dandora miaka mingi, ikifika hio wakati, mtakuwa na shinda mingi sana, kwa sababu security ya hapa na imetajwa mara mingi, iko mbaya kabisa, mkitaka kutembea usiku, nyinyi ndio mtaumia, kwa sababu hakuna security. Kwa hivyo nawasihi, msikubari votes zenu kununuliwa usiku, kujeni mchana kama hapa, watu wanaongea halafu wanatembea vile wanatembea.

Lile jambo lingine, ni mamba ya voters, voters ningeuliza wale wanapeana hizi voting cards, ziwe zinapeanwa kila wakati tunaendelea, zile nazo, zinabadirishwa, zile zitabadirishwa kama mimi sitaki kuchaguliana Nyeri, ama sitaki kuchaguliana Embakasi, kule ninaenda yangu kama nimebadirishiwa, ichomwe hapo hapo, kwa sababu kama haitachomwa hapo hapo, hizi ndizo zitakuja kufanya rigging na mtachagua viogozi wale hampendi, kwa sababu ya votes zenu mliwaachia, na wakati mliwaachia, zitawekwa kwa mabox zingine halafu ziharibu wale viogozi mnataka. Sithani ni jambo la mwisho kwa sababu mimi sikuwa na kuja hapa kuwa na siasa ama nini, ni ya , mambo ya President, ama wale watakuwa Heads of State, hakuna haja ya kuwa na Head of State, na yule mtu ako kwa opposition ama kwa nini ndiye atakuwa ati Leader of the opposition, hapana, huyo leader of the opposition, pia awe anapewa powers kama za President, ndio at least anatetea watu wa oppostion vile inatakikana, kama ni mambo imekuja, inatakikana, wakae chini hao wawili, lakini sio mtu mmoja anakaa kivyake na katibu yake. Kwa hivyo mimi sina mengi, ni kuwajurisha tu ya , tutume commission hii ijaribu kuangalia mambo yetu, ya katiba, na ndio tuwe na serikali ile ambayo itatuongoza na njia ilie iko sawa sawa, na hiyo maneno yote umesikia hapa mashinda, mashinda, mashinda, sio kitu ingine imeleta hizo shinda, ni sisi wenyewe tu tunajiletea, kwa sababu ya kuchagua viongozi hawajui mashinda na maneno ya vile wananchi wanatakiwa kukaaa. Asanteni.

**Commissioner:** Asante bwana Wachira kwa maoni yako, tumeshukuru, hatuna swali, jiadikishe pale. Lamek Osieko, Romano Miriku utamfuata,

**Lamek Osieko**: Kwa majina naitwa Lamek Osieko, ni mkaaji wa Dandora, yaale ambayo nataka kuzungumza kwanza ni

hali ya security, kwa nchi hii, hii kwa sababu ile number ya police ni chache mno, na wananchi ni wengi, kwa sababu kama 30 million, na police hawafiki ata 100,000, hiyo haiwezekani. Sasa lazima tuaanze community policy, ambayo wale vijana wetu ambao hawana kazi pia, serikali ifanye budget yao, na wasaidiane na police kwa areas ambayo wanatabuliwa na wazee wa area hiyo, under the chairmanship ya chief, na wawe vetted, na wawe na certificate of good conduct, sasa wasidie police kazi baada ya kutenguliwa, ndio hali ya hiyo insecurity, itaendelea, lakini kama bado, police ni chache mno, na vivaa pia lazima wapate zile zakufanya kazi, kwa sababu wamekuwa more advanced na wako na sophiscated weapons kuliko ata ya police, na magari pia za police, ziwe ambayo zinaweza kufanya kazi, sio kama ya mahindra ambayo mtu anapata pesa kidogo, ama apate rafiki yake amuuzie ili apate commission, na gari ambazo zinaenda na police, sio faster at kuchase zile za wezi,

Ya pili ni, Health care programme, Kenya inafaa kuwa na Health Care Programme kama nchi kama za America ambayo watu wanachangia kwa sababu hii NHIF, wale ambao hawafanyi kazi, hawawezi kuchangia, sasa unaweza kugojeka, nahuna pesa, lakini serikali, kati ya ile ushuru watu hutoa wakinunua bidhaa, iwe sehemu furani iwekwe, itengwe, kusaindia wananchi ikiwa wanaungua, na hio cost sharing pia nina-disagree nayo, na wawe na health care programme kwa wananchi wote.

Pia kuna flood management, na ni haibu sana kama haka kama capital city kama Nairobi, at watu wameenda na maji. Na kwa sababu serikali haina flood management programme, ambayo inaweza kurudisha hali kama hizi, ziepuke nayo.

Gabbage management, serikali haina mipanga ya gabbage management kwa nchi hii, ndio takataka inaweza tupwa mahari popote, for example, hapa Dandora population iko juu zaidi na unaona they are living with the gabbage, na unajua diseases kama cholela outbreak, inaweza kuwa XX wakati wowote, kwa sababu gani? Watu wanaishi na taka, na serikali haina programme ya gabbage management. Kama unaweza fanya recycling, na wawe na gabbage management programme, hii ukabira watu wanaita ni shinda kubwa, mimi naona ni wale viongozi wenyewe ndio wanaanzisha. So tuwe kama nchi ya Tanzania, ambaye Mwalimu Nyelele alikuwa ametilia manane sana ya unity ya nation, kwa sababu, from the ministers, kwenda chini, hata kwa President, utaona driver ni kabira yako, turnboy ni kabira yako, security yako ni kabira yako, hio inamaanisha una imani tu na kabira yako. It should be, if I'n a luo, my driver should be a kikuyu, my secretary should be a kamba, ione pia ita-improve ile lugha nitaongea kwa office, itakuwa ni lugha ya kitaifa, kwa sababu sitakuwa na nafasi ya kuonge lugha yangu, that one will promote national unity.

Maneno ya President kupata 25% kwa kila province, hio si haki, President ipate 50% kwa upigaji kula wote, na awe President, lakini sio 25%, sababu kuna areas zingine, huwezi pata hio 25 % sababu ya hii ukabira, sasa ikiwekwa 50% itakuwa wewe umewakilisha nchi nzima ilivyo.

Death penalty, hii hali ya kukumu watu kunyongwa, si haki, hivi majuzi tuliona kisilu alitolewa gerezani, ati alishitakiwa pia wakati mwingine kuua Gama Pinto, pengine wewe hukutenda hio jambo, lakini tayari utakuwa umenyonywa, na hukutenda hio, sasa iwe wa-replace na life imprisonment, kwa sababu, hata ukichukua muda gani ukweli inaweza patikana na unaweza

kuaachiliwa huru. Lakini ukinyongwa halafu, baadaye ukweli upatikane, na wewe tayari ulikuwa umenyongwa, hio sio haki. Iwe life imprisonment instead of dead penalty.

Watoto ambao wamezaliwa na wakenya, hata kama ni nje, ama dani ya Kenya awe automatically citizen wa Kenya, isiwe in shinda, hata kama umezaa ata kama uko wapi, uwe automatically watoto wako ni wanakenya.

Military programme, iwe wanajezi badala ya kungojea vita ama kutufanyia practice kuonyesha technics yae wakati wa national holidays, hio tunaona inapotesa lasiri mali ya nchi. Kama tuko na disasters kama hii El-nino rains, wapewe jukumu waanze ata wajenge mabarabara sababu wako na hizo vifaa, wanajeshi wetu wasiwe wanaishi tu msituni, kuna wakati wanazeeka bila ata kufanya kazi yeyote, wakigojea vita. Kati yetu, uhusiano wetu na neighbouring countries ni nzuri mno, sioni dariri ya tutaenda vitani, so badala ya hao kukaa msituni, wakuje wafanye zile kazi za mikono ambayo inaweza kusaidia nchi, na itagenerate resources for this nation. Sasa mimi naona warundi huku saa zingine, wasi-retae kama hawajaenda vitani, kwa sababu hakuna vita.

Judges should retire at the age of 60, hii baada ya kuweka judge kwa sababu kwa wakati huu judges wanakaa mpaka 74 years. Hio lazima uchanganyikiwe, sababu hata wazazi tuko nao, ukishakuwa zaidi ya 70 years, lazima uchanganyikiwe. Sasa kama ni huyu ndiye mtu ambao atakuwa anatoa uamuzi, sioni kama hii umri ni mzuri kwa judges. Walitae at the age of 60, not 74 kama ilivyo sasa. Nchi hii ukishikwa, unasemekana , wewe sheria inasema “you are not guilty until proved guilty”, lakini tayari umeingia cell, umefungwa, baado unagojea kufungwa, unangojea case yako. Tayari umewekwa dani, mimi naona huwezi semekana you are not guilty until proven guilty, uwe you are “guilty until proven not guilty”, iwe kinyume ya hio, kwa sababu, tayari umeingishwa dani, umepigwa, and “you are not guilty”, mtu ambaye si not guilty, hawezi akawekwa cell, so hio nataka ilekebishwe.

Number ya wizala, zipunguzwe, iwe , kama ni 15 na haionekane hio ni 15, si wizara ya maji ni tofauti na environment, energy, tofauti, hapana, iwe trimed, sababu expenditure ya serikali inaenda mingi kwa sababu ya hizi ministries mingi, so number ya ministries ziwe reduced, karibu ataanzishwa very soon ministry of none living things ambayo haitatusaidia. Ministers na ambassadors, ama heads of parastatals, lazima wawe vetted na parliament, President anaweza, only kupropose, lakini ni wale wabunge watamhoji huyu mtu kama alikuwa na record mbaya, ama anaweza fanya hio kazi. Ndio wa ta endorse, badala ya mtu tutolew kichakani na awe waziri, hio exactment yake kuwa waziri na hajakuwa nini, kitabo asettle down, miaka tatu imeisha, kwa sababu bado hajaamini yeye ni waziri. Labda alikuwa balozi nchi fulani, ama yeye alikuwa ni mkuu wa jeshi, sasa sijui ni diplomacy gani anaweza fanya na hajawai kufanya public relations. Sasa hio naona lazima iwe vetted ni mtu gani huyu anateuliwa, kwa sababu watu ni wengi. Yangu ni hayo. Asanteni.

**Commissioner:** Asante bwana Osieko, hata karibu nikuambie maliza, lakini asante umeniangalia akili ukamaliza, nimeshukuru. Osieko kuna swali, goja kidogo,

**Commisisoner Salome:** Asante bwana Osieko, umesema kuwa watoto wanaozaliwa na wakenya, wawe ni laiya wa Kenya popote pale walivyozaliwa, hata katiba ya leo dio vile inasema, ile pahari penye huwa na swala ni kuwa, mtoto anayezaliwa na mwanmme mkenya popote pale, huyo mto to ni mkenya, lakini anayezaliwa na mama mkenya akiwa wamezaa na mtu asiye mkenya, sasa huyo mtoto hapatiwi ulaiya wa Kenya. Sasa hapo maoni yako ingekua vipi?

**Osieko:** Mimi nitaona huyo mtoto awe tu mkenya, kwa sababu hata America, ukioa msichana wa America, na umekuja naye hapa, America wata kuregard kama mmoja wao. So mtu ambaye ako na mtu wenu huyo ni mtu wenu kwa sababu damu yenu iko hapo. Asanteni,

**Commissioner:** Asante bwana Osieko nimeshukuru kwa maoni yako, ningependa kumwita Richard Mwangi, sorry nilikuwa na muita Romano, Romano, pole, pole, halafu Richard atamfuata,

**Romano K. mitiku:** Kwa majina kamili ninaitwa Romano K. mitiku. Yangu ya ni kushuruku kila mmoja wetu ambaye ako hapa, mkubwa kwa mdogo. Kwanza kwa katiba yetu, tungependa kupendekeza ya , kwa sababu tuko na wakenya wamehitimu kwa elimu, na kila siku, na wengi wetu ambaye hawana kazi, ningependekeza ya , katiba yetu, iruhusu zile kazi ambaye specified kuwe kila mmoja wetu, tuseme ni one man one job, kwa sababu unaona, kwa makazi mengine, mtu mmoja unaona anapokea karibu cheque ishilini kwa mwezi mmoja wakati wengi wetu ambaye wamehitimu, ata dururu hawana kw mfuko na wako na uwezo wakufanya kazi. Ndio unaona kazi miingi sana zinakutwa zimeharibika kwa sababu huyo mtu ako overburdened, hawezi kufany kazi effectively kwa sababu kazi ni mingi ile amepewa na hafanyi, na hataki kuaachilia kwa sababu nia yake ni mshahara, lakini si kutumikia wakenya wetu, si kutumikia wananchi wa nchi hii.

Ile ingine ningependekeza ya , katika city yeyote, mayor awe anachaguliwa na wananchi na asiwe ako kwa ward yeyote, achaguliwe na wananchi ili awatumikie wote vilivyo, asiwe anasema mimi ni lazima nitumikie ward yangu ili wakati mwingine nipate kula.

Ya tatu ni ya , mimi sioni ni kwa nini watu wengi wa nchi hii kwa sasa ambaye wako na thousands of acres of land (idle) na wengine hapa hawana chochote, hata mahari pakulala hawana, wengine wanalala kwa barabara. Ningependekeza ya wale wanataka hiyo mashamba, wawe taxed, kwa every acre of this piece of land lies idle, hiyo pesa itumike kusomesa watoto wetu ambaye hawasomi kwa sababu ya kukosa kalo. Ningependekeza , elimu kutoka nursey school mpaka university nchi hii iwe free, hiyo itatusaidia kwa sababu hata hii mashinda unasikia tuko nayo hapa na pale, ya watoto wetu ambaye tunaita chokola, haitakuweko, kwa sababu tutakuwa tayari tumepata a source of income. Hawa watu wanaweka mashamba kubwa na mna hiyo, wako na ingine ya kuweka na ya kutumia, basi, hiyo in upande wa free education. Kwa idle land nayo tumesema ipewe nini? Tax – kwa kila acre ambayo iko idle. Base constitution yetu, serikali nayo ione mahari ambaye iko idle land, ambaye inaweza kufanyiwa irrigation, irrigation ikifanywa, hata kama ni tuseme ni sukuma wiki, itakuwa infuu na kila mmoja ako area,

atakuwa ana-afford. Sasa kwa saa hii nina ongea, nyaya moja ni karibu shilling kumi ambayo tungekuwa tunanua hata shilingi moja, ama sumuni, tuko na shamba kubwa sana ambayo ni idle, tukitumia lake Victoria hapa maji iende ukambani, chakula hapa hatutamaliza, hata ingine tutaweza kuuza nje.

Ile ingine ni ya , Head of state, yeyote yule atakuweko, kuwe na restrictions zile ziko na xxxx zile haziko na maana kwa sababu ya kutumia pesa ya tax payers, ati ni ya liberty, na hiyo pesa ndio ingetumika mahali ambao unasikia iko watu hospitali, wengine watu wetu wanakufa, wamekosa pesa ya dawa, hawapati, kwa sababu ya mismanagement of our resources. Ile ingine ni ya , kwa upande wa maji, maji ni uhai, na maji ikiwa uhai, ningependekeza ya katiba yetu mpya ambaye tunaangalia iaandikwe, mtu ambaye yule amewekewa kama ni mita, alipishwe mara moja, lakini hiyo ingine, wananchi wawe wanapewa maji free. Na mahari iko social areas mahari kama kijiji kama hii, kuwe na water points, ambayo wataweza kuwa wana chota maji communal. Tuwe communal, kwa sababu wengi hapa wanakufa juu ya kukosa juu ya kukosa hata chakula, anaweza kuwa na chakula, lakini hana shilling tano ya kununua maji mtungi moja, na maji ingine mnasikia inakuwa mismanaged, ingine inamwagika kwa barabara hakun mtu hapa anaangalia.

Ile ingine nayo ni hii ya voter registration, voter registaration iwe continuous, kwa sababu kila siku, mkenya anafikisha miaka 18, si rush hour, endeni mkafanya registration, wengi wetu hawako serious na maisha yao hapa, tukiona mlolongo ni kubwa, hatuwezi tukaenda kupanga laini mpaka asubuhi, ukiona tukijipeana mpaka kama saa zile tunachomwa na jua huko, tangu asubuhi ni kwa sababu, tuko na uchungu ya yale ambaye yametupata. Kwa hivyo voter registration, iwe continuous exercise.
Ile ingine ni hii ya kwamba, tuko na provident fund, ya wale watu ambaye walikuwa wakifanya kazi. Ningependa kupendekeza ya , kama ni NSSF, kwa sababu life is bad, ya wakenya and generally in the world is reducing. Hio 55 years, ni mingi sana kwa sababu wetu hata hawafikii hapo, wengi wetu wanawachishwa kazi ata wakiwa na miaka 30. Sasa unaambiwa wewe enda ukaungojee miaka 55 ufike ndio utapewa pesa yako. Ningependekeza ya , wakati mtu anapewa barua mahari alikuwa anafanya kazi, kama anataka kwenda kufanya kazi yake, saa ile imepata retirement letter, ama amekuwa retrenched, alipwe pesa yake akafanye kakazi kake hata kama ni ya kuuza sukuma wiki aishi na watoto wake. Kwa hayo machache, commissioners wetu, nimeshukuru sana kwa sababu ya kutupatia nafasi hii, asanteni.

**Commissioner:** Asante sana bwana Mitiku, you were very clear, ende ujiandikishe pale. Richard Mwangi, halafu John Macharia, John Wachira,

**Richard Mwangi:** Macommissioners, na wananchi wa Dandora, habari zenu? Kwa jina naitwa Mwangi Cucu, na mimi pia ni mkaaji wa hapa Dandora, na nimefurahia kwa vile tumeweza kupata macommissioners leo, isipokuwa hatukuweza kupata nafasi, ama hawakuweza kututangazia, hapo kitabo watakuja hapa, wengine wamejua hivi karibuni wanakuja na hatukuweza kuwa na mpango tutaweza kupresent our views, lakini nimefurahia kwa sababu hiyo tumekuwa nayo, na mambo ya katiba, ni kitu ambacho tunajua ni kitu inakuhusu ukiwa mwananchi wa kawaida. Nikiongea upande wa katiba, vile ningepropose, upande wangu, tuko na hii kitu tunasema inaitwa Presidential Power, tunajua President mwenyewe, sisi laiya hatujajua tofauti ya

the President Decree ama directive ama kisheria, tuchukue mfano, ata kama ni President akikuja hapa aseme hii jia ifungwe, hatutaweza kujua tofauti ni sheria, ama ni directive ametumia, kwa hivyo, tungetaka katiba, hata kama ni sheria imebadirishwa, tujue imebadirishwa na jia gani, hiyo ni maneno tunataka na tunasikilia inafaa kubadirishwa.

Ile maneno ingine, maoni yangu ningesema, ni upande wa distribution of our resources, Tukichukua mfano, tunajua kuna watu wanapata hata mshahara wa million moja, kuna mwingine hapati hata dururu, na tukiangalia hapa, world bank vile wanasema mambo ya poverty, unapata majority of 70% of our population, ni mtu hawezi afford 80 shillings per day, na ukiangalia 80 shillings per day, hiyo ni pesa hata haiwezi mwenyewe kukulisha, hata lunch yenyewe haiwezi tosheka, na ndio unaona mambo ya insecurity inatokea sababu wachache ndio wanapata, national cake inakuwa shared by few, natunataka atleast, yule anapata one million, aweze akagalao apate elfu mia moja, the rest nine hundred iweze kuajiri vijana wengine. Kwa hivyo ningepropose namna hiyo, mambo ya revenue na mambo ya tax, tuko na campuni ambayo tunajua, kampuni tukitaka tujue kama inaenda hasara ama faida, wanatupatia hesabu, sisi hatujawai kuona serikali yetu inatupatia hesabu. Hatujajua kama wanaenda hasara, ama wanaenda faida, na juzi ndio mlisikia ati kwa hasina yetu hatuna chochote, na ndio mnaona uchumu imepolomoka, hata hatukuwa tikijua, lakini kama tungekuwa tunapangiwa hesabu, tungeona ya , from 199fulani, kuna mpango, na hata kama ni uchumi unaanguka, unaona unaanguka na jia gani, hata investors wale waliona kwa gazeti juzi, mliona kama ni investors wale wanakuja Kenya, ni wachache sana. Kwa hivyo mambo ya investment kama hakuna, kwa nchi, ndio mnapata kuna shinda. Kwa hivyo, tungetaka, upanda wa parking, tujue, serikali inachukua kiwango gani? Inapata kodi kiasi gani, na inatuambia kwa barabara, tumembakia kiasi hii, imembakia hii, na hii ingine tutapeleka upande huyo mwingine. Kwa hivyo, upande wa kodi, tungepropose wawe wanatupatia vizuri. Pia, ningepropose upande wa hawa wananchi walikuwa hapa wanalalamika wanasema mambo ya choo, mambo ya shinda, Embakasi ni pahari iko shinda. Mambo ya squarters na kadhalika, na ningepropose, hawa wananchi wanasema wanataka wasidiwe, hiyo ni mambo tunajua our government, ikienda kwa paper work, inafanya vizuri sana, lakini kuimplement, inakuwa ni shinda sana. Tunataka wawe na ile kodi sijui tunaiita orbseman, ambaye tukiweka pale, kama ni huyu mama alikuwa anasema serikali, hata akienda kwa Kinyago, ama anaenda wapi, anaenda kupigia yule anamwambia shinda yake, sababu hata saa hii ukienda kwa serikali uwaambie tuko na hiyo shinda hawawezi jua, lakini tukakuwa na hio kodi, tutakuwa na that body, tunajua ya , wewe unasema hivi, na ulisema kwa munda gani, kama choo huwezi kaa miaka 5 bila choo, angekuwa tunajua from the 5 years imeenda, na alikuwa amesema, wametufanyia nini. Kwa hivyo, hiyo mambo ningependekeza, upande wa judiciary, wa leo hata mtu asikuthulumu, hata siku hizi unasikia hata mtoto wa lawyer, or prominent person, anakuambia, ukiniguza unajua mimi ni mto wa fulani, sababu, wa leo ukitaka ku-hire a lawyer, of which tunajua, (mimi nimekuwa nime-hire a lawyer very recently, mimi ni chairman self help group fulani, na nilishtuka kupata a lawyer, huwezi pata lawyer na shilingi mbili) lawyer unampata na over 20,000, na pengine hata ni kitu kidogo sana. Natungeuliza, kama ni serikali, iwe inatusaidia, na tuwe na community courts, hiyo community court, hata kama ni mtu alikupiga kofi, tutapata pahari pakwenda kusingizana. Na community court, ina urgue without any lawyer, na after urgument, wanakuja na that conclusion wanasema, yenyewe, niliona makosa iko kwa fulani. Hapa ukichukua mfano hapa Dandora, leo sijaona wakubwa wale wanatusimamia pale, isipokuwa laiya wa kawaida akiongea na anaangalia kado asiulizwe jioni kwa nini ulisema hivyo. Tuko na haki ya kusema hivo, tukienda pale police, yetu iko hapa post, tunajua kawaida kuna ile pesa wanawashangia

ama wanawapatia, wawe wanasimamia post kama hiyo, tuseme hata mnaweza shikwa, na ukishikwa jioni, hakuna vile unaweza patiwa chakula huko, na tunajua atleast kuna pesa ile wanategewa pale na serikali, inabidi, kama ni mtu wenu aende akuletee chakula pale, ni kwa nini? Na incase kama mtu wenu hayuko karibu? Inaonekana hata anaweza kufia kwa? Kwa cell. Tunataka tujue, kama ni police, wanapatiwa kiasi ya pesa, na ukifika pale uko na haki ya kujua, ni kwa nini mimi sijapatiwa mafasi ya kukula, kwa hivyo, upande wa police pia, ningesema hata kama ni statement, kabla hujaandika statement, tunaenda through toture, na unpata mtu ana confess kwa sababu ameteswa kwa munda. Ningeonelea hapa serikali, tuwe na yule mtu anafaa, ama awe ni representative wameteuliwa na watu wa kanisa ama community. In case unaandika statement pale, unaandika, usiandike kwa sababu wewe umekuwa totured, unaandika kwa vile wewe unajua maneno iko hivi, naunatoa maoni, ama unaandikisha statement kulingana na vile na unajua. Lakini wa leo tunajua, ukishikwa, unakuwa totured, na unaconfess ile mambo haitakikani. Nikiongea mambo ya environment, pia sisi wakaaji tuko na haki ya kujua environment itatunzwa namna gani, tukiangalia hii dumping site, yenyewe, inacreate jobs upande mwingine, lakini hatujui hii dumping site ililetwa pale, ni sisi tuliipata hapa ama ilitupata pale? Ikikuja, tulikuwa tumeulizwa ikuje pale ama walikuwa na uwezo gani wa kudump pale? XXX watu wakisema mambo ya dumping site, Tunajua wale watoto wetu wanazaliwa hapa, hata niko na furaha kwa sababu, hata kama hatujakuwa kusema ati tulalamike, isipokuwa ni maoni yetu. Kama at least ata mngetokea 41 muangalie pale, nyinyi macommissiners mungenjiwa yenyewe Dandora, watu wanaisi kwa Mungu, hata wengine wamenono sababu ya kubreath ile hewa mbaya iko pale, sio ati kwa sababu ya afya. Watoto wengi wetu wanazaliwa pale wakiwa kipofu, hata the breathing ile ukibreath pale, yenyewe unapata hapa kuna shinda. Na ukiamka asubuhi, ndio unasindwa, Kenya tukiangalia ata ninichukua mfano nikifika nyahururu, yule mtu wa North Eastern, kutoka huko, akifika Nyahururu amesema amefika Kenya. Sisi hatuonangi Dandora kama tuko Nairobi, hata hatujuangi kama tuko na any municipality ambaye inatusimamia upande wa kiserikali, Kwa hivyo hapo ningeomba, kama ni mambo ya environment, tungejua na tuko na haki ya kujua. Nafikilia nataka kumalizia kidogo, upande wa land distribution, nafikiria kuna mwingine aliongea dakika mbili isipokuwa unipatie tu dakika moja. Nikiongea mambo ya land distribution, tunapata ya hapa Dandora tunasema mambo ya watoto na shule na kadhalika, lakini, ile sehemu tulikuwa tunategewa kado na city council, tuweza kujengea shule zetu baadaye, zote zimekuwa grabbed. Hata mimi nashindwa, tutajenga shule zetu za baadaye wapi? There is no planning, na tunataka hiyo mpango ya planning, iweze kutekelezwa. Nikimaliza tu kwa haraka, ningepropose namna hii, tuna jua mambo ya walee watu wame-root our economy, na sisi tunathania ati yule mwizi mbaye anachukua bastora, anapiga mwingine. Huyo ndiye tunachuki. Hapa tukiongea mambo ya kuroot economy, tunajua watu hawana hakika ama hawajui lini wale wameroot economy watakuja kuchukuliwa hatua, kwa mauni yangi ningepropose, wale wameroot our economy, waweze kurudisha zile vitu wameimba, na wawe executed by public, wanyongwe kiunyama. Asante

**Commissioner:** Asante sana bwana Cucu, jiandikishe lakini sikiza bwana Cucu, usiogope na mtu yeyote asiogope hapa kuona maoni, hakuna mtu atakufuata baadaye, uliambia tume nini, mimi ni mara ya kwanza pengine mnasikia hakuna askari abaye ako hapa, ama chief ama councilor ama MP, atakuuliza umesema nini mbele ya tume, ata kama uko na maswali, na mtu akikuuliza jioni hata kama ni rafiki yako, piga report kwetu na tutachukua hatua. Asante, endelea mzee.

**John Wachira:** Habari zenu nyote? Kwa majina ni John Wachira, ningetaka tu kuchangia maoni ya katiba, maoni yangu ya katiba ni kama ifuatafyo, nineonelea katiba ya sasa tuwe na Prime Minister, Office of the Rais, mamlaka ya Rais yasiw kama vile yalivyo sasa. Mamlaka kutoka kwa Rais yagaiwe office ya Vice President, na vile vile yagaiwe katika ya Prime Minister, Rais atakapochaguliwa, awe Rais wakuhuthulia vikao vyote vya bunge, ili awe akijibu maswali ya wabunge kuhusiana na office yake. Vile vile Vice President awe akihuthulia vikao vyote kama kawaida, na kujibu maswali kuhusu office yake. Prime Minister awe akihuthulia vikao vyote vya bunge, kujibu maoni ya office yake ili sisi tuwe na transpalence na accountabilities from highest office to the lowest. Asanteni.

**Commissioner:** Asante, kuna swali, goja bwana Wachira,

**Commissioner Salome:** Tukimpata Prime Minister ama waziri mkuu, atakuwa ndiye mwenye mkuu wa serikali na yeye kwa kanuni za katiba ndiye mwenye ataenda kwenye bunge, na kujibu maswali, juu ya serikali, sasa umesema tupate President mwenye ataenda kujibu maswali kwenye bunge, na Vice President aende ajibu maswali kwenye bunge, na Waziri Mkuu aende ajibu maswali kwenye bunge.

**Wachira:** Nimesema hivo kwa sababu, ingekuwa ni vizuri kwa sababu tumerahisisha kazi, tumekuwa na kazi Rais kumpata Rais kwa sababu tutakuwa na Vice President na tunaweza kutuma ujube kupitia kwa Vice President, kwa Prime Minister, na ikamfikie Rais, na hivi ikiwa atakuwa na majibu ya kuwika anaweza kufika nakujibu.

**Commissioner:** Asante bwana Wachira, jiandikishe pale, tumeshukuru kwa maoni yako, Asnte, Naomi Wanjiru, Naomi wanjiru, Julius Juma Ong'ang'o, Patrick Irungu, Patrick Irungu, Karibu, Peter Ndirangu yuko, utamfuata.

**Patrick Irungu:** Asante commissioners, na wananchi kwa jumla, majina yangu ni Patrick Irungu Kirugo, naningependa kutoa mapendekezo yangu katika ubadirishaji wa katiba yetu. Mwanzo kabisa, ningetaka kuongea kuhusu serikali yetu, ile ambayo tungetaka kuunda, kwa sababu wakati huu tuko na vyama vingi, ningepropose ya , hata chama ambacho kitashinda, kiweze kuunda serikali ya National Unity ili isilikshe watu wote, hata wale walio wachache kwa sababu wataakilishwa katika bunge.

Jambo la pili, tungeongea mambo ya health ya wananch wa Kenya iwe kila mkenya ambaye amezaliwa Kenya, ako na haki ya kutibiwa bila kuwa na cent lolote, mahari popote, na pia pia upande wa education, tungependelea ikuwe education kutoka nursery mpaka university, ikuwe ni ya bure ili tusiwe na watoto ambao hawasomi, kwa sababu wamekosa pesa ya kalo.

Upande mwingine tungeangalia upande wa kazi, hii nchi yetu hata kama ni security, imekuwa ya juu sana, sana sana imekuwa kwa sababu watu hawana kazi. Tungepropose serikali itafute bill za kupata kazi, kwa vijana sana sana, na hata kama hakuna XXXXX tunajua vizuri nchi yetu ni agricultural country, na kuna nchi ambayo ni semi-desert, ambayo serikali ingeweza ku-utilize kutafuta maji, na kuweza kufanya kama horticultural, na vijana wetu wapate kazi huko.

Ile ingine, tungeangalia upande wa corruption, wale watu ambao wamekuwa katika maoffice ya serikali, na wamekuwa wakilaumiwa kwa ku-root our economy, ingetakikana, hata kama ni nani, achukuliwa hatua kali sana, ambayo ni kama kufingwa maisha, na kuwa hawezi kuhudumia katika office yeyote ya serikali.

Ile ingine, ni kwa upande wa mishahara, na job grouping, katika nchi yetu, kuna job groups, ambazo ziliwekwa, sijui ziliwekwa wakati wa mkoroni ama ziliwekwa wakati gani. Kuna watu ambao wanaitwa jobgroup A, mpaka sijui imefika group E ama G. Kuna wale ambao wanapata mishahara ya juu sana, kama saa hii tunajua kuna mtu anapata mshahara wa million moja, ambapo kuna mwingine anafanya kazi tu kwa serikali, na hawezi pata mshahara ya elfu tatu, kwa hivyo tungetaka, ele gap katika wale masikini na wale wako juu, iwe inakaribiana kidogo.

Ile ingine ni kwa upande wa tax, serikali yetu tunajua inachukua tax kwa kila mkenya, kama ako kazi ama hana kazi, kama ni mgojwa, ama yeye si mgojwa, tungeomba serikali, iweze kuchukuwa kodi, iwe na formular fulani ya kuchukua kodi, kwa wale watu ambao wako kazi, kwa wale watu ambao wako na uwezo. Tungeona, ni vijana sana kuchukua kodi ambaye ni mgojwa, wakati anaenda kununua dawa imewekwa mpaka VAT. Hiyo tungeomba serikali, iondoe koti zingine, kama hizo ambazo zinafinyilia wananchi.

Hiyo ingine, ni kama kwa upande wa mabaraza, kama hii city council ya Nairobi, tungeona ni vizuri, city council kama watakuwa wakichukua kodi, wawe wakitupatia services zile ambazo zinafaa. Kama wakati huu, City Council huku ukikuja kuanza kibada ya kuuza mboga, wanakuitisha licence, ambao pale kuna charges ya dustbin, ambaye hio dustbin huipati, kuna charges ya sewage, na mambo ingine, na mambo ingine, huku sewage zinanungunika mnasikia watu wakilalamika, zile takataka ambazo wanakucharge, wanakulipisha pesa hakuna mtu wa kuchukua, kwa hivyo tungesema, kama watakuwa wakichukua hizo kodi, wawe wakitupatia services zile ambazo zinafaa.

Ile ingine ni kwa serikali, kwa upande wa mawaziri, wale watu ambao wanaminiki maoffice kubwa ya serikali, kama parastatals, na majudges, na watu wengine, hiyo ingekuwa ni mzuri, kama wangekuwa wana-appointiwa na bunge, kwa sababu imeakilisha kila mtu, kutoka kila upande wa nchi. Kwa hivyo tungeona ni mzuri, kwa maana wakati mtu anachaguliwa na mtu binafusi, anaweza kuwa manipulated na huyo mtu kwa njia ya rahisi.

Ile ingine ni kwa upande wa security, isipokuwa watu wameongea sana mambo ya security, kama hapa kwetu, Dandora, na mahari zingine, tunaona hakuna security, kwa sababu, kama ni waizi, wanatembea tu free na wanajulikana na ata wale watu wamewekwa kulinda amani, isipokuwa, unaweza pata kunaimbiwa pale kwa plot, na saa hiyo askali wanasika vijana hapa hati hawana vitaburisho. Hilo tungeomba serikali, kama ni wale police, kama hawana toning ya kuwa na good relationship na public, sana sana waache kutrainiwa sana mambo ya vita, waturainiwe mambo ya sheria na vile watahudimia wananchi. Asanteni.

**Commisisoner:** Asante bwana Irungu, umeeleweka vizuri, jiandikishe, tumeshukuru Peter Ndirangu, Peter macharia, Peter Macharia, Simon Muturi, endelea bwana.

**Peter Ndirangu:** Asante sana tume ya katiba, ningemshukuru sana kwa kuweza kutembelea sisi siku ya leo, na sana sana nitalaumu wale walitayarisha hapa, kwa vile walituleta mwisho wa Dandora, kama mimi nimekaa hapa miaka mingi na sijawahi jua hapa, nilianza kutafuta hapa saa tatu, nimekuja kujua saa taano ati panakuanga hapa, nimeshinda nikisungushwa na gari, kwa hivyo siku ingine, wale watamtayarishia kuja hapa, mjaribu, tuko na hall vile mlisikia mwenzangu hapa, tuko na hall mingi sana kuko ambazo, ni watoto tu wanakumianga huko dani, hakuna kitu zinafanyiwa huko, kwa hivyo mngetutayarishia siku ingine mkija hapa, mtatutayarishia pahari tutakutana, wananchi wote wa Dandora.
Haya, mambo yangu yale niko nayo, nitaanza na kuhuzu majudge, kuhusu upande wa majudge, mimi ningeonelea kuwa, imekuwa ni gumu sana ndio unaona majudge wako corrupt, kwa kuwa wanachaguliwa na mtu mmoja, mimi ningeonelea hawa majudges, wawe wakichaguliwa na MPs, na pia mawakili wapewe hio nafasi yakuchagua majudges. Hilo ndio oni yangu ya kuanza.

Jambo la pili, wale wameweza kutebelea mahakamani, mnaangalia mambo ya prosecutors, mimi ningeonelea, prosecutors, asiwe tu ni mtu ambaye anatolewa kwa police anafudishwa fudishwa kidogo hivi halafu anaanza kuambiwa awe prosecutor, ningeonelea, isipokuwa tunajua kuna wale wametoka kwa law firms, prosecutor awe ni mtu ambaye anatoka kwa law firms, mtu ambaye amesomea sheria, na hata mambo ya kuhusiana na wananchi.

Jambo la tatu ni kuhusu President, ama Prime Minister, ikiwa kutakuwa na President ama Prime Minister, mimi ningeonelea isiwe ati kuwa ati wee ukiwa tu ati umezaliwa hapa Kenya, ati wewe ndiye tu unaweza kupigania kiti ya President. Ikiwa wewe ni mwananchi (citizen) yaani tuseme umekua citizen wa Kenya, hata kama umetoka England, hata kama ni wapi, uwe ha haki ya kupigania hio kiti. Ndio hii sababu unaona imeleta vita katika nchi nyingi, kwa kuwa tukisikia President atakuwa mkikuyu, wajaluo hawataki kusikia hiyo, tukisikia President atakua mjaluo, mkikuyu hataki kusikia hiyo. Tunaweza kuwa na President, ambaye ametoka hata nchi ya nje, hata kama ni Mr. Clinton akitaka kuja kupigania hii kiti hapa, awe huru, si ati lazima awe mkikuyu ama mjaluo ati amezaliwa hapa Kenya. Hio mimi ningeonelea, inasaidia hata kama miaka ya baadaye, hatujui kama Kenya itakuja kuwa kama Rwanda. Hio itakuwa inasaidia, yule ambaye mumemchaguwa hautasema ni Kikuyu, hautasema ni Jaluo, Mkamba au nani.

Oni yangu ya tatu – jambo la tatu ningeongea kuhusu Attorney General, Attorney General ningeonelea, isipokuwa sijui kama saa hii aka na assistant, ningeonelea kuwe na Attorney General wawili, kwa vile kazi ya Attorney General inakuanga ngumu sana. Sio wengi washa wahi tomboa. Hata yule tuko naye hapa, isipokuwa tuchallenge yeye, ni vile tuko in a corrupt government, hii kazi inakuanga ngumu sana. Hio ningeonelea wakuwe wawili, na wawe wanachaguliwa na Parliament na lawyers.

Jambo la nne, ni kuhusu maendeleo. Mambo mengi ile umeona imeleta shinda hapa Kenya ni kuhusu hii mambo inaitwa maendeleo. Mimi ningeonelea kama ni barabar inatakiwa ijengwe pahari, isiwe tu hati mbunge ameenda kupiga kelele kule mbungeni ati njia ya kwangu nataka ifanywe hivi ifanyw hivi, hii upande wa maendeleo ningeonelea kuwe na committee ambayo itakuwa inaangalia maendeleo ya pahari furani. Utaenda sehemu zingine, utakuta kuliwekwa barabara ya lami, na hiyo barabara utakuta ni mbuzi zina lala huko, wamama wakishatoa mahindi kwa shamba, wanazianika huko zikauke, hii sasa mimi ningeonelea, ikiwa ni mambo ya maendeleo, kuwe na committee, na sana sana ningependa committee ambayo si ya hapa Kenya, iwe ni committee yakutoka nje, kwa vile kama ikiwa majudge wetu wanakuja kuchunguzwa na watu wakutoka nje, hii committee iwe inatoka pahari pengine ambapa kama ni mzungu ametoka England, hajui mkikuyu anakaa namna gani, anasikianga mkikuyu, anaenda anaangalia hio pahari, kama ni barabara inajengwa, inafaa ama haifai, ndio hii pesa ya wananchi iwache kupotea bure bure.

Jambo la tano, ni kuhusu elimu, elimu hii imesemwa na watu wengi lazima iwe bure, lakini kuna kitu ingine ningesema, ikiwa itakuwa bure, serikali isomeshe mtu (kama mimi ilinisomesha nimeenda nimeenda nimesoma zaidi, nimesoma hata nimeingia huko University, nimeng'ang'ana na vitabu, hulali, huli, halafu baadaye, inakuwa je? unatoka nje, unakuja kushindana na mtu ambaye hakuenda shule kuuza sukuma huku na maziwa.) Mimi ningeonelea, ikiwa ni namna hiyo, serikali kama inakusomesha, halafu inashindwa kukupatia kazi, kuwe na kiwango fulani utakuwa unaenda kuchukuwa huko, kwa hiyo serikali, ikiwa kama sisi tukiwa University tulikuwa tunaambiwa, ukitoka kuna ile kiwango unatoanga kwa serikali, ukisha pata kazi, na kama hupati kazi, na ulisoma, ilikupotezea wakati, kwa nini usiwe na kiwango fulani utakuwa ukiindai, ndio ikutafutie kazi? Nimekuja jambo langu lingine ni kuhusu hawa walemavu, mtu ambaye ni mlemavu, ningeonelea awe akiangaliwa ni kiwango gani ya ulemavu, huwezi kuwa hun jicho moja, halafu wewe ujiite mlemavu, kama hii ingine inaona, wewe sio mlemavu, iwe inaangaliwa ni kiwango gani ya ulemavu. Na mlemavu yeyote, asiwe analipishwa tax, na pia upande wa ulemavu awe na pia na haki ya kwenda kudai kiwango fulani kwa serikali. Hilo ndilo jambo langu la saba.

Jambo langu na nane, ni kuhusu, child abuse, wananchi wenzangu, tunasikianga child abuse child abuse, lakini chokola sio wote ambao wanafaa kuwa chokola, sasa hii ningemuonyesha watoto wengi hapa, ambaye baba yake unasikia ni mechanic pahari furani, mama yake unasikia ni secretary pahari furani, na huyo mtoto unasikia ni chokola, ni kwa nini? Ni kwa sababu, hawa watoto, wazazi wao, mama yake akitoka kazi, anaend kwa pombe, baba yake akitoka kazi, anaenda kwa pombe, mtoto, haendangi shule, Kama hii town mnaona hapa Nairobi, utakuta watoto wengine hapo ufikirie ni chokola, naonanga wamama wakipea ati pesa pesa hivi, na hafai kuwa chokola, wengine ni watoto wao kuwa careless, sasa mimi maoni yangu ingekuwa hivi, hawa watoto, kama kuwe na community ambayo itakuwa inaangalia nyumba za watu, ikiwa ni wewe umekuwa umeanza kuabuse hawa watoto, kuwekwe sheria ya kusema, kiwango furani ya mshahara yako, itakuwa inakatwa inaenda kwa hawa watoto na kuwasomesha bure, kama mnashindwa, namnanyang'anywa hawa watoto, wanaangaliwa na serikali.

Haya, kuna jambo lingine kuhusu matajiri na masikini, mimi najua hapa kabila tunakuwanga na mbili, usindanganywe ati huku

unasindanga ukiniita mimi jaluo, mimi mkamba, mimi kikuyu, lakini hapa tuko na kabila bili, masikini na matajiri, Hii ni jambo ambalo ningependa iangaliwe kwa umakini kabisa, kwa vile hii gap yakuwa ati matajiri na masikini, ati umesikia vile hawa wenzangu wanasema ati mtu mmoja anapata million moja, mwingine ata hapati kitu, hio ningeonelea pia liangaliwe.

**Commissioner:** Last two points bwana Ndirangu

**Ndirangu:** Kuhusu upande wa health, ndio nitasema, ninaonelea tuseme kama upande wa health kama ni hapa Dandora, vile unaona city council hatuangalii masilahi yetu, wawe wakionywa kuchukuwa hata koti,

Jambo la mwisho ndio ni malize, ni kuhusu upande wa serikali, ikiwa serikali itakuwa inashindwa kutupatia security ya kutosha, ukiimbiwa (kama saa hii kwangu kumefahamiwa) uwe unafanyiwa kitu kinaitwo compensation, unaenda hapo Kinyago, unaandikisha zile vitu zako zimepotea, halafu serikali inakugalimu hizo vitu, asanteni.

**Commisisoner:** Asante bwana Ndirangu, you were very clear, please go and register in there. Thank you very much. Nilikuwa namuita sasa Peter Gichane, yuko, Susan Ombengo, utamfuata.

**Peter Gichane:** Hamjambo nyote? Kwa majina naitwa Sospeter Gichane, ningetaka kutoa maoni kadhaa, na kwa sababu ninaona niko maoni mengi, labda nitaenda kwa bio bio , na mengine ya mesungumuzwa, kwa hivyo nitapitia .

Kwanza ningetaka kusema kwa upande wa serika, ningeuliza kuwe na kile kiti cha Prime Minister, besides the President na tukuwe kama nchi labda kama Israel ambao wako na Prime Minister na President, Prime Minister akuwe ndiye overroall leader, na akuwe incharge wa Parliament, akuwe pia the Chief Executive Officer, na pia akuwe elected directly, juu yake kukuwa na President ambaye pia atakuwa ni kama overall manager, so tha the Prime Minister becomes the leader of the government, the President becomes the overall manager of the National institution, na akuwe incharge ya overall management and administration of government policies, na pia akuwe elected by the Parliament, akuwe incharge of something like the Provincial Administration, na civil service. Hao wawili ningeona wakuwe wanaangaliana, each to check the other, for purposes of cheques and balances. Juu ya hiyo, kwa kiti ya Prime Minister, Prime Minister asikuwe Prime Minister kam hatapata zaidi ya kula 51% kwa zile kula zote zimepigwa, na kama itakuwa ni President pia, lazima apate hiyo kiwango, ndio tuweze kujua ya the President, or the Chief Executive, is the presentative of the majority.

Jambo la pili ikija ni Parliament, ningeuliza, all appointments done by the Chief Executive, zikuwe vetted na zikuwe ni kama za Ministers, Judges, Public Service Commission, Electral Commission, Attorney General, Chief Justice, Controller and Audit General, Parastatal Chiefs, kwa sababu hatungetaka kuona, mali ya uma vile institutions that are public like the NHIF, NSSF, COTU, even something like Kenya Power and other parastatals, being headed by people who are not direct from the President. Besides that, tukiendelea kuwa ni kwa registrator, mishahara yao, ya Parliament, haistahiri kuwa issue yao

wenyewe, because you cannot expect a thie to catch a thief. So I would suggest that a special commission be set up to comprise of something like three judges, the Attorney General, the speaker, the judicial service commission, three members of the public service commission, and the chief justice. Besides that, ningeuliza kuwe na Government of National Unity, or coalition which will be representative of all parties with majority seat, if any political party wins, over that MPs in Parliament, then they are entitled at least to be one of their members sitting as a minister or assistant minister. Vote of no confidence in the government, ile ambayo inapitishwa na parliament, iwe by 65% . Pia kila mbunge, anasitahili kuwa anahuthulia mukutano mmoja kwa kila mwenzi, katika ile constituency ambao anawakilisha. Hii ndio tuhakikishe ya , mbunge anafanya ile kazi anafanya. Kwa wakati huu, naona hata mbunge akichaguliwa, anasema ni miaka 5 niende huko, nikule niende. Kwa hivyo lazima tuhakikishe that there is one particular forum that a Member of Parliament should hold. Sorry, Chief Executive akuwe ni above 18 years and not more than 70 years and then akuwe ni mtu wa degree, sio mtu mtu ambaye aliachia standard 4, na anasimamia maproffesor. Hio ndio maana tumeona ya Kenya, kumekuwa na upolaji mwingi sana wa mali, kwa sababu wakubwa wamekuwa tu ni watu wa kuweka signature, na mambo kama hiyo.

**Commissioner:** Take your last two points, we shall read the memorundum. Just the last two points.

**Gichane:** Lile jambo lingine nilikuwa nataka kuomba, ni kukuwe na commissions to be established, at least there should be a human rights commission, a national disasters commission, and a social services commission. Jambo lile nitasema likiwa la mwisho, ni , pia lazima tuangalie tukiwa wakenya na tuone ya , hii nchi, resources, sisi tunaendelea kukuwa wengi, in other words the population is growing, but the resources are not growing, so what do we do? To cover that, I would suggest that every family hould have a maximum of 3 children, kila familia ikuwe na watoto, wakizidi sana wakuwe watatu, na wakizidi hapo kukuwe na taxation, na juu ya hiyo, serikali iweze kuelimisha hao watoto watatu mpaka University, na iwatafutie kazi, kazi ikikosekana, kwa hao watatu, lazima basi serikali iweze kutoa pesa ya kusimamia hao watu mpaka wapate kazi. Kwa hivyo hayo mengine itabidi nipeana ile karatasi nilikuwa nayo. Asanteni,

**Commissioner**: Asante sana bwana Gichane, goja kidogo kuna swali,

**Commisisoner Solome**: Asante sana bwana Gichane, umetuelezea kuwa ungetaka kumuona waziri mkuu mwenye atachaguliwa na bunge, na watu wengi wenye wametusungumzia leo asubuhi wamesema, kuwa, wangetaka kuona mayor wakichaguliwa na wananchi, moja kwa moja, kwani wakichaguliwa na madiwali, hao wenyewe hawatumikii wananchi wanatumikia, wanaogopa tu wale madiwani waliwachagua. Je sasa tukipata waziri mkuu mwenye atachaguliwa na wenzake kule bunge, atawatumikia wananchi, ama atakuwa akilitumikia bunge?

**Gichane:** Mimi vile nilikuwa ni mesema, nilikuwa nimesema, tukuwe na Prime Minister ambaye ako elected directly na wananchi, lakini President akuwe elected by Parliament, that is the Prime Minister, itakuwa tu kama infact mfano mzuri ni kama tu Israel, Prime Minister anachaguliwa na wananchi naye President anachaguliwa na Prime Minister through the advise of the

Parliament.

**Commissioner:** Umeeleweka, Susan, Nahashon Onyango, you will follow her.

**Susan Ombeo:** Mimi nimesema asante Commisisoners, Niko hapa, mimi ni Susan Ombeo, na mimi natetea watoto (mimi ni mwalimu). Hapa Dandora nimekaa miaka mingi sana, na nimekuja hapa, kuelezea juu ya watoto, watoto wetu wanateseka, kama sasa tuko na watoto shuleni, wachache hawalipi school fees, na hao watoto hata walimu wenyewe, hatuwalipi, wanafanya kazi ya kusaidia, muwaangalie. Hio ni jambo moja ni meeleza.

Ya pili, sisi wamama, nikirudi kwa wamama, sisi tukiolewa,

***End of tape 4***

**Tape 5**

***Starts like this***

Anaona yeye hasara ikiponyokea hio shinda, sasa anaweka ata wengine, dudu ikiwakula hajali, kama tuseme hii area 6 ya Dandora, imezibwa barabara hiyo, na takataka, na ilikuwanga shortcut hata ya kwenda police Kinyago, ambapo unefanya wananchi wengi kuteseka. Na la mwisho hasa ningependa kuquote kitu kimoja, tume. Hii mambo ya serikari kuweka vitu kama jeshi ya barabara hii, ningependa ifutiliwe bali, juu serikali yenyewe ilisema wakati walipointroduce kitu kama TLB, walisema itakuwa inatoa hao vijana,wenya wanamann barabara, huku ili hiyo itakuwa inaongoza, na nilithania mpango yao itakuwa wanajenga office, ya mangari, yenye wana deal na TLB maofficers watakuwa wa kimonitor their movement, lakini walisema tU kwa msemo lakini hawakufuatilia, Kwa hivyo, nathani ni hayo tu.

**Commissioner:** Asante bwana Onyango, tumeshukuru, jiadikishe, Samuel Njeru, sorry, utamfuata bwana Macharia, hapa baadaye, Charles Mwangi, haya endelea,

**Mwangi Warigwe:** Asante sana commissioner, na wanaDandora wenzangu? Kwa majina mimi naitwa Mwangi Wareigwe,naishi hapa Dandora, kitu moja mimi ningetaka kusema, ni kuhusu mambo hii ya slum dwellers, na street dwellers, mara mingi sana watu wanaambiwa, inaonekana kama ni kawaida, watu kukaa kama hapa Gitari Marigu au kwenda huko kuchokola, lakini hii yote, inaonyesha ni kuwa serikali yetu haijali watu wale wengine. Kuna watu wachache wanajiona, hawa wanafaa kula mzuri, na ile mabakio wanatupia sisi hapa pande hii. Kitu ilioko, ni kuwa, Kenya, sasa, hapa kila mmoja, sasa anafaakuwa na plot yake, hata hapa Naiobi, watu wakihesabiwa wote, wale ambayehawana plot, wanaweza kupata, ukiambalia kama huko Ruai, au huko bali kidogo, unaweza ona, watu wote wakichukuliwa hapa, wale ambaye hawana pahari, wanaweza kuwa settled pale, na wawekewe skuli, na wawe wanaendelea maisha mzuri. Kuwe na programme mzuri ya kusettle wale watu wanaishi katika slums, au wale wanafanya chokola huko. Kwa hivyo ni moja naona, hata wacha sio Nairobi pekee yake, Kenya mzima, hakufai kuambiwa, mtu hana shamba, au hana pahari anatoka, hana pahari anatoka, Kenya, ni

kubwa kweli, ukiangalia population ilioko, na ugawanye ile mashamba iko, utaona kila mmoja, anaweza kuwa na pengine acre kama ishilini, kila mtu, kila mkenya anaweza kuwa na acre kama ishilini, Kwa hivyo hatufai kuambiwa, wewe uko landless na huyo mwingine ako na melfu ya acre. Kwa hivyo hiyo ni njia moja ningetaka Natural resources iwe, imegawanyishwa, sawa sawa, ile kila mmoja awe ana pahari pake anaita nyumbani, na kutakuwa hakuna tabu yeyote ile tunaona hapa, watu wengine tunasema security, ndio, security itakuwa mzuri namna gani, wewe unakula unashiba, mimi nakuangalia ukila, sasa hii na mna gani itaweza kuelekea namna gani? Kwa hivyo, hiyo kitu, iangaliwe sana, land resources inafaa inafaa iangaliwe na inaweza kusolve problems nyingi. Hapo tena ni ngetaka kuongea kuhusu hii governance, ningetaka hii kutoka sublocation kuwe na national assembly, au mbunge ya kijiji, kutoka hiyo, hiyo bunge ya kijiji, kuwe na ingine ya location, namna hii division, mpaka district province mpaka national. Hii sasa, itafanya hata yule mkubwa, awe answerable to the National Assembly, at the sub-location level, na ndio sasa ile haki, ulimpatia, ukamuambia mimi nataka wewe uende uniakilishe pale, unaweza kumng'oa kama hakufanya vile unataka, unaweza ng'oa. Na ile bunge ya kijiji, pale pale itakuwa ikiresolve mambo yenu, mambo wale watu wako hapo, kama ni security, kama ni mambo ya masomo, kama ni mambo ya Daktari, medical, mambo kama ile, ile mambo ya kijiji inaweza kuwa na maneno mingi, hata security, kuliko kupatia watu wengine, tunasema iko police, au iko chief, sisi wenyewe, tukiwa tuseme kama hii ni bunge yetu, tunaweza angalia maneno yetu kama ya security, tuseme security area hii iko namna hii namna hii, na wale wanaharibu ni hawa, na kwa hivyo tunachukua hatua hapo hapo, kama inazidi, tunaipeleka kwa hiyo ingine ya juu, ya location, namna hiyo namna hiyo mpaka mambo yote itakuwa ni sisi sio watu wengine wakutoka nje. Nimesikia mwingine akisema, pengine tu ite, wangereza waje wasaidie sisi wa bali, aa, mimi kwangu, problems zile tuko nazo, ni sisi wenyewe, tunaweza kusolve. Na ndio hapo, naona, upande wa governance au kuangalia maneno yetu ya development, tuanzie nyumbani, bunge ya kijiji, neighbouring assembly, ya sublocation, location, division, province, mpaka national, na hiyo pengine, iwe ndio inaangalia uhusiana wa nchi yetu na mambo ya nje,

**Commissioner:** Point mbili za mwisho sasa,

**Wariegwe:** Ni hiyo tu nimekuwa sina mengi isipokuwa nimetaja hiyo ya land issue, na mambo ya hiyo neighbourhood assembly.

**Commissioner:** Asante bwana wariegwe, asante umeeleweka, karibu ujiandikishe, karibu bwana njeru.

**Samuel Njeru:** Asante sana wacommisisioners, kwa majina mimi naitwa Samuel Njeru, na kwanza ile nitasungumzia ni Presidential and Parliamentary elections. Hii mimi ningetaka kwanza nipropose sasa hiyo ningefikilia ifanywe muaka huu, tusiendelee mbele, vile wengi wanasema tuongezwe miezi ingine sita, hiyo miezi sita mimi ningepropose tusiendelee nayo miezi sita, tuwe na election mwaka huu. Na hiyo, tukiwa hapo hapo, wale tunawachagua, mimi ningefikilia ni mzuri, tukichagua watu, tuchague wale iwe iko kwa record kwa Presidential and parliamentary election, mtu akiwa na criminal activities na akiwa ameimba, akiwa ameuana, akiwa amefanya nini, asikubaliwe kusimama kwa hiyo Presidential Elections or Parliamentary civic elections, iwe iwekwe kwa katiba, ndio kwa kuwa tuko na wakora wengi sana huko kwa bunge, tuko na wakora kwa city council, tuko na hata wauwaji, na hiyo ingefaa kama katiba ingelekebishwa, iwe hawa watu waondolewe.

Jambo la pili, ni hii serkali, ile itaundwa, iwe serikali ya National Unity, iwe serikali ya muungano, ya kila watu wale watakuwa wamechaguliwa na vyama vyote, lakini hizo vyama vile ningepropose, vyama navyo vipunguzwe, katiba ipitishe tuwe na vyama vichache na vile zitakuwako, na vile zitaunda hiyo serikali, naye serikali ikiwa, (ile tutaunda), itengeneze financial ethnic zile zao, tusiwe tunatengeneza financial estimates zile zinaweza kutegemea mapato ya nje. Tuwe tukitegemea ile mapato, tunapata kwa nchi yetu, lakini sio kutegemea mapato ya nje kwa kuwa kama sasa, tumekuwa na shinda mingi, kwa kuwa tunategemea World Bank, tunategemea IMF, na wale wengine. Kwa hivyo mimi ningefikiria hizo, tungefikiria financial estimates, ikitengenezwa serikali ikitengeneza financial estimates yake, iwe inategeneza financial estimate from the income ile Kenya yenyewe, inaweza kupata, sio kutegemea mahari ingine. Ile kitu imeleta ufisani Kenya, sana sana ni hii kitu mnaita harambee, watu wamepindua harambee, harambee ilikuwa kitu ya kusaidiana, lakini siku hizi imekuwa ni kutu ya wizi. Watu wanatengeneza habari ya harambee, wanatengeneza harambee wanaimba pesa, wanatengeneza harambee ya kutengeneza shule, badala ya kukutembelea kujenga hiyo mashule, hiyo inakuwa ni pesa ya kuimbiwa na wale wanapewa hiyo jukumu ya kujenga hio mashule. Na hiyo ningefikiria ni mzuri, tumalize hiyo kitu inaitwa harambee, kama ikifanywa, serikali ipate njia ingine yakijenga mashule au kutengeneza mabarabara zetu lakini tusitumie hio jina harambee.

Kitu ingineni kama hii gabbage ya Dandora, kweli hii ni kitu inatudhulu sana, watu wa Dandora, Gabbage hii kumekuja MaPCs, Kaguthi na Lokoloo walikuwa ko, akasema dumping site itaenda, Kaguthi akakuja akasema gabbage itaenda, bwana Nyenze, Minister wa environment akakuja hapa akasema gabbage itaenda, Bwana Kamotho akakuja hapa akasema gabbage itaenda, kijana yule amechaguliwa hapa juzi bwana Uhuru Kenyatta, naye akakuja akasema gabbage itaenda, Hii serikali mimi nauliza, kama haina mwelekeo, kila mtu anakuja anasema gabbage itaenda, and they don't put that one into action, kwa hivyo serikali ikisema kitu, tutafanya hivi, lazima hiyo kitu ionekane imefanyika lakini sio serikali kuambia wananchi, inadanganya wananchi wale wamewachagua, inadanganya kila siku tutamfanyia hii, tunamfanyia hii, na ni mali ya ume wanatumia, tafadhali hiyo ilekebishwe kwa katiba, iingizwe kwa katiba waambiwe, serikali ikisema, ikifanya kitu, ikipromise wananchi kitu, iwe ni haki na sio ya kundanganya.

Ya mwisho, nitasema ni kama vile ufisadi mwingine, kama hapa Dandora mumeuona kwa macho, iko gari hapo gari ya police inazunguka, gari GK 2223, inazunguka kwa kila bar ikichukuwa shillingi mia moja, na nyinyi mwaona, na wakati tuna-report hiyo, tumeshajaribu kwenda kwa police, tumeshajaribu na tunasikia hiyo pesa wanaokota, wanagawa kutoka kwa mdogo mpaka kwa yule commissioner, kwa hivo, hakuna mtu mzuri kuliko, hata commissioner wa police hata yeye ni kwa kuwa hiyo mambo inafanyika, hata yeye inafanya hiyo corruption. Kwa hivyo corruption hiaanzwi na yule ako chini, inaanzia na even commissioner mwenyewe, kwa kuwa watu wake wanafanya namna hiyo na tunaona, na hawaulizwi, na wanafanya hiyo kazi sio kazi inafanyika, hio sio kazi ya kusaidia wananchi, kwa hivyo mimi ile kitu, ya mwisho, ni hii tunaika registration of organizations, in the Attorney General's chambers or wherever, all organizations are registered under the societies act, kwa Attorney General, na mimi nimeona makanisa, ingine ingine inaomba shetani, ingine inaomba sijui nini, ingine inaomba nini, wengine wanakula watoto, wengine wanachomana kwa nyumba, wengine wanatoa nguo wanaomba wakiwa uchi, sasa unasindwa hizi nazo zilikuwa registered na nani? Ni kama hakuna sheria ya kuchunguza hizi makanisa ndio tuondolewe kwa

kuwa, zingine zikiwa za aina hii, after that moral za watu wakenya zitapotea, na hatutakuwa na morals, kwa hivo tunauliza commission hii, iwekwe kwa katiba, kitu ikiwa registred ikiwa ni organization yeyote, ikiwa registered, iwe kweli imejulikana ni kitu inasaidia wananchi, iwe ni kitu ya kumwambudu Mungu, lakini sio hizo za kumuambudu shetani. Tumeona commission naye zimetolewa, hata zile watu wanaomba shetani, ikifika mahari, inasimamishwa, kwa kuwa mtu furani ako huko. Kama unaomba shetani, na wewe unatuongoza, kweli utatuongoza kwa haki? Mtu akiomba shetani anaongoza watu kwa haki? Hawezi kutuongoza kwa haki kama ni mtu wa kuomba shetani, na mimi ningemuuliza commission hii, hiyo iwekwa kwa katiba.

La mwisho, nikuuliza habari ya education yetu, mimi ningeuliza education kama vile mmeona sasa, ukienda kwa nursery, kwa primary schools, mtomo analipishwa shilingi elfu tano, mtoto wa primary. Mama hana mahari ya kutoa, kama watu wa Gitari Marigu, mmesikia zile shule ziko hapa, nyingi na za informal kwa kuwa ni za kusaidiwa, ile formal ni karibu shule nne, na hizo nne haziwezi zikatoshea watoto wetu ya Dandora, kwa hivyo ni jukumu lenu commissioners mukitengeneza hii education act, mseme education iwe free na iwe free, kama hakuna harambee, shule ilijengwa miaka tano, na haijengwi tena, unasikia mwalimu akipeleka mtoto huko, anaitishwa building fund, na hakuna kitu inaongezwa, shule ni ile ile, mawe ni ile ile, krasi ni ile ile, isipokuwa desk inaweza kufujika na iwe replaced. Mimi singeonelea ni vizuri tuwe tukilipisha wazazi. Asante.

**Commissioner:** Umeeleweka bwana Njeru, Asante sana jiadikishe pale. Goja kuna swali.

**Commisioner Salome:** Asante bwana Njeru, ningetaka utupe pendekezo lako juu ya vyama vya siasa, umesema ziwe chache lakini hujatuambia uchache upi?

**Njeru:** Ningetaka ziwe chama kama tano.

**Commisisoner Salome:** Ok. Asante.

**Commissioner:** Asante sana, Charles Nyaga, Charles Nyaga, James Macharia, James Macharia, Peter Amino, Peter Amino, George Waweru, George Waweru, Antony Njoroge, Antony Njoroge, Michael Odiek, Michael Okiek, W. O. Ayaga, Reuben Kimani, karibu. Rashidi Odhiabo, Rashidi Odhiabo, utamfuata,

**Reuben Kimani:** Greetings to you all commissioners and all those people who have attended this constitution review commission.

**Commisioner:** We receive your greetings, tell us your name first for the record.
**Reuben:** My name is Reuben Kimani, My protests are as follows:
Creation of the office of the ombudsman to be in the next new constitution. The office of the ombudsman to have security of tenure and to be approved by members of parliament with two third of parliamentary members, to be on the same grade as that

one of the Chief Secretary and the Head of the Civil Service Commission, to retire at the same age as that of judges. XXX to provide PTA to have 220 secretaries one from the parents and the Headmastet to be the other secretary of the PTA. All the committee members to be of the minimum mean grade C of Kenya Certificate of Primary Education, the chairman of the PTA, primary education, to be selected by the parents, but not the committee as it is at present. Also the secretary, and the treasurer to be elected by the parents. Special meetings to be given a notice of 18 days instead of the present 14 days. Termly budgets to be made but not annual budgets, embessement of school funds to be a crimimal but not civil case as it is presently,

**Commissioner:** Bwana Kimani, for your information we do not want you to read every part of your memorandum, it is too long, we want you to highlight very few parts, the remaining 3 and a half minutes. I gave you five minutes, and you have taken two and you haven't even gone through half of the page, highlight the most important parts in the next 4 minutes.

**Reuben:** Civil proceedings against the government to be 36 months instead of the present 12 months. University employees to retire at 55 years and not at 60 as it is presently. 500 people to the present xxx , if our Kenya parliament passes every bill which the public will find that it is not good, evidence actually to be amended so as for the copies of the original ducument to be allowed by our courts after a sworn affidavit that the original document are lost, stolen or burned. Consent to prosecute, and xxx to be given by the Attorney General as to why he entered xxx and the dependants to oppose by giving their reasons as to why it should not be entered by the Attorney General So the act to be amended to provided as the all those people to xxx elected offices be be of minimum KCPE standard. Cooperative act also to be amended so that the holders to be of the minimum KCPE certificates. Good award payments to be paid in two cheques, one to the lawyer, and one to the person who was awarded those court awards. High court judges to be appointed by the President but to be vetted by the Parliament and to retire at 65 years when one requests but the compulsory retirement to be 70 years, also to be vetted by the Parliament. Civil servants, from honourable secretary and above, to be employed on contract basis of 4 years each but renewable up to when one will reach the age of 55 years.

**Commisisoner:** Pick the last two issues now,

**Rueben:** National Social Security fund contributors to be at the age of 40 years, 45 or 50 years.
500 people to be required to be the minimal to press the Attorney General to sue anyone or any company, if he refuses to do it. Gabbage management to be provided in our environment act to provide that rubbish will be dumped any estate from the neighbouring estates.

**Commissioner:** Thank you Mr. Kimani, we shall read every single sentence from that memorandum, so please register it and and leave it with us, thank you very much. James Kasemba, james kasemba,

**Rashid odhiambo Alogo:** Thank you so much, the commissioners as well as all Dandora residents. Now my names are

Rashid Odhambo Alogo, I have about 7 points to put across but first, at least I have to express my statement to the government. (***interruption)*** My first request is to the government, now the constitution is too preminen given democracy, and as it is in Kenya, this review, I think it was given such a short period. Other than the Lankasta, constituency which we were given, so many years ago, I think this is now the golden opportunity we as the common people are having. Especially in expressing our views on how we would want our government to govern us. Now I would want the government to increase the period of this commission because, whatever we are doing here is going to govern Kenya for so many years, I think 100 years and more. Elections should not interfere with this process, the election if anything, the elections came and went, and even if we hold election this time, it is going to take only 5 years, but whatever we are doing here, is going to help ourselves govern ourselves for the next over so many years.

Now my 1st point, is about the organs of the state, now in any democracy, the organs of the state, that's the regisrator, the the judiciary, as well as the representative of the land. In Kenya as it is, the balance seems to be there or if it is there, then it is by mere word of slogan, because the representative, seem to be much more powerful and is sitting on the regislature as well as the jucidiary. My request is that we should have a constitution where the 3 organs of the state are balanced. Now as you can see, in Kenya, it is the Head of the Executive i.e the President, who appoints even the judiciary, it has all controls over it.

The 2nd point I want to put across is on the judiciary, our judiciary, I don't know if it is because it is appointed by the Executive, but it is actually very much corrupt. Cases are too slow, things are I mean , they are too much of xx xxx there. Then judges at the lower courts are giving a court of appeal a little bit of hard time because whatever they are judging, those people are ruling, and the judgement, people are dissatisfied and they flock the court of appeal, this happens because the judges, whatever they say, they are ruling and the judgement is unquestionable. I should think if, whoever appoints the judges, that is the person in the President, is questionable, then why not the judges?

Now, No. 3, is on the political parties, with the arise and coming of multi partysm, I think we Kenyans are not so observant on this issue, like it is, we are having over 4o political parties, some of which we even do not know, now I would suggest that we have 3 political parties, 3 and I think this should be a must, and the few political practice we have, will actually bring sorberness in us and we will work very much positive towards the political team in Kenya.

Now No. 4, is the sizes of the constitution, it is the jurisdiction of the President to create few constitutions, now the President being an MP, he also have his lot, and he being the Head of the Executive, I think so many things are imbalanced, because in parliament, votes are made on one man one vote, irrespective of the size of your constituency or the number of people you represent. I should think the constituencies should, we will find that the sizes are almost the same so that when we go to voting, we will be at least fair.

No. 5 is about the police force, our police force are a little bit so much corrupt. Such at times I always think you would rather

meet the thugs rather than the police, because policemen are becoming double. One thing they are plained xxx, then number two, they government officers, they do anything they want. They rob, they ask for bribes, and then they do all sorts of things, Now in short I should suggest that we establish a wing that will overlook the work of the police, like we have the military police and this office should be idependent and accessible to the common man, because it is hard, who are actually seing what these policemen are doing.

No. 6 is on election, I think the elections of the President should be held separate from that of MPs and councilors. Then the President should be an affiliate of any constituency, he should not be an MP, then he should have 2 five year term as it is today, then for the MPs, I should suggest that they be be given 2 five year term, just like the President, especially in one given constituency. Whoever will be interested in the elections, to be elected for the 3rd five year term, should either change the constituency or leave it.

On the issue of NSSF, the age which was set by the government, for refund of NSSF fund is 55 years, I think the average death age of Kenyans today is about 45 years, if you analyse properly. I think they should reduce this age because people have become so fragile, to get at the age of 45, people will even be appreciating you. So they should reduce to around 40 years, so that you enjoy the benefit of whatever you saved. Then, on the same issue of NSSF, there are conditions which qualifies somebody to get the refund of his NSSF, say like age evidence which is a mandatory licence to death once you are diagonized to be HIV positive. I should think, you should be given all the funds so that you help yourself.

My last point is on the labour, especially the Ministry of Labour, labour laws seem to have been XXx. In the private sector, which employs almost 85% of Kenyans, there seem to be a lot of things going on, now SKE and Kenya Association of Manufacturers seem to be pocketing the labour ministry, most of the employees, upon which the government get taxes, are blaketed under casual force, but in the real sense they are not casuals, in so doing , the employers actually robbing the government of so many taxes in form of PAYE, NHIF, and all these others, in other words these taxes, on the other hand they are trying to subject their employees to substitute and slavery because whoever employs you as a casual, it means in the later days, when you will leave the same employment, you will not have anything to depend, say in terms of services and so on. At the end of every pay I think you have may be half XXX and so on. Thank you so much.

**Commissioner:** Thank you Rashid, you were very clear, please register at the table there, Nancy Muthoni, Nancy Muthoni, Joo ukaseme yako tafadhali, Lucy Wambui yuko, Lucy wambui, Yuko? Endelea,

**Nancy Muthoni:** Hamjamboni nyote? Kwa majina ni havyo mmesikia, Nancy Muthoni, Nakaa upande wa Canaan Dandora phase I mwisho. Kwangu hapa kusema habari ya corruption, corruption hii tunayo hapa, na ni Kenya mzima, kwanza imetokana na sisi viongozi, kwa maana, viongozi, sababu mahali pahali mtu yuko, pako na kiongozi, wake yule mwenya anamuogopa. Kabla ufike, pale juu, huyu kiongozi mko naye mahali uko, yeye ndiye ameanza corruption, kwa sababu

ukimuendea na jambo fulani umuambia bwana chairman, au bwana chairlady, au secretary au treasurer, kwa maana kijiji kama hiki ya Kinyago, na ile ya kwetu canaan, tuko na chairlady, tuko na chairman, tuko na hata na secretary, tuko na hiyo central committee ya mahala tuko. Ukienda mahala kama hapo umua
mbie niko na shinda hii na hii, na hili lingine, atakuambia, uko na shillingi 500 nikupeleke kwa police, ndio aende akakutetee hilo jambo kwa police, kumaanisha hiyo corruption imetoka mahali ulipo. Na ndiye sasa, ukifika kwa police, unakuta corruption iko juu sana kwa sababu ya hii kitu kinaitwa Toa Kitu Kidogo. Na hii kitu kidogo, kimeharibu hata sisi, ni kwa sababu saa zile jioni usiku, mwendo wa saa mbili ukikutana na police, kama ni vijana wameshika vijana, inaitwa train, inaitwa "mugithi". Mnashikanishwa nyinyi mlolongo mkuubwa, kutoka hapa mpaka pale mwisho. Wewe kama mzazi ukienda kufuata huyo kijana yako ameshikwa, unaambiwa, police anakwambia tumetumwa na mkubwa. Mkubwa anataka 50,000, na hiyo 50,000 umefikilia sisi tutaitoa wapi? Kwa hivyo watakuja washike huyu kijana, ndio na wewe mama ufuate huyu kijana, utoe shillingi mia tano. Ukienda kwa huyu mzee wa kijiji kwa maana wameelewana na huyu police, atakwambia pia, twende na wewe lete shilling mia tatu, umepunguziwa mia tana unatoa mia mbili. Hiyo corruption, hata sisi wenyewe tuko na corruption. Na sisi kama laiya, kwanza, ukijua umeshikwa, na una haki yako ya kujitetea, ukijua umeshikwa na huna kosa lolote, usiogope, pelekwa pale police, pelekwa jera, sababu wewe unatetea haki yako. Usiwaonyeshe hio pesa, maanake ukiwaonyesha hio pesa, hamtakosa kushikwa nyinyi vijana, mtakuwa kila siku mnashikwa, kila siku mnashikwa, na saa hiyo ni mkubwa ameitisha kitu kidogo.

Ya pili, ni grabbing, hiii grabbing ya hizi open spaces, hii grabbing imekuwa ya juu sana hii Embakasi, na hiyo corruption, imekuja na sisi viongozi, kwa sababu tumeona open space kama hii, haijajengwa, pengine imetegewa zima moto, imetegewa shule, imetegewa hospitali, na mimi kwa sababu, niko na jaa, nitakuja kwa mwananchi kama huyu ni mconfuse, lete shilingi elfu tano, pale kuna kichaka nitakugawia plot pale, na wewe zako zinakuuma kwa mfuko, unatoa unaenda unamatia, unampatia kama nani na yeye si city council? Si umempa nguvu, ya kukimbia kwa City Council, aende akapeana hio pesa kwa city council, na wewe tayari unalia mfuko jaa na mtoto wako jaa.

Haya, nayo ya tatu, ni hii mambo ya hospitali, na hii habari ya shule, juzi President alitagaza shule ni free, sisi wazazi ambao tunasomesha watoto kule tukiendea Headmaster, anakwambia enda kwa President alitagaza shule ni free. Iko free wapi? Ni lazima ulipe, na tuliambiwa shule ni free, hio, kudanganya wananchi, kudanganya wazazi, hiyo ni haki kweli ya mwananchi? Anadanganywa. Hii Hospitali kama Kenyatta, ni hospitali ya serikali, ukienda pale pesa pia ya kulipa card, sijui dawa, sijui nini, huwezi ukatibiwa. Si lazima utakufa? Kama hauna uwezo utapelekwa wapi? Hiyo ni haki ya mwananchi kweli?

Haya, tukikuja jambo lingine, la mhimu ni hii, sisi, (laughter) Wacha tu nimalizie hapo,

**Commissioner**: Hapana, Muthoni, goja, joo, joo joo, sungumza tu, Niko na dakika mbili zilikuwa zimebaki zako, maliza.

**Muthoni:** Shinda za hapa ukiendelea kusugumza saana, kuna wengine watakufuata, na kabisa kabisa kama serikali tuko nayo

hapa, hapa wametuma watu wao, kuja kupeleleza, ni kiongozi mgani alisema hii na hii na hii, Ata ukipeleka malalamizi yako kule, utafukuzwa, ndio maana nimesema nikatie hapo. Jana, nasungumza habari ya jana, pale kweti kanaan, ile njia ikitelemka ukivuka na korogocho, palikuwa na kikundi kubwa sana, na ilikuwa ni wakora, na wakaua watu wawili, yesterday, waliua watu wawili, tulipoenda Kinyago, police walipokuja, walisema ni Mungiki, na hii mungiki, ilifanya kosa gani kwa serikali, na hii serikali na mungiki, katikati ya serikali na mungiki, ni nini inakulana hapo katikati? Ni nini inakulana katikati, kwa sababu utauliwa, ukutwe pale umeuliwa, isemekane ni mungiki, na tena sio mungiki alikuuwa, hio serikari mwenyewe, ndiye alitumia hiyo njia ya kunja wewe uuliwe, Serikali, wanashikana, na vikundi, vikundi vya watu hapa, vile unasikia zinatengenezwa zinaitwa, bagdad, kuna hiyo jama ya mungiki, kuna hiyo ingine ilikuwa inajiita pale tariban, hii tariban, na mungiki, na hii inaitwa bagdad, na hiyo ingine inajiita vikundi vikundi za vijana, inaongozwa na akina nani? Si ni serikali imeongoza hii vijana. Na hii vijana zinakuja kuuliwa si ni vijana zetu,? Ni kwa nini hii serikali, na hii serikali ndio tuko, ni kwa nini haiangalii masirahi, imalize hii jambo linaendelea? Ni kwa nini? Eh, tulipoenda Kinyago jana, mtu mmoja hakuwa amekufa, tukakuja na police wa kwanza, huyu mtu alikuwa analia woi, nisaidieni, nisaidieni, Police alimliza, ulipiga duru? Ulikuwa unaimba wapi? Huyu mtu akamwambia, saa zile nilikatwa panga ya kwanza, nilianza kupiga duru, nikaambiwa nisipige duru tena, nisaidie, alimuacha pale akiwa anaongea, na alikuwa hari mahututi, akaenda kwanza Kinyago, akatwambia tuchanga change pesa pale, ndio akuje achukuliwe, alipokuja kumchukua, alikuwa amebakisha kitu kidogo tu, kumuingiza kwa gari, ndiye huyo akakata roho. Serekali ni ya nini tumewekewa pale? Wizi unaendelea, ni ya nini tumewekewa hapa? Wizi unaendelea, wanakimbia kwa nyumba ya chang’aa, kushika mtu yule anauza chang’aa, kushika yule kijana anauza bangi, na mwizi amepitia pale na buduki, anasema yangu nimewacha, ni kazi yangu wanatufanyia serikali? Serikali inatufanyia kazi gani? Hii wizi wa buduki, imetokana na wapi? Na yule mtu anasitahili kuwa na buduki, ni askali tu peke yake, laiya anatoa buduki wapi? Dio akuje kuuwa mwenzake na buduki? Na serikali ndio inasitahiri kuwa na buduki laiya anatoa buduki wapi? Hii crashes kila mara unasikia, Kariobangi kuliawa watu 22,. Hata kama chairman, uko na haki gani ya kuorganize kikudi ya vijana na kuwapeleka kwa shamba fulani? Walinde hiyo shamba, hati ndio mwishowe upewe plot, na mwishowe utatoka hapo na saduku. Ni serikali gani hiyo inalinda wananchi? Ni serikali gani hiyo inalinda wananchi? Ni haki gani hiyo inasema, wewe kama chairman wa kijiji, na ni mimi ninataka kukula ile nyumba, na hakika ninajua ile nyumba ni ya fulani, nitachukua kikundi wa watu 50 niwanunulie gallon mbili ya chang’aa, halafu niwapatie elfu tano waende wakagawane, wakuje wanisimamie mimi nichukue ile nyumba. Ni haki gani inasema hivo? Haki gani inasema hivyo katika hii Kenya? Tena, sijui niseme nini, kwa maana mambo ni mengi sana hapa ya kusema, Wacha tu iishie tu hapo, tutakutana tena.

**Commissioner:** Asante Muthoni, wacha nikuhakikishie kwamba, ikiwa mtu kutoka lea atakufuata, akuulize kwa nini umesema hayo umesema mbele ya tume, joo Kencom House 2nd floor utupe habari, na sisi wenyewe tutafuata hilojambo, umeelewa? Irene Kienze, Eric Mwangi, Eric Mwangi, Mary Muthoni, Mary Muthoni, Gabriel Nyanjui, Gabriel Nyanjui,

**Gabriel Nyanjui:** Kwanza ni kushukuru, mimi ndiye naitwa Gabriel Nyanjui, yangu ile niko nayo, ya kwanza, nilikuwa nasema, ni lazima Rais apimiwe mamlaka ya kazi yake, asiwe awe anafanya kazi zote, aachie mawaziri, na ile kazi zingine zote wale wanatakiwa mpaka ile ya chini mpaka ya chief. Ya pili, tunaona police wamepewa uwezo zaidi, na ndiyo corruption

imeongezeka zaidi, kazi ya police ichunguzwe, na hii mambo ya corruption ijulikane vile inaendelea, tena hapa tunasikia tuko na masquarters, masquarter gani wanaweza kuwa katika nchi yao? Serikali impange mpango, hawa watu wanaitwa masquarters wagaiwe mashamba, tusiwe tukisema tuko na masquarters, na bali tuko na watu wako na ma-acre mingi ya mashamba, maelfu ya acres na bando ni wakenya.

Jambo hilo lingine, ni wasichana wawe wakilithi mali ya mababa zao, kama vijana, ili kuwa kama msichana amegaiwa shamba, kama hao vijana wengine, kama anaolewa anaenda anaongezana hiyo shamba na yule amemuoa, halafu inakuwa sasa mali yao. Sijui kama hapo imeeleweka? Sasa imekuwa, msichana akipatiwa mimba, anaenda anafukuzwa shule na yule kijana amempatia mimba anaedelea na masomo, sasa hiyo, ikiwa naomba kama ni kufukuzwa shule hata kijana awe anafukuzwa pia, halafu hii wanawake, inasemekana wanapata watoto hawana baba, ikiwa mwanamme amempatia mwanamke mimba, awe anasukumwa mpaka analinda huo mtoto analea, hio iwekwe nguvu. Halafu hii ya mayor, awe anachaguliwa na laiya, na ndio sasa tunaona vile anachaguliwa na macouncillors, anafurahisha macouncillors, wananyakuwa mali yote ya nchi, ndio sasa awe anaona amekalia kiti mzuri. Na tukiingilia hii mambo ya unyakuaji, ingekuwa mzuri kama mtu sasa anachaguliwa, iwe inajulikana mali yake imefika wapi. Kama sasa ni mtu amekalia kiti, mali yake ijulikane, ndio sasa akitoka kwa hio kiti, atatuelezea ile mali ingine ameongezea, amepata na njia gani., kwa sababu unaona mtu wa miaka 40, unasikia ako na mabillion ya pesa, na ukiangalia mtu wa kama miaka 40, kama ameendelea na masomo vizuri, pengine kama alipata kazi akimaliza masomo, hio ni kusema ametafuta miaka kama miaka 10, 15 yule amejaliwa kazi mapema. Na mtu kama sasa kwa hio miaka 15 ako na mabillion ya pesa, si hapo iko wizi? Hiyo tuwe tunajulizwa vile imeenda.

Halafu hii mambo ya retrenchment, ukiangalia wale watu wamekuwa retrenched, wengi wao sana ukiangalia, ni vijana, na bora wazee wamewachwa kazini? Vijana ndio wanakuwa retrenched. Sasa kama ni hiyo mambo ya kazi imekuwa chache, iwe inaangaliwa miaka, wale wamezeeka zaidi wanaenda nyumbani wanawacha vijana, halafu nao vijana wanatafuta pesa kidogo, ya kulisha familia zao. Na hii mambo ya kazi, tena imekuwa shinda, kazi sasa kama ni kazi imepatikana mahali, wewe umesomea hio kazi, umequalify, lakini huwezi pata hiyo kazi, unaulizwa experience ya miaka kama tana, na hujafanya kazi mahali, sasa hapo, vijana wetu watapata kazi kweli? Hata kama wako na qualification gani.

Sasa hiyo yangu ya mwisho, nilikuwa naomba tu kitu kama masomo, na hospitali, serikali iangalie hiyo vitu inatakiwa ipeanwe bure kwa ile kodi tunapeana yote kutoka kwa zile kazi tunafanya, iwe inasimamiwa na hiyo. Asante.

**Commissioner:** Asante sana bwana Nyanjui jiandikishe pale, na uache memorandum yako kwetu, bwana mbugua ualikuwa amewachwa mbele, tafadhali joo ukatoe maoni yako, Samuel Mbugua, halafu Benard Kamau yuko? Benard Kamau, utamfuata.

**Samuel Mbugua:** Asante sana kwa ma-commissioner wetu, majina yangu Sammy Philip Mbugua Muhinja, mimi nashukuru kwa sababu tumepewa nafasi, ya kutoa maoni yetu kuhusu katiba ya Kenya, ambayo hiki ni chombo mhimu ambacho

mwananchi wa kawaida anategemea na hata nchi mzima. Jambo ambalo mimi ningependa kusema, nitasema tu kuhusu, tunaita Public Preservation Act, Hii act imekuwa ikitumiwa na President kimakosa sana, kwa sababu leo akitaka kuleta, kudispatch GSU hapa katika hiki kijiji, watakuja, wanapiga watu, wana-rape wanawake, na wananyang'any'a. Kwa hivyo hio act ningeona, iwe reviewe, ili wakati wowote jambo likitokea, iwe ya ni lazima hilo jambo litapelekwa bunge, ionekane kama kuna haki ya kuletwa watu kama GSU hapa

Ya pili, ningetaka mamlaka ya Rais na ya mahakama na yale tuko na ya bunge, itenganishwe, Bunge iwe na kalenda yake mwenyewe,

Mahakama nayo iwe na uhuru wake wakuchagua kama ni wakili na nini, judge mkuu, mahakama nao wawe wanachaguliwa kulingana na ujuzi na hata miaka ya ufanyi kazi na record zao. Kwa sababu tunaona ya , utaona ya , maisha sio rahisi, kesho unasikia ni judge mkuu ana anakuwa ni judge wa mahakama, hali haja-practice ama hajafanya kazi ya mahakama ndogo, kwa mda fulani. Hii tena ikiwa ni judge amechaguliwa, awe anapelekwa, kama ni President amem-appoint, ana propose, aende katika committee, yaani selected committee, ambaye itahusiana, tayari itakuwa imepangwa kwa even mawakili na hata watu wengine ambao wana sifa zuri. Mtu awe anasifa jema, katika nchi,

Habari ya kuchaguliwa kwa mtawala wetu, Rais shati awe akichaguliwa moja kwa moja na wananchi, wakiwa pamoja na makamu wake, na wale ni lazima wawe na 100% ya zaidi ya 51 kwa kula zote ambazo zimepigwa.

Tena kuhusu constituency, ama mambo ya wakilishi, ni lazima igawanywe kulingana na idadi ya watu, kwa sababu, ukiona wakati ambapo kitu kama DC ililetwa, ililetwa katika district, district moja iko na shule tano, na district ingine, tuseme district kama Pokot, na Kisii, Kisii iko na shule kama 500, na Pokot kuna shule kama 20 ama 50, lakini pesa zikagawa katika ki-district, kama ni million, 3, kisii million 3, Pokot million gapi? Tatu, Kwa hivyo, resources ama wakati wa mpango wa maendeleo, iwe inapangwa kulingana na idadi ya wananchi, wala sio katika ya wilaya.

Ya pili, kuna jambo ambalo tunaongea sana wasichana, ambao tunawaita street children, Jambo ambalo, serikali inafaa kuwa naye, ni kujenga, retreation center, tena kuondoa taka taka ambazo, hawa vijana wengi wamekuwa wakitegemea, sababu tumewafanya kama nguruwe, Huyu mtoto, hiyo takataka ikiondolewa, hatakuwa na nafasi ya kwenda kuchokola huko, na ile ya , kabla hajapelekwa shule, kujiunga na watoto wengine, awe amewekwa chini ya wagali retreation, awe tabia yake amekuwa conciled, ili ikiingia kwa shule, aweze kuwapatana na watoto wengine, hilo litakuwa ni jambo la serikali, kuhusu informal schools ambazo ziko hapa, City Council inawajibu, kwa kuwa inazigawia pesa kwa sababu ni jukumu yao kufanya hiyo kazi. Sio jukumu ya mwananchi wa kawaida, lakini ni kwa sababu katika mipango yao, ya mji walipanga kimakosa, na hilo jambo liandikwe hata katika katiba yetu ijao iwe ni namna hiyo.

Ya pili, kuna kitu ambayo tunaona ya , police wetu, they are very corrupt, lakini hata sisi wenyewe, katiba tutaunda mzuri sana

lakini hapa katiba inaweza kuwandikwa kwa sisi wananchi wa kawaida, ili hata wewe ujue haki yako. Usiwe unategemea ya kila pahali,unaenda ni pesa utapeana, sababu saa hii tunapeana maoni, nawewe jioni unaelekew Kinyago na shilling elfu moja, unataka huyu asikwe. Unaona, hivyo na ikiwa hilo jambo litakoma lazima tuwe na kitu kinaitwa civil police, wakisaidiana na police ambao wako hapa. Hawa civil police, wanajua tabia ya watoto na vijana. Kabla ya mtu kupelekwa police, kuna kamati ambayo anafaa kuwa inachunguza, huyo mtu. Mimi ningeonelea, kila constituency, iwe ina mtu anaitwa attorney, ambaye amekuwa appointed kutoka office ya mkuu wa sheria, kwa sababu, police asipochukua hatua, yule wa pili kutoka kwa office ya mkuu wa sheria, ana haki ya kuchukua malalamiko, ile achunguze, na amuru huyu mtu asitakiwe. Lakini sasa hatuna hiyo jia, so hiyo iwe katika katiba.

**Commissioner:** Last Point.

**Samuel:** Hebu tuangalie kitu tunaita elimu, elimu nimeguzia, hio hata siwezi kurudia. Tuone kitu kinaitwa health care, tuwe, hizi pesa ambazo, wafanyikazi, kama mimi ninatoa kwa National Hospital Insurance Fund, siwe zinaweza kusaidia wananchi wa kawaida, kwa sababu ni insurance, Na hiyo pesa hazitumii, na sisi watu ambao tunachanga. Lakini unakuta zimechukuliwa, zinakopeshwa watu ambao hawachangii. Kwa hivyo hizo pesa, zinaweza kutumiwa kusaidia mwananchi wote wa kawaida, ambaye hajiwezi, hilo ni jambo mhimu. Kuna hii NSSF. Hizo pesa ziwe zinachaguliwa managers ambao wanachanga hizo pesa. Kwa hivyo hizi pesa zinaweza kutumiwa kusaidia mwananchi wote wa kawaida, ambaye hajiwezi, Hilo ni jambo mhimu. Kuna hii NSSF, hizo pesa, ziwe zinachaguliwa managers, ambao wananchanga hizo pesa, na hio uwe mchango, faida yake, inaweza kusaidia wakongwe, ambao hawakuwa na kazi, na watu ambao hawajiwezi. Badala ya iwe ikikopeshwa watu matajiri, wanafanyia biashara, lakini iwe inachukuliwa kusaidia kama watu wakongwe. Na hapo hivo iwe kama pension ambapo watu wanaweza kuwa wanapata nini? Wanalipwa bada ya kuwa wazee, badala ya kuwa inatumiwa hovyo hovyo. Hayo ndio maoni yangu na nimeshukuru sana.

**Commissioner:** Asante sana bwana Mbugua, jiadikishe pale, goja, kuna swali,

**Commissioner Salome:** Asante sana bwana Sammy Mbugua, kwa maoni yako, mimi nina swali kwako, umetueleza kuwa ingetakiwa kila kikao cha bunge, kufanywa usawa, inalingana na watu wenye wanaishi pale, sasa pahali kama hapa Dandora, ama Embakasi, kila mtu anakaa karibu karibu, MP akija kutoka asubuhi mpaka jioni, atakuwa amefika kona zote za constituency yake, kuna pengine MP mwingine mwenye yuko Madela, kitabo aone watu wake, na hizi mvua, na barabara mbaya, inamchukua kume, sasa naona tukisema lazima watu wakuwe usawa, kule kwenye ubari wa watu wamekaa bari bari tutatumia je? Ama tutatumia xxxx vipi kuwahusisha wale wananchi, kwani pia hao ni wananchi wa Kenya?

**Mbugua:** Mimi nimesema, ya kila jibo ya wakilishi, liangaliwe kulingana na idadi ya watu kwa sababu ya kugawa lasimari ya nchi, kwa sababu utakuta, ya , nafikiri sasa mimi ninaishi North Eastern, ukichukuwa kutoka area moja kufika ile ingine, au kwa ufupi ni maili thelathini, lakini ukiangalia idadi ya watu ni wachache sana. Nimepeana mfano Pokot, ituchukuwe, kuna

constituency moja na Kisii, tuchukuwa Nyaribari chache, na hao watu wakati serikali inagawa pesa, imegawa Nyaribari chache ikawapatia million mia moja, na kule West Pokot, tuseme kama central wamepewa million mia moja, wananchi wa kawaida ambao wako kule Kisii, je hio mugao ukigawa utakuwa sawasawa? Hauwezi kuwa sawasawa. Ndio nimesema, rasimali zigawiwe kulingana na idadi ya watu, wala sio ukubwa wa ardhi.

**Commissioner**: Asante Bwana Mbugua kwa maoni yako, neenda ujiandikishe. Michael Ngajo, Michael Ngajo, Waaweru Gichimo, utamfuata.

**Michael Njogu:** Good evening, yangu ni machache, nataka kuongea juu ya employment. Kitu ya kwanza tunajua, tuna vijana wengi sana hawana kazi, kwa hii nchi yetu, na nimeonelea ya serikali yetu imeharibu international relations, ya , siku hizi vijana wakitaka kwenda America, wanaitishwa visas, wakitaka kwenda Britain, ni visa, na wakati huu ukienda Britain, utakuta kwa notice board, wanaadika vacancy, wanataka wafanyikazi, na hapa kwetu Kenya, tuna watu wengi hawana kazi, kwa hivyo ningetaka tuseme ya , the employment act tuseme nchi yetu ya Kenya ianze ku-export labour, from today, na wale youth wote hawana kazi, graduates, certificates, wote within a ward wanaenda wanaenda wanajiadikisha pahali, hao vijana, majina yao inakuwa put in a website, tuko na international website ya makazi, ili nchi zingine kama Namibia, ili kama hii tulikuwa nayo ya meli, inaitwa je? Ni cruise ship, isitokee. Ili ikiwa ni Namibia wanataka waalimu, wanaend kwa hiyo website, hiyo website iko na jina ya mtu, amesoma mpaka wapi, ili huo mtu akitumwa serikali pia iwe inapata tax yake pale.

Ya pili, ningetaka kuongea ni kuhusu, manene ya street children, street children is a making of the society, hakuna mtoto wa barabara, watoto wote tunajua wana wazazi, na ile survey sisi tumefanya, tumeona ya 98% ya street children, wako na relatives ama mzazi ama guardian. Na ile kitu iko, tunajua watoto siku hizi wanatumiwa kama biashara, ukiwa na watoto tisa, uambie mmoja chukua Kenyatta Avenue, chukua shilingi shilingi, mwingine chukua Moi, Kauda, jioni wanakuletea pesa gapi? Si ni mingi. Tungetaka serikali ifanye hivi, under the childrens act, sijui kama tuta-interest kwa constitution, tufanye census, tuhesabu watoto wote wa street children tuwapatia registration certificates na ID, na wazazi wao tuwaite. Na sababu tunajue our children officers most of them are corrupt, tutumie the new act. Ikuwa Mzazi ameachilia mtoto kweda barabarani apelekwe jera afungwe miezi sita. Hakuna mtoto wa barabara. Na hiyo tutamaliza.

Ya tatu, tunaongea maneno ya slums, slums are the making of the chiefs, slums zinatengenezwa na machiefs, na hiyo, I have worked in slums for many years, na ninajua chief akipelekwa katika pahali hakuna kiwaja ya kuuza, hataki. Chief akiambiwa machief wote Nairobi mzima wanapigania wakuje Embakasi, kwa sababu Embakai iko area ya kukula. Chief akipelekwa Karen, hio hata ni mateso, afadhali atafanya harambee apelekee DC. Ya kwanza, ningetaka tufanye hivi, serikali under the housing act, ama the land act, wahesabu watu wote wa slums ni wagapi, na watu wa slums semeni kama hapa KCC kunapeanwa shamba hapa, kuna acre sijui City Council inachukua 30 acres, zile zingine 60 wanataka kukula, hiyo tunajua. Na ile kitu ningetaka kusema, 3rd Mau mau, 2nd mau mau in Kenya will come from the slums, na challenge is this the commissioners, can you go direct in the slums in Embakasi, we have about 4 slums, mchoose kwa hao watu, because I know they are suffering

so much. I have worked there for over 13 years and I know what is going on there. Ile ningetaka kusema ya slums ni hii moja, Can the government form a commission on slums immediately, wahesabu hawa watu na wale watu wako kwa slums, we know there are landlords, there are landlord tenants,and there are tenants. Ikiwa mtu ni tajiri na ako na manyumba huku tutupe huyo, asipewe, lakini masikini apewe kiwaja. Ya pili, slums ili ikwishe, mtu akipewa ata kama ni pale KICC, hio plot asiuze.I know there are donors who are willing to fund housing projects, kama World Bank, IMC, wakipewa ile kiwaja pale, kwa sababu tunajua watu wale walikuwa kibagara walienda kutengeneza soweto. Saa hii KICC wakigawiwa na City Council, watauza, wataenda kutengeneza slums zingine Ruai.. So ni vita ya paka na panya in the slum village issue. Kwa hivyo serikali lazima with immediate effect form commission on that, if not so, let me tell you they are naturing problems. Ya pili, I know slum villages are the havens for the Members of Parliament. Wanajua kula hutokanga kwa slum villages, hata ma-councillors, kwa hivyo they are happy when they are many slum villages ili waendelee kuexploit people. We also know NGOs are commercializing poverty in the slum villages, under the disguise of community development. Hiyo ni kitu ingine tuangalie.

Ya tatu, corruption, corruption is in our blood in this country, we know accounter changes after thirty years, nakuambia this country, hata wale watoto tunazaa, hata watu wale wanaajiriwa leo, ukiajiria mtu kazi kitu ya kwanza ni kuuliza, am I controlling petty cash, is there any money, is there anything? Ya kwanza, I'm saying all civil servants should declare their wealth, all of them, they should declare their wealth. Ukiajiriwa, tuseme, nimeajiriwa leo I have only one plot nimepewa na baba yangu, because we know, you have a case of a magistrate juzi alimpeleka his visitors at Grand Regency, one day lunch akatumia 3 million, a judge in the high court, 3 million treating people, hiyo 3 million anaitoa wapi? Ya kwanza siku hizi my friend if you do not have money don't go to the courts, we know the courts, watu wale wako jera saa hizi, 90% are innocent. 90% of prisoners in Kenya are innocent.

Ya tatu, ningetaka police station iko hapa Kinyago, inatakiwa ihamishwe immediately, because I have realized, tukiitoa hapo, criminality itakuja chini, sababu asikali wa siku hizi tunajua wanajua tu kuzurura tu hapo phase I wakiitisha watu pesa, wale askali wazuri wakiletwa pale buruburu, OCPD anahamishwa within one month. Tulikuwa na mzuri sana alikuwa anaitwa Muchacha, alitolewa because he wanted to finish those businesses.

Ya mwisho, political parties, this country only requires 3 political parties, the more political parties we have, the more problems we are creating and I'm seing us heading to the Rwanda situation. Sababu zile parties tuko nazo sasa, ni za kikabila. Tukiwa na parties 3, three strong parties, who should be funded by the government, life would be better. I'm very sure and I want to thank you commissioners, I know you are going to make the best constitution in the world with your support because it will be inclusive and I'm happy with your work.

**Commissioner:** Thank you very much Michael, please register at the back and give your views. Dan Lumumba,

**Waweru Gichimo:** Asanteni sana ma-commissioners wetu na wana Dandora wenzangu, Kwangu hii ni siku mhimu sana kwa

sababu katiba ilikuwa imesemekana, sio ya Wanjiku, katiba ilikuwa imesemekana ni ya bunge, na kwangu kwa leo is a dream come true. Kwa sababu sikujithania labda siku moja nitaweza kukaa mbele ya kikao kama hiki, na niweze kutoa maoni.

Kwanza kabisa, yangu ni mambo kama matano hivi, ya kwanza ni , ningependekeza ili katiba ambayo tutakuwa nayo, iwe na kitangulizi (preamble) . Ninapoenda kwa makitaba kuangalia angalia katiba zingine, na nchi zingine za nje, kwa sababu we cannot leave in isolation, mimi nilipata ya, katiba zingine ambazo, wenye nchi fulani waliwahi kujitengenezea, lazima inakuwa na kitangulizi ama preable, kwa kimombo, ni maneno machach amaye kwa ufupi, huelezea philosophia ya kugawa mamlaka, kuanzia juu mpaka chini, kwa hivyo hiyo preamble nimeiandika ni taifoward kwa commissioners na nina hakika ya wataifikisha vile ilivyo. Ya pili, sana sana mimi ningependelea kuona ile katiba ambao tutatengeneza, ikimpunguzia, Rais wa nchi yetu mamlaka sana. Kwa sababu ninaamini ya , ile shinda kubwa ambayo tuko nayo, kwa wakati huu, haijatokana na wananchi wenyewe kutofanya kazi kwa bidii, haijatokana na labda waalimu, kutotii sheria na kufunza watoto kwa bidii, bali imetokana na kitu ambacho kinaitwa hii office ya Executive Office. Nitatoa mfano, wa nyungu ya Kiafrica, tunapowekelea nyungu yetu pale kwenye mawa tatu, si lazima mawe zote huwa zinatoshana? Ikiwa mawe moja itakuwa kubwa, basi ni kumaanisha ya ile nyungu italala pande moja, itamwaga zile chakula na kumaanisha hiyo chakula basi haitaifa maanake ile moto itazimika. Kwa hivyo, Presidential, yani hii executive office, kuonya mamlaka yote ama serikali yeyote ambayo imara, lazima tuwe na executive, lazima tuwe na judiciary, ambayo ni ma-court yetu, na ya tatu tuwe na Parliament yetu, lakini inavyo onekana ni , hata kwenye hii katiba mzee hii, ukiiangalia, utathania ya , kule ilitoka, wale watu waliokuwa wakiitengeneza walionekana sisi labda siku moja, kama ya leo, hatutaweza kujiuliza, hii katiba ilitoka wapi? Kwa sababu, inaonyesha ya , Rais ndiye presiden amepewa mamlaka mengi sana. Rais inasemekana ako above the law. Ningependelea ile katika tutakayo itengeneza, iwe Rais asiwe juu ya sheria, nobody should be above the law. Na hii pia tukuwe na provision ya impeachment, ya Rais akifanya jambo, lolote ambao wananchi huenda wakaona, si la manufaa kwao, waweze kuuliza yale maswali kupitia kwa bunge na basi hata kama ni kula ikutokuwa na imani, itolewe, kwa hivyo, maoni yangu hapa, kuhusu uRais, ile katiba tutakuwa nayo, mamulaka yagawanwe, kwa usawa. Kama ni ma-court zetu, ziwe ni ma-court ambazo zitakuwa independent, uamuzi wake wakuheshimika na wananchi wa nchi hii, na labda kama vile mnenaji moja amesema ya , ma-court zetu kwa wakati huu, zikitoa uamuzi, court of appeal inaonekana ina kazi mingi sana kwa sababu, huyu, huyu Rais, ambaye nimeongea amepewa madaraka mengi sana, ndiye huwa na jukumu la kuwateuwa judges, na judges mara mingi utaona atawateuwa kulingana na urafiki, wa kijaluo, hivyo ni , huenda ikawa yule judge atakayeshikilia, mamlaka ya kuongoza kesi yako, si judge ambaye ana ile ujuzi wa kukaa na kuamua kesi kwa court yeyeto ile. Na hivo hivo, ndivyo pia kazi inapofika ya kuteuwa mawaziri wetu. Unaona ya mawaziri wengi wale tuko nao, infact hata hawafaii kuwa pale kabisa, lakini kwa sababu mamlaka ya Rais hakuna mtu anaweza kuuliza decree, kama leo nikisema, huyu ndiye atakuwa waziri wa energy, hata kama hajui lolote kuhusu energy, hata kama wewe ni daktari, lakini so long as President amesema ndiye atakuwa waziri wa energy, atapewa hicho kiti, na huku yeye labda alikuwa amesomea ufugaji. Kwa hivyo, kama ni uteuwaji wa mawaziri wetu, ningependelea labda mawaziri na ma-judge wetu – hawa ni watu ambao tunawahesimu sana, hiyo kazi ipewe bunge, kuwe na kamati maalum ya kuchunguza na kuhakikisha ya , wale wanaoteuliwa majina yao hayajakuwa kwenye uharifu wakati mmoja au mwingine.

**Commissioner:** Last two points please

**Waweru:** Jambo la hilo lugha ambayo tutatumia kuandika hii katiba, iwe ni lugha ya kueleweka. Tafadhali hatuna haja ya kutumia lugha ambayo inaeleweka tu na mawakili, na wale watu ambao wanaitwa ewrite au wasomaji.

Jambo la nne, ni kuhusu electral commission yetu, namna electral commission yetu itakavyo tengenezwa na katiba tutakayo iandika. Tafadhali, kawaida ya ile katiba tuko nayo ni , electral commissioners wote wanateuliwa na Rais isipokuwa juzi, wawe wakiteuliwa na Rais, ile kazi wametufanyia, tumeiona, kwa hivyo, once bitten twice shy. Hatungependa, ya , Rais awe akituteulia ma-commissioners wale wanasimamia uchaguzi. Tungependa ya , wale ma-commissioners wa electral commission, wawe wanachaguliwa na vyama vyote vya kisiasa.

Ya mwisha pia, ni provision ya coalition government. Tuwe na provision ya coalition government kwenya katiba mpya ambayo tutakuwa nayo. Na ya mwisho kabisa, ni kuhusu kura ambazo Rais tutakaomhitaji, tungetaka awe amepita na kura kiasi gani? 51% majority, na ile round ya kwanza, kama basi haitawezekana, kuwe na candidate ambaye atakuwa amepata hio 51% basi kuwe na runoff. Asanteni sana na Mungu awambariki. Nina swali kwa ma-commissioners, mwisho kabisa.

**Commissioner:** mwisho kabisa kabisa kabisa,

Waweru: Ni tumesoma kwa magazeti na na vyombo vya habari, electronic media, ya mda ambao muliitisha wa kutengeneza katiba, huenda usiwe wa kutosha. Na tuna mengi yameandikwa, je nilikuwa na jiuliza hapa, Chairman wa commission anasema you are on track, na wengine wanasema hapana, tunahitaji kuongezewa muda, tutaamini lipi tukose kuamini lipi? Asanteni.

**Commissioner Lenaola:** Asante bwana Waweru, keti hapo ni kujibu, usiende mbali kwanza, sababu lazima nikujibu. Asante kwa swali lako, kawaida katika mikutana kama hii yakuchukua maoni, hatuchukui maswali, wala hatujibu, lakini kwa maana swali ni lamaana, nafikiri ni vizuri kukujibu. Tume imeamua kwa mpangilio wake, kuangalie sheria ambaye imetuma tume, hatuwezi maliza kazi kabla December mwaka huu, na tunafuata sheria sana ambayo inasema kuna vitu fulani, lazima tufanye, tukaona kwanza, kama ni lazima kila mkenya atahushwa na hii kazi ya kutuma katiba, na kama ni lazima sisi kama tuwe tufanyie kazi ya kutuma katiba, ni wajibu yetu lazima hii kazi ifanyike bila kuwa na kazi supu supu haijaifa vizuri, tukasema , ikifika mwezi wa tatu, kazi itakuwa imeisha. Chairman wa tume hajasema yeye mwenyewe atamaliza kazi kabla ya October, alisema kabla kuna vitu fulani ambavyo lazima ifanye by October. Kwa hivyo sisi wote wanatume, 29, akiwako Attorney General wa nchi, Amos Wako, tumeona kazi itaisha peke yake mwezi wa tatu mwaka ujao, lakini, ikiwa bunge, itaenda itoe vitu fulani kutoka Act, kwa mfano, baada ya sisi kuandika hii report ya Embakasi Constituency, itarudi tena kwa nani? Kwenu, Baada ya katiba kuandikwa katika draft, ile draft constitution, lazima irudi tena wapi? Kwenu, muingalie kama mambo yenu yame? Yameandikwa. Lakini bunge inasema , mambo kama hayo, katiba irundi kwenu muangalie kama mambo yenu yameandikwa, mambo ya report ya constituency, wamesema hiyo itolewe kutoka wapi? Kwa sheria. Ili by October mwaka huu, baada ya draft ya kwanza kutoka, na bila hiyo kurudi kwenu, wapeleke wapi? Wapeleke bunge ama liishie bunge?

Tukasema sisi wanatume, hatukuchaguliwa kufanya kazi nusu, nikiwaambia mtupatie comprehensive, review of the? Constitution. Kwa hivyo ni hayo tu. Kwa mambo ya magazeti, mambo ya kusema sijui nini, hayako kwa tume. Tumeelewana bwana waweru? Kwa hivyo mambo ya magazeti nimeyasikia, umeyasikia yetu. Mlitupatia kazi kufanya, mpaka tufanye nini? Kazi safi, hapana ugali umeweka maji, maji imechemka ukaongeza unga ukatoa. Na unga hii ugali maneno yao ambao mnasema tax, na kama huu unga haujaifa, tunawambia chukueni mkakule, mtakula? Basi ni hayo, bwana lumumba, Wilson Juma James,

**Dan Lumumba:** kwa commissioner, na watu wa Dandora nyote nimewashukuru sana, kwa majina naitwa Dan Lumumba Mito, sitaongea mengi sana, bali nitaguzia tu machache, kwanza kuna mambo ya mhimu sana ambaye inatusumbua, sio sisi wakaaji wa Dandora peke yetu, ni wakenya, hiyo ni police harassment, kwanza mimi sijui kama aliandikwa kazi ya police ili akuje ahangaishe laiya wa nchi, hiyo kitu huwa inanisumbua sana na ina tatizo sana.

Ya pili nasikia watu wanalalamika juu ya Presidential powers, juzi juzi nilipitia kati ya hawa wabunge, viongozi wetu wakisema wanataka wafanye uchaguzi, mwanzo walikuwa wanataka mambo ya katiba, kisa baadaye sasa waligeuka, wakasema wanataka uchaguzi kwanza ndio wafanye mambo ya katiba, sasa hii kusema tu ukweli inaonekana kuna mambo fulani inaendelea, labda tunandanganywa na watu wetu, labda kuna siri ingine hawa viongozi wako nayo ambaye sisi hatujui. Juu tukiambiwa tulekebishe katiba, punde si punde, unaambiwa apana ngojea kwanza tufanye uchaguzi. Na saa hii unasikia, wanasema, hawa watu wakubadirisha katiba yaani commissioners, wasipewe muda wamalize hii kazi, je, hawa watu msimamo wao, ni upi?

Ya tatu, ni mambo ya judiciary, unajua hapa kotini makoti zetu siku hizi unakuta ni kama biashara, unakuta kesi imeenda kotini, hata vile inafuatwa, hata huelewi, mtu anakaa kwa cell, anarudishwa kotini, ni kama tu ceremonial reporting, imekuwa ni kama mchezo tu, mtu anakuja kotini hata ile ilimuleta kotini hata huoni.

Ya nne, inafaa serikali yetu iangalie vile wananchi wa Kenya wanaishi, hizi manyumba, sijui kama serikali haikuwa na mpango, hapo mbeleni, hata ukiona vile sisi tunaishi, ni style ingine mbovu sana. Kwa hivyo ningependa serikali yetu iangalie, vile sisi wenyewe tunaishi. Watupangie njia ya kuishi.

Mbele la hiyo, mimi ningeiguzia mambo ya tusema mambo ya plots that housing, unakuta watu wengine, wachache wameishi vizuri sana na wengi wanaishi kwa hali ambapo hata ukiangalia wewe mwenyewe unasema, hawa, kweli sio wakenya. Wanaweza kuwa ni refugees, wametoka nchi fulani, kwa hivyo serikali ya Kenya inafaa iangalie mambo ya housing, wapange (serikali ) ipange vile watu wake wanaishi, kuna hii kitu (kwangu mimi naweza sema ni illegal exportation. Unakuta mtu ananunua sukali kutoka nje, na hapa kwetu tuka na sukali zimejaa kwa store. Mtu anatoa mchele kutoka ng'abo, kuitwa hapa mchele imejaa kwa store. Hii mchele inatoka ng'ambo ama hii sukali imetoka ng'ambo? Sijui ndiyo tamu sana kuliko hii yetu. Halaru unakuta, kuna taxes ambao zinafaa zilipwe hapa, kwa airport ama parts na unakuta mchaache, kuna madugu zetu

wengine hata wachache hawalipi hata hazi taxes. Naunakuta hii sukali yetu sasa inajaa kwa store na inaharibika hapa, ama mchele, na sisi tunalia hati hakuna chakula sijui bei ya sukali imepanda, natuko na sukali hapa na inaharibiwa tu na serikali. Ningependekeza hiyo pia serikali iangalie.

**Tape 6**

Unakuta mtu moja ako na kazi kama kumi na sisi wakenya tunalia hakuna kazi, je hata ukimwambia yule mzungu unamuuliza uende ukafanye kazi kwao, atakuuliza na je, Mr. X ako na kazi kumi, na watu wengine hawana kazi, je unaniambia ukweli ama unani enjoy? Haya, tulipopata uhuru, kuna mambo mingi yaliguza, mambo kama masomo, mambo kama mambo ya hospitali, mambo kama housing, na serikali pengine walikuwa wanataka tu uongozi, yaani uhuru, juu ata hii katiba ilitengenezwa ilichukuwa mda mfupi sana, ndio walisema ati walikuwa wanakibiza uhuru. Ndio walikuwa wanakibiza uhuru, lakini, mambo kama elimu, ilikuwa je kwa sababu walisema elimu itakuwa ni bure kutoka standard one upto standard 7.ilikuwa je? Mambo ya hospitali, ilikuwa namna gani, mpaka unakuta mtu ambaye hajiwezi anakufa tu ata kwa sababu ya homa. Ni nini inaendelea mbaya hapa Kenya?

Tuko na mambo ya wakulima, Agricultural sector, si ninafikiria serikali inaweza tenganeza pesa kiasi fulani, yakununua pengine bolea, mbegu, mimi nilikuwa naonelea ya bolea, begu na vitu zingine kama pumps, kuna area zingine ambayo lazima watumie pumps, ndio maji ifike kwa shamba, mambo kama haya serikali inafaa ipewe wakulima bure ili tupate chakula sawasawa,

**Commissioner:** Last point please,

**Dan Lumumba:** Katiba ya Kenya hata tuite wazungu, watoke ng'ambo wakuje watutengenezee watuundie katiba ile safi, haiwezi ikafanya kazi kama sisi wakenya hatuwezi tukakubari kufuata katiba yetu. Kama hatuwezi kubari, kufuata sheria yetu, hata hii tuko hapa, tunajaribu kutoa maoni ni kazi bure. Unakuta hata police ambaye amepewa mamlaka ya kuambalia serikali imefuatwa, na kuna utulifi, ndio ana-behave kama mtoto ambaye hajakanyanga shule, Kwa hivyo ningewaomba, tume muangalie hii maneno kabisa kabisa baada ya hii katika ifanye kazi, ifuatwe vizuri, hata mambo ya kusema ati powers of the President, those are nothing. Kwa hivyo asanteni.

Commissioner Lenaola: Asante sana Dan, tunajaribu kufanya hivyo, jiandikishe pale, kama hatukuwa tunafikiri ni katiba nzuri, hatungeketi hapa tangu asubuhi. Ben Mtu wa mwisho, toa point zako speed tatu halafu uende ujiandikishe.

Benard Kamau: Asante kwa officer ambao wametumwa hapa kwa, Asante kwa maofficer, na wanadandora, nimepewa nafasi hii ambayo ni wakati mwingi ilinisubua nikijiuliza, nitafika parali kama hapa ni ulize maswali ambayo inanisubua kwa kichwa ama ni gani. Hapa sisi, mimi ni Benard Kamau mwangi, hio kitu imenisubua wakati mrefu sana kwa kujiuliza kama mimi nina uhaki wa kuishi ama sina. Katika hii Dandora nimekaa, huu ni muaka wa ishilini, katika Dandora hii, mimi naonekana kijana lakini yale maisha nimekula huku, nikiyataja, ni ya kusubuka, vile mnasema kulikuwa na dumping, vile mnasema kuna dumping, imenikuta nikiwa hapa. Kwa hivyo serikali imeanzia kuharibikia juu, mpaka chini, na sisi wenyewe ndiye tumeiharibu, kwa kuwa, kama

sasa tulikuwa na ma-officer wa city council, wakati wa mwanzo, ambao walikuwa wametenga sehemu ambayo inahitajika, yaani inaliza mwana Dandora lakini sasa hakuna.

Katika Dandora hii tumepewa police station, hapa Kinyago, zamani tulikuwa na moja pale Ruaraka, ndio police yetu ilikuwa, wakati ilikuwa police ni moja, hatukuwa tunasuburiwa kama wakati huu. Police amepewa mamlaka, sijui kama ni sisi tumemuajiri ama ni yeye ametuajiri, kwa hivyo, askali ameenda juu zaidi kwa kupewa mamlaka na Rais, na nikitaja hayo, nimeyaona, nao wenye wanarithi katika hizi mnasema ati ni grabbing, yule amewapa mamlaka ni officer kutoka kwa city council, ndio apate malupulupu kutoka kwa wadogo wake. Kwa sasa, katika hii Dandora, kulikuwa na ma-open spaces, yote imejengwa. Katika Embakasi hili, hakukuwa na dumping pahali popote, ililetwa na hii kwale zilikuwa zinachimbwa, ya kudump, sasa imezidi imekuja mpaka kwa maplots, ukiingia kwa plot, hata yaale ma-sewage yalikuwa yametengenezwa yameharibiwa na hiyo dumping. Kwa hivyo, serikali, imeharibikia juu kwa kupewa kwa Rais mamlaka ambayo hata yeye mwenyewe imemshinda. Ikafika kwa mwananchi wa kawaida, naye amejichukulia mamlaka kuzidi yale yanaweza. Nikitaja hayo, katika vijiji, kuna chairman, ambaye amejuchukulia mamlaka, anasema yeye ni chairman, anakula pahali ako, yote anamaliza. Police naye akiwa pale, OCS, mwenye amesimama pale, yeye ndiye kiye kichwa yake, nayeye ndiye muajiri wake. OCS ndiye analinda askali, akuje aku-harass kwa ajiri ukimpelekea report, kama alipelekewa kitu, hatakuchukuwa kama wewe ni mwanadamu.

**Commissioner Lenaola**: Point ya mwisho,

**Kamau:** Mimi yangu, maoni yangu, katiba ambayo inafaa, kutengenezwa wakati huu, ni ya kunyima ambayo ni tajiri yule ameajiriwa, na muwajiri, watenganizwe kabisa, kama ni Rais, akichaguliwa na laiya, maoni yakumuendesha yatoke kwa laiya. Kama ni askali, ameajiriwa kwa police station ambayo ni commada, maoni asitoe kwa police, atoe kwa laiya. Hayo tu ndio ningeona.

**Commissioner Linaola:** Asante sana bwana Kamau kwa maoni yako. Neenda pale ujiandikishe, nashukuru kwa yale umeyasona. Itanibidi sasa kufunga kikao. Tumeshukuru kwa wale wamekuja, tumeshukuru kwa maoni yenu, na kesho tutakuwa Mukuru Kwa Njenga, pia katika Embakasi constituency na kabla sijaomba tupatiwe maombi, tungetaka kumwambia muzee atuambie yale ako nayo, halafu tufunge mkutano.

Basi commissioners, mimi yangu ni machache sana, kwa wale hawakuwa hapa asubuhi, mimi naitwa Raphael Thimbo, ni mmoja wa kamati ya constituency ya katiba, tuko kumi, wengine wameondoka, na wengine hapa wamembaki,lakini mkubuke, mimi nataka kushukuru ma-commissioners hawa walikuja saa mbili, hata ingawa watu hawakuwa wengi, lakini nafikiri wameenda na maneno mengi kuliko watu, ama si namna hiyo? Watu walikuwa wachache, lakini maoni, paper work ile nimeona wamechukua ni asante sana kwa watu wa Dandora. Ya mwisho, kuna watu wana commissioners, tulisoma civic education, kitambo pale, wale tulikuwa catholic for 4 days, watu wa Embakasi nafikiri ndio walifanya vizuri sana, ni vizuri tujishukuru hivo, sisi tulifanya

mambo ya civic education without even a single cents from the commission, lakini wakipate lazima watatupatia, hiyo hatutaiongea kwa sasa, tutaenda kwa office zao. Kwa hivyo, kuna wale watu tulisoma karibu 400 ambao ndio training of trainers. Walikuwa wamejitayarisha, na tulionelea under Embakasi Development Consortium, ambayo ni kikundi kilijiunga wakati mambo ya civic education ilianza, wamejaribu sana, mpaka wametengeneza at least kakaratasi, nafikiri ni ya maana, kuonyesha, wale walio-participate, walifanya kazi na walisoma, ili wawe ready kusomesha wengine. Civic Education nafikiri commissioners zitaendelea, itaendelea kwa munda mrefu, sio kusema ati mkimaliza kazi ati civic education inaisha, lazima watu wetu waelimishwe. Kwa hivyo, ile ingine kabla hatujapeana hii certificate, wale hawatasikia jina lao hapa, consortium ingali itatengeneza hizo zimembaki na wanaweza kuja pale office-ni kwangu, pale karibu terminus, wakiuliza office ya Thimba, hapo, si ya chairman, ya Thimba, watakuja watapata certificate zao hapo. Kwa hivyo, ile ingine, coordinator bwana Maina, ako hapa, amejaribu sana kuleta vitabu inaohusu katiba, vitabu chache chache, na tulifungua library kwa hio office, mtu yeyote angetaka kunja kuelimika kidogo, na mambo ya katiba, anaweza kuja pale achukuwe kitabu, aende asome within a week or two, halafu arundishe, ndio mwingine apate kuchukua. Kwa sababu si nyingi. Kwa hivyo every working day, mtu anaweza kuja pale na achukuwe kile kitabu na aende ajielimishe, ili ajue anatengeneza katiba ya aina gani. Basi nafikiri kwa hayo machache, na ma-commissioners wako hapa, ningewauliza, wale watasikia jina lao, tutapeana chache, hizo zingine wenyewe watachukuwa pale, ili tufupishe mda, ma-commissioners wako hapa, wapeane hizo certificates, ili wale waliosoma, kweli wajulikane walifanya nini? Walisoma. Basi, bila kupotesha wakati mwingi, tunataka Mary Achieng, kama ako aje hapa, na tufanye haraka kidogo, halafu Teresia Kinyua, afuate, Edward Omolo, hawa ni wale walimaliza training ya 4 days, thank you very much Elimina Mwimali, Beth Nyambura, Grace Murage, Sarah Hamed, Lydia mramba, afuate number nane, Anne Wanyoike, nilimuona hapa sijui kama ameodoka, Anne Wanyoike, Mary Muthoni, nafikiri Mary Muthoni ako, Mary Muthoni afuate Lydia, Cathrene Kutukulu, Cathrene, haya, fuata hapo, na mwisho ni yule mtu alikuwa anaitwa Samuel Muhinja. Yule alikuwa anatoa maoni hapa, ameodoka? Basi, kwa hayo machache, wale wamebaki, watakuja kuchukua hizo certificates pale, na kwa hayo machache ningeshukuru ma-commissioners, tumeona maajabu leo, mkutano wetu leo umeenda vizuri, na wale vijana, ambaye tulimbaki hapa wa kijiji, tubaki ndio turudishe hii viti. Kwa hayo machache, thank you very much .

**Commissioner Lenaola:** Ningepeda tuombewe Mungu na mzee wetu hapa, asimame atuombee Mungu..

**Mzee:** Asanteni ma-commissioners, kwa kazi nzuri ya siku ya leo, moja tumshukuru Mungu, mtu ako na kofia yake, anaweza kutoa, tuinamishe nyuso zetu ili turudishe shukulani kwa mwenyezi Mungu.

Asante sana, baba Mungu wa binguni, ni kwa sababu ni katika uwezo wako mambo yote hutedeka, tunajua kabisa kabisa, baba wewe usipojenga nyumba, binadamu kujenga ni kazi ya bure, na sasa tuko katika muongozo wa kujenga nyumba yetu na tunakualika katika muongozo huu, tunajua tulikualika tangu kitabo baba, na ulikuwa ukienenda na sisi kwa kila pangilio lolote na kwa kila agenda yeyote tumewahi kuzugumzia, na tunajua ya , tutakapomalizia utakuwa pamoja na sisi, na katiba yetu itakuwa ya kulida nchi yetu kuleta amani, tunajua ni kwa sababu ya maofu ya shetani, mambo mengi huwa imetokea hapa na pale, umwagaji wa damu, lakini kwa sababu wewe uko pamoja na sisi, na pia unasikiza malilio yetu baba, tunajua, utalida na hayo

yote ya muofu shetani. Sasa tunakurudishia shukurani kwa sababu ya kuwa mwenye kiti wa mkutano wa leo, kutokea asubuhi, baba saa mbili asubuhi mpaka sasa imeedelea kufika saa kumi na moja, tumeuona mkono wako kwa sababu hatujapata furugu ya kina yeyote, hatujapata maradhi ya aina yeyote, wala hatujawahi kusikia jaa, tumefumilia mpaka joto ya jua baba, lakini ni kwa sababu ya uwezo wako baba. Twakushukuru na tunajua ya utaodoka pamoja na sisi, mkutano umefunga pamoja na sisi, utatulinda na yote tutakayo pata mema, tutakushukuru na kukurudishia shukurani, Asante sana tunaomba kwa Jina la Yesu tukiamini utatenda, tumeomba na kuamini. **Amen.**

The meeting ended at 5.00 PM

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**